## BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Tano – Tarehe 16 Aprili, 2007

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mhe. Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge wa Urambo, ambaye pia ndiye Spika wa Bunge letu, leo amekalia kiti chake cha Ubunge. *(Makofi*).

Tangazo lingine ningependa kueleza kwamba Ofisi ya Spika, imetoa usafiri kwa wale wanaotaka kwenda kumzika Marehemu Dr. Aaron Chiduo na ujumbe huo utaongozwa na Mheshimiwa Gideon Cheyo. Mheshimiwa William Shellukindo yumo katika msafara huo na Mheshimiwa Abdulkarim Shah pia yumo. Lakini kama kuna wengine watapata nafasi, basi litaondoka saa tatu na nusu aasubuhi hii, nafasi bado zipo na basi litarudi leo hii hii. Kama kuna Waheshimiwa Wabunge ambao hawakujua na wangependa kwenda, basi wanakaribishwa.

## MASWALI NA MAJIBU

### Na. 54

### Posho kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji wana kazi nyingi na ngumu katika maeneo ya ndani na nje ya maeneo yao:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwalipa posho za kutosha kufidia muda wanaopoteza katika kushughulikia maendeleo ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wenyeviti wa Mitaaa, Vitongoji na Vijiji wanafanyakazi ngumu katika maeneo yao. Kazi wanazofanya siyo za kuajiriwa bali ni za kujitolea. Kwa hiyo, Halmashauri zinawalipa posho kwa kazi ngumu wanazofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanafanya kazi kubwa ya kusimamia shughuli za Maendeleo katika maeneo yao. Katika tangazo la Serikali Namba 3 la tarehe 7 Januari, 1994 Halmashauri zote nchini zilielekezwa kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji si chini ya asilimia 3 ya makusanyo ya vyanzo vya mapato wanavyohamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kufuata kodi zenye kero na ambazo baadhi zilikuwa ni vyanzo vya mapato vya Halmashauri bado kuna vyanzo vya mapato ambavyo Halmashauri zetu zinawajibika kuvikusanya. Aidha, kwa kutumia vyema fedha za fidia ya vyanzo vya mapato vilivyofutwa tunao uhakika kwamba Halmashauri zina uwezo wa kulipa posho kwa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kwa viwango wanavyostahili.

Aidha, zipo Halmashauri ambazo zinatekeleza agizo hili. Kwa hiyo, kwa mara nyingine tena nazielekeza Halmashauri nyingine ambazo hazijatekeleza, zitekeleze agizo hili mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Biharamulo vyanzo vikuu vilikuwa Kodi ya Maendeleo na ushuru wa mifugo, malipo yalikuwa asilimia 3 ya makusanyo. Baada ya kufuta kodi au vyanzo hivi viwili mwaka 2004/2005 Wenyeviti wa Vijiji walianza kulipwa Shs.15,000/= kwa mwezi. Mwaka 2005/2006 motisha hiyo ya Wenyeviti na vijiji ilishuka mpaka Shs.10,000/= ili Wenyeviti wa Vitongoji nao wapate Shs.5,000/= kama motisha. Hivyo kila Halmashauri itaendelea kulipa motisha hizo kwa Viongozi wa aina hiyo kulingana na uwezo uliopo, lakini isiwe chini ya asilimia 3.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina swali ndogo la nyongeza.

(a) Kwa kuwa hao watu ni watu ambao nao wana wajibu wa kufanya, wanahitaji kula, wanahitaji kuvaa, wanahitaji kusomesha watoto pamoja na mambo mengine. Hivi kweli posho ya shilingi 5,000, kwao hata kwa siku moja wanaweza kumudu mahitaji watoto wakala, wakanywa, wakavaa na kusoma?

(b) Pamoja na kwamba wameruhusiwa kupewa posho hizo, Naibu Waziri anaweza akaniambia tangu mpango huo uanze kutekelezwa, Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji katika Wilaya ya Birahamulo wameishapata kiasi cha shilingi ngapi na wamelipwa kwa miezi mingapi mfululizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji hawana ajira ya kudumu, wao wanafanya kazi ya kujitolea na ni viongozi wa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanalipwa ile asilimia 3 kama motisha na siyo mshahara. Kwa hiyo, ile kazi ni ya kujitolea. Pamoja na hayo tunafahamu kwamba wanafanya kazi nzuri sana na wana kazi nyingi.

Lakini kwa maelezo ya Serikali tulielekeza Halmashauri zote kwamba jamani katika makusanyo yao *at least* asilimia 3 irudi kwa ajili ya kuwalipa hao Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji na tangu tutoe agizo hilo mwaka jana wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Azzan Zungu, baadhi ya Halmashauri zimeweza kutekeleza agizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Biharamulo. Biharamulo wao huwa wanawalipa motisha ya shilingi 10,000 kwa Wenyeviti wa Vijiji na shilingi 5,000 kwa Wenyeviti wa Vitongoji. Hela hizo siyo kwamba wanalipwa kila mwezi, ni baada ya muda kama Halmashauri imepata makusanyo wanachukua angalau kiasi fulani cha fedha wanawalipa kulingana na walivyojiwekea utaratibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ninachoomba Halmashauri nyingine naziagiza kwamba zitimize wajibu wake wa kuwalipa motisha hao Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti Vijiji na Wenyeviti Vitongoji kama tulivyoagiza na kwamba lile tangazo la Serikali mpaka sasa hivi halijafutwa. Kwa hiyo, wakienda kinyume cha hayo ina maana wameenda kinyume cha tangazo la Serikali.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali ilifuta kodi ya maendeleo iliyokuwa kero kwa wananchi. Lakini bado Serikali ikaanza kutoa ruzuku badala ya hiyo kodi kwenye Halmashauri; na kwa kuwa wakati wa kulipa kodi asilimia 20 ilikuwa inarudi vijijini na Wenyeviti wanapata posho.

Je, kwa nini hiyo ruzuku inayotolewa na Serikali badala ya kodi ya maendeleo, asilimia 20 isiendelee kurudi kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli baada ya kufuta vyanzo

vya mapato Serikali inafidia kiasi cha yale mapato kwa kila Halmashauri. Kila Halmashauri inatakiwa kurudisha asilimia 20 katika vijiji kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Ninachoomba au ninachoagiza kwa Halmashauri ziendelee kutoa hiyo asilimia 20 kwa vijiji ili vijiji vyenyewe vijipangie mambo ya kufanya ya maendeleo pamoja na kiasi cha asilimia 3 kwa ajili ya kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji.

Na. 55

**Ujenzi wa Barabara ya Uru – Moshi**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kampeni za uchaguzi mkuu uliopita Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara ya Uru toka Moshi Mjini; kwa kuwa barabara hiyo ndiyo tegeemo la masoko yote ya Moshi Mjini kuleta vyakula na bidhaa nyingine toka kwa wakulima; na kwa kuwa ni kweli kwamba, wananchi wa Uru walimpa Rais kura nyingi sana.

Je, ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Uru itatimizwa Lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika kampeni za uchaguzi Mkuu uliopita Mheshimiwa Rais aliahidi kusaidia matengenezo ya barabara ya Uru toka Moshi Mjini. Barabara ya Uru anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge inaunganisha Manispaa ya Moshi na vijiji vya Moshi Vijiji vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ambavyo ni Mwasi Kusini, Kishimundu, Mwasi Kaskazini, Mnini, Kyaseni, Mruwiya, Materuni na Wondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ni muhimu kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa Manispaa na Wananchi wa vijiji vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Barabara ya Uru kwa upande wa Manispaa ya Moshi ina urefu wa kilomita 2.0 na kwa upande wa Moshi vijijini ina urefu wa kilomita 13.0. Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kuitambua ahadi hii imetenga awamu tatu kufanyia matengenezo barabara hii.

Kwa mwaka 2006/2007 wametenga shilingi 80,000,000 kutoka fedha za mfuko wa barabara kutengeneza mita 400, kwa mwaka 2007/2008 zitatengwa shilingi 152,000,000 kwa ajili ya kutengeneza kilomita moja na mwaka 2008/2009 zitatengwa shilingi 130,000,000 kukamilisha mita 600 za barabara zilizobaki. Aidha, kwa upande

wa Halmashauri ya Moshi kupitia Bajeti yake ya matengenezo ya barabara kwa mwaka 2007/2008 itafanya matengenezo ya kawaida kwa kiasi cha shilingi 9,000,000 ili iwe inapitika kwa uhakika wakati tukisubiri upatikanaji wa fedha za matengenezo makubwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami yana gharimu fedha nyingi na sasa hivi Serikali haina fedha za kutosha kugharamia mahitaji yote ya matengenezo ya barabara nchini. Tunachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ahadi za Mheshimiwa Rais zitatimizwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana ndani ya kipindi cha mwaka 2005/2010. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa ruksa nami niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Barabara hii imekuwa ni kero kwa miaka mingi hasa kipande kile cha Mjini, na tangu kauli ya Mheshimiwa Rais itolewe mimi nikiwa ni mmoja katika Madiwani mwa Manispaa tumekuwa hatutengi fedha japokuwa nimesikia ametenga fedha, lakini ahadi hizo huwa ni hewa. Kwa sababu wanafikiria ahadi ya Rais itakuja kujenga hiyo barabara. Kwa hiyo, kila mara fedha zinapopatikana zinapelekwa katika barabara nyingine na zinaachwa kupelekwa katika barabara ile kwa sababu barabara ile mimi nimejenga hoteli pale na mimi ni Mpinzani na wanatumia hiyo kwa kutokuijenga barabara hiyo na nimekuwa ninapiga kelele kwa zaidi ya miaka 5 wakati nikiwa Mbunge.

Je, Naibu Waziri atalaizimisha Manispaa sasa itimize ahadi yake ili barabara ile iweze kupitika kwa sababu ni muhimu siyo tu kwa maendeleo ya uchumi, lakini hata vilevile kwa watalii ambao wanatumia barabara kwenda katika mahoteli yaliyoko katika barabara ile? Hilo swali la kwanza.

La pili, ili kweli Naibu Waziri aione tabu iliyoko pale ninamwomba aniahidi atakuja kuona ile barabara ili ashuhudie na lini ataweza kuja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, lakini u-*withdraw* yale maneno ya kwamba kwa sababu kuna hoteli yako na wewe ni Mpinzani, yale maneno uyafute kwanza.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama yale maneno yanakera ninaomba kuyaondoa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kumweleza a-*withdraw* ile *statement* kwa sababu mambo mengi tunayatekeleza hatuangilii upande wa wapinzani au wasio wapinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kero ya barabara hii inaeleweka kwamba hiyo barabara ilitengenezwa kwa kiwango cha lami kwa muda mrefu sana na lami ile imechakaa. Ndiyo maana tumeahidi kwamba tutahakikisha kwamba barabara hiyo

inatengenezwa. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema mwenyewe kwamba yeye ni Diwani. Ninajua hoja zote zinajengwa kwenye Halmashauri husika. Mimi ninamwomba tu azidi kusisitiza kwenye Halmashauri yake zile fedha ambazo zimeahidiwa kutengwa zitengwe na zianze kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, ni kwamba barabara ile iko Mjini na kila mmoja ameishapita na anaifahamu na mimi mwenyewe ni mmojawapo ambaye ninaifahamu hiyo barabara kwamba imechakaa. Kwa hiyo, nimeishaiona na tunaifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 56

**Wanaume Kuruhusiwa "*Labour Room*"**

**MHE. HAROUB S. MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Uzazi wa Mpango kwa asilimia kubwa unawasaidia kuzaa salama; na kwa kuwa wanaume wengi nchini hawakubaliani na uzazi wa mpango; na kwa kuwa hapa nchini hakuna utaratibu wa kumruhusu mume kuingia "*labour room*" ili ashuhudie mkewe anavyojifungua.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka kuanzisha utaratibu huo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Haroub Said Masoud kwamba Uzazi wa Mpango unawasaidia wazazi kujifungua salama na kupunguza vifo vya watoto wachanga. Mpango huu ni mzuri na moja ya mikakati ya Wizara ya Afya na Ustawi ni kuwaelimisha wanaume na jamii kwa jumla kuelewa athari zitokanazo na uzazi usiokuwa wa mpango ili washirikiane na wake zao kikamilifu katika kupanga uzazi na kuwasaidia wanapokuwa wajawazito ili waweze kujifungua salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa wanaume wote wajishirikishe vizuri ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambao bado wanaendelea kupata watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na utamaduni wa Mwafrika na maadili ya tiba toka hapo awali kitendo cha kuzaa kwa heshima na unyeti wake kimekuwa kikifanyika kwa siri kati ya mama anayejifungua na mhudumu anayemhudumia. Mhudumu anaweza akawa ni ndugu wa kike, Mkunga wa Jadi, Muuguzi au Daktari katika vituo vya kutolea huduma.

Kwa kawaida huduma ya kumsaidia mama anapojifungua imekuwa ikifanywa na akinamama isipokuwa pale mama anapojifungulia hospitali ambapo anaweza kupewa huduma na mtoa huduma mwanamke au mwanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwauliza wanawake ambao wamewahi kupata uchungu na hatimaye kujifungua watasimulia adha ya maumivu wanayopata wakati wa tendo la kujifungua. Wengine wakiapa kwamba kamwe hawatarudia kubeba mimba. Kila jamii ina desturi zake na desturi nyingi hapa nchini tumezibadilisha au kuzikemea kutokana na madhara tunayoyagundua kwa mfano, kurithi wajane.

Kwetu sisi Watanzania kitendo cha kujifungua tumekipa usiri, unyeti na heshima ya pekee. Tunapotaka kubadilisha mwenendo huo au mienendo mingine hatuna budi kujiuliza tunalenga nini, kupunguza maumivu ya mama anayejifungua, kuboresha uhai wa mtoto au kutaka kuona jinsi mama anayejifungua anavyopata tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vyetu vingi vya kutolea huduma za afya hapa nchini vina chumba kimoja tu cha kujifungulia ambamo mara nyingi wanawake zaidi moja wanajifungua kwa wakati mmoja. Katika mazingira hayo si rahisi kuruhusu mume au *boy friend* kuingia ndani kuangalia mke anapojifungua. Iwapo utaratibu huu utaanzishwa itabidi kubadilisha mfumo mzima wa wodi ili vyumba vya kujifungulia viongozwe kukidhi usiri kati ya mzazi mmoja na mzazi mwingine.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimelemewa. Kwa sababu nilitarajia Mheshimiwa Naibu Waziri atalijibu swali hili. Lakini hata hivyo, swali moja ninalikataa, nitauliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amenijibu vyema kabisa na amekubaliana na mimi kwamba iko haja mawazo yangu yaweze kufanyiwa kazi, na vilevile katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hata mwenyewe mzazi anapojifungua anaapa kwamba hatataka kuzaa tena.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri haioni kwamba ikifanyiwa haraka na sisi tukaona jinsi tabu kubwa wanayowapata wake zetu, tutawazalisha taratibu? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu swali la msingi nimesema kwamba hao akinamama wanapata shida sana na nikasema tunapobadilisha desturi tujiulize kwamba kuwepo wetu katika chumba cha kujifungulia tunalenga nini na nikauliza kama je, tunafikiri kuwepo katika hicho chumba tutapunguza maumivu. Sasa hapo nitakapohakikishiwa kwamba hiyo ni njia mojawapo ya kupunguza maumivu nitakuwa tayari kuharakisha hili zoezi. Ahsante.

Na. 57

**Hali ya Kituo cha Mandondo**

**MHE. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inathamini huduma za tiba zinazotolewa na Waganga wa Jadi, na kwa kuwa, baadhi ya Waganga hao wana vituo vinavyolaza wagonjwa wengi kuliko hata hospitali zetu za Wilaya:-

(a) Je, Serikalil haioni kuwa, ni vyema kukisaidia Kituo cha Mandondo, katika kijiji cha Kijango Kata ya Magoma, huduma muhimu kama maji safi, vitanda, huduma za umeme japo wa '*solar*' na baadhi ya majengo kama vyoo kwa kuwa kituo hicho ni maarufu ndani na nje ya nchi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, ni vyema wahudumu kwenye kituo kama hivyo wapatiwe mafunzo ya awali ya huduma za afya hususan upande wa kinga?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Laus Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kuhusu Tiba Asili hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Sheria iliyotungwa mwaka 2002, sheria Na.23 ni Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Sheria hiyo inaelekeza kwamba kutakuwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Baadhi ya majukumu ya Baraza hili ni pamoja na kutoa elimu kwa watoa huduma za tiba Asili kuhusu namna ya kuyaeleza magonjwa kwa wagonjwa, uwekaji wa kumbukumbu na taarifa za wagonjwa, usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kutumia vyoo na taratibu za kurufani wagonjwa mara watambuapo kuwa hawana uwezo wa kuwatibu. Baraza linafanya kazi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kupitia Waganga Wakuu wa Wilaya ambao ndio waratibu wa huduma za Tiba Asili Wilayani. Lengo kuu ni kuweza kurasimisha huduma hizi ili ziweze kutambulika na kutumiwa na watu wengi zaidi pale inapolazimu.

Baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Laus Mhina, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Waganga wetu wa Tiba Asili wamekuwa na wanaendelea kutoa huduma za tiba hapa nchini na Serikali inatambua mchango wao. Baadhi yao wanawatunza wagonjwa sehemu wanakoishi na wachache wanazo sehemu maalum za kuwalaza wagonjwa wao; Kituo cha Mandondo ni mojawapo cha vituo hivyo. Kwa kuwa utaratibu wa urasimishaji unasimamiwa na Baraza na kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amekitambua kituo cha Mandondo kuwa ni kituo kinachotoa huduma nzuri, napenda nimshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya kuona namna ya kukiweka katika mipango wake wa Wilaya ili kuweza kutoa msaada kama alivyozungumzia maji safi, vitanda, huduma za umeme japo wa '*solar*' na baadhi ya majengo kama vyoo.

(b) Utoaji wa mafunzo kwa wahudumu wa Tiba Asili ni jukumu la Baraza na Wilaya husika kupitia Mganga Mkuu wa Wilaya kwa kuwatumia Waratibu wengine wa Tiba Asili katika ngazi ya Wilaya. Ni matarajio yangu kuwa Mheshimiwa Mbunge atashirikiana na Halmashauri ya Wilaya yake na Mganga Mkuu wa Wilaya *(DMO)* kuweka katika mpango wa Wilaya mafunzo ya watoa huduma wa Tiba Asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu, kuwasisitiza Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwamba Tiba Asili inatambulika na Serikali. Hivyo, katika ngazi ya Mikoa na Wilaya ni wajibu wa Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini kuratibu na kusimamia huduma za Tiba Asili kwa mujibu wa Sheria Na. 23 ya mwaka 2002, ikiwa pamoja na kuratibu mafunzo ya Tiba Asili kwa Waganga wa Tiba Asili.

Na. 58

**Tatizo la Maji Nchini**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna huduma ya majitaka hapa nchini na kuna wananchi ambao hawana huduma hiyo na kwa kuwa, wananchi hao wanalipia huduma hiyo kila mwezi.

Je, Serikali inasema nini kuhusu dhuluma hiyo wanayofanyiwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Maji ina jukumu la kusimamia huduma za majisafi na uondoaji majitaka katika Miji Mikuu ya Mikoa 19 pamoja na Jiji la Dar es Salaam. Huduma hizo hutolewa na Mamlaka za Majisafi na Majitaka za miji chini ya uangalizi wa Bodi husika ambazo ndizo zenye mamlaka ya kupanga bei za huduma kwa ridhaa ya chombo cha udhibiti cha *EWURA*.

Hadi sasa ni Mamlaka 10 tu ambazo Arusha, Moshi, Mwanza, Morogoro, Tanga, Mbeya, Iringa, Dodoma, Tabora na Dar es Salaam ambazo zinatoa huduma ya uondoaji wa majitaka mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida Mamlaka zote zenye huduma hii huwatoza wateja wake gharama za uondoaji majitaka ambazo zina uwiano na gharama za huduma ya majisafi ambazo hutolewa kwa wateja hao. Gharama hizo ni huduma ya uondoaji majitaka ni kati ya asilimia 30 na 50 ya gharama za huduma ya majisafi kwa wale tu waliounganishwa kwenye mfumo wa majitaka.

Wateja ambao hawajaunganishwa hupatiwa huduma ya kunyonya mashimo yao ya majitaka (*Septic Tanks*) yanapojaa. Wateja hao hulipia huduma hiyo moja kwa moja kupitia Halmashauri za Miji au watu binafsi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kuwalazimisha wananchi ambao hawajajiunganisha kwenye mifumo ya majitaka kulipia huduma hiyo kupitia Ankara zao za huduma ya majisafi ni kinyume cha taratibu zilizowekwa. Iwapo kuna mteja yeyote ambaye amelazimishwa kulipia huduma hiyo pasipo kuipata, naomba nipatiwe taarifa ili niweze kufuatilia na kurekebisha makosa hayo.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa ni kinyume cha utaratibu kuwatoza *fee* wale ambao hawajaunganishiwa maji taka; lakini pia ameomba kupata taarifa; napenda kumthibitishia taarifa ninayo na ninafahamu kuwa kitendo hicho kinafanyika. Je, anawaeleza nini wananchi wale ambao tayari wanalipia maji taka na ni kinyume cha Sheria. Pesa zao watarudishiwa na kama watarudishiwa, watarudishiwa kwa kuweza kupewa na wao kama Idara ya Maji wanavyofanya mtu akichelewa kulipa maji analipa na faini; na wao watalipa kwa faini?

Swali la pili kwa kuwa ni kinyume cha sheria kuwatoza watu huduma ambayo hawaipati. Je, Waziri anaeleza nini kwa wale ambao tayari wamewatoza watu huduma ambayo hawaipati watapata adhabu gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa ajili ya kuwafahamisha wananchi wote ya kwamba kwa yeyote yule ambaye anatozwa huduma ya maji taka na yeye hapatiwi huduma hiyo, napenda kuwafahamisha kwamba waende moja kwa moja kwenye Ofisi zetu za Mamlaka ya Maji husika ili waende wakarekebishiwe kosa hilo na pia gharama ambazo walizolipa zitabadilishwa na zitaingizwa kwenye ankara yao ya maji safi ili zitakatwa humo moja kwa moja. Pia napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la faini watakapokwenda huko kwenye Mamlaka husika na wenyewe wana taratibu zao za kazi litazungumziwa huko.

**NAIBU SPIKA:** Yenyewe haitakuwa faini itakuwa na riba. Sikuona mtu mwingine tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Keenja.

Na. 59

**Tatizo la Maji – Dar es Salaam**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji jambo linalosababisha ugonjwa wa kipindupindu usiondoke Jijini humo; na kwa kuwa,

kumekuwepo taarifa mbalimbali juu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali kuondoa tatizo la maji; na kwa kuwa, Makao Makuu ya Wizara ya Maji yapo Jimbo la Ubungo.

(a) Je, kuna ukweli gani kuhusiana na taarifa kwamba, kuna maji mengi chini ya ardhi kati ya Kawe na Bagamoyo na Kusini mwa Bandari ya Dar es Salaam na kwamba, litajengwa Bwawa kwenye mto Ruvu?

(b) Kama taarifa hizo ni za kweli, vyanzo hivyo vitaanza kutumiwa lini ili kuondoa tatizo la maji Dar es Salaam?

(c) Kwa kuwa, Jimbo la Ubungo yaliyoko Makao Makuu ya Wizara ya Maji kuna tatizo kubwa la maji. Je, Serikali ina mipango gani ya kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo la maji kutokana na Jiji kuwa na vyanzo vichache vya maji visivyokidhi mahitaji na mtandao wa usambazaji maji ulio chakavu. Ni kweli kwamba maeneo kadha kuzunguka Jiji yana maji chini ya ardhi yanayoweza kuongezea maji kutoka vyanzo vya sasa vya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Mtoni na Visima. Maeneo hayo ni kama Nzasa, Kimbiji, Mpiji na Mpera ambako utafiti bado unaendelea. Mpaka sasa visima vitatu vya uchunguzi na vitatu vya matumizi vimekwisha chimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inao mpango wa kujenga bwawa kwenye Mto Ruvu eneo la Kidunda ili kuongeza upatikanaji wa maji kwenye mitambo ya maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya Mpiji, Kimbiji na Mpera na tathimini yake unafanyika na unakadiriwa kuchukua miaka miwili kukamilika. Aidha, muda wa ujenzi kukamilika kwa Bwawa la Kidunda utajulikana baada ya usanifu wa Bwawa na uandaaji wa michoro yake utakapokamilika.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ubungo hupata huduma ya maji kutoka kwenye mtambo wa maji wa Ruvu Juu. Mtambo huu hutoa lita 82 milioni kwa siku ukilinganishwa na mahitaji ya maeneo yanayohudumiwa na mtambo huo ya lita 116 milioni kwa siku. Kutokana na uwezo mdogo wa mtambo na uchakavu wa Mitandao kwenye maeneo yanayopata maji kutoka kwenye mfumo huu, maji hayo kwa sasa hutolewa kwa mgao. Aidha, Serikali hivi sasa inaufanyia ukarabati mtambo wa Ruvu Juu, mabomba yanayosafirisha maji safi pamoja na matanki ya maji Kimara.

Mradi huu utakaoanza mwaka 2008, mabomba ya usambazaji maji yatalazwa kwenye maeneo 16 vikiwemo vijiji vifuatavyo vya Jimbo la Ubungo ambavyo ni:

Kiluvya, Kibamba Shuleni, Mbezi Msigani, Mbezi Mukabe, Kwembe, Mbezi Temboni A, Kibanda cha Mkaa, Kimara Baruti, Msewe, Changanyikeni, Ubungo Kibangu na Ubungo Kisiwani.

**MHE. CHARLES N. KEENJA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri kama ilivyokawaida yake. Lakini nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kutokana na hizi hatua nzuri zinazochukuliwa na Serikali ambazo zinaendelea na nyingine ziko katika mipango, Serikali sasa inaweza kutuambia ni lini wananchi wa Dar es Salaam wanaweza kutegemea kupata maji ya uhakika au tutaendelea kwa miaka mingapi kuanzia sasa katika hali hii ngumu sana ya upatikanaji wa maji na hasa zinazotokana na hali hiyo? Swali langu la pili ni kwamba katika mwaka jana na mapema mwaka huu kuna vipindi ambavyo maji yalipatikana kwa mgao lakini kwa uhakika zaidi. Saa hivi hali imerudi kuwa mbaya sana huko Kimara Baruti, Makoka, Manzese na Kadhalika. Je, nini kimetokea na kuturudisha kule tulipokuwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba upatikanaji wa uhakika wa maji wa Jiji la Dar es Salaam unategemea na tafiti hizo tunazofanya ikiwemo Bwawa hilo la Kidunda na pia visima hivi vya majaribio. Lakini kwa upande wa Bwawa la Kidunda si rahisi kwa sababu ndiyo tuko katika awali ya kuangalia mambo mbalimbali yakiwemo eneo zima na kutoa fidia kwa wananchi kwa sababu kutakuwa na vijiji zaidi ya sita vitavyomezwa na Bwawa hili na hali kadhalika kuanza polepole mambo ya michoro na usanifu, si rahisi kusema sasa hivi kwamba kuanzia lini Jiji la Dar es Salaam litaondokana na adha hiyo ya maji lakini pole pole tunavyozidi kwenda ndivyo ambavyo tutaanza maji yataanza kurekebishika.

Kwa mfano visima hivi vya majaribio, Kisima cha Kimbiji kimeonyesha mategemeo mazuri sana na Kisima cha Mpiji na Wizara yangu imefika kushuhudia maji hayo ni matamu, mazuri na ni mengi mno. Lakini bado tafiti zinaendelea tupate uhakika. Lakini hayo yakikamilika ni maji ambayo yanaweza yakaongezewa ili ile shida ya maji Dar es Salaam ikaanza kupungua polepole. Narudia tena Kidunda ni mpaka ambapo tutakapokamilisha usanifu na kila kitu ndipo hapo sasa tutajua thamani na tutajua wakandarasi watakuwa nani na ndipo tutajua hali halisi lini inaanza.

Kuhusu swali la pili ni kwamba napenda kwanza kuwapongeza *DAWASCO* na *DAWASA* kwa kazi wanayoifanya. Kwa kweli hali ya maji ya Jiji la Dar es Salaam ni ngumu kwa kufuatana kwamba mitambo ni michakavu na sasa hivi inakarabatiwa.

Lakini hata hivyo anajitahidi chochote kilichopo kinagawiwa na mfano maeneo ya Kimara Wizara yangu tumekuwa tukiyatembelea kwa muda wa wiki kadhaa zilizopita tumekagua hali si mbaya sana kama jinsi Mheshimiwa Mbunge anavyosema na kuna sehemu kama za Kimara kule *TANESCO* sasa hivi tunawajengea *Viosk* kwa ajili ya kuwasaidia na kuna sehemu nyingine ambazo tutaweka mtandao. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba tunaomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie lakini tunajitahidi kwa kila hali kuhakikisha maji haya yaweze kuwasaidia wananchi wa Jiji la Dar es Salaam.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo linalowakabili wakazi wa Jimbo la Ubungo linafanana na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ambako ndiko kwenye vyanzo vikuu vya maji, Mto Ruvu, Mto Rufiji na Mto Ruaha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwasaidia wananchi hawa ambao wanatunza mazingira vizuri maji hayo yanakuwa ni mengi na wanaofaidika ni wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wao hawapati kitu ukizingatia majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wamefanya tafiti wamegundua kwamba kwenye ardhi ya Mkoa wa Dar es Salaam kuna maeneo mengi ya maji na pia amewapongeza *DAWASCO* na *DAWASA*, kuna mkakati gani ambao hao wanaofaidika wanapata pesa wakati wanaotunza mazingira na maji mengi kupatikana hawapati kitu. Je, kuna chochote watakachogawiwa wananchi wa Mkoa wa Pwani ili waondokane na adha ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba kwa sasa hivi ukarabati wote unaofanywa na pia programu hiyo ya maji haihusu Mkoa wa Dar es Salaam peke yake pia na Mkoa wa Pwani sehemu za Kibaha watanufaika na hiyo. Lakini hali kadhalika Wizara yangu ina njia nyingine mbalimbali za kutoa huduma ya maji kwa Mkoa wa Pwani ikiwemo miradi ya kupitia katika programu hii ya maji vijijini ambapo ninauhakika kuna vijiji ambavyo vitanufaika na hali kadhalika miradi ya zamani tumepokea kwa ajili ya kuirekebisha. Kwa hali hiyo yanayofanyika Mkoa wa Dar es Salaam hali kadhalika manufaa yake pia yanakwenda katika Mkoa wa Pwani; na katika katika miradi ya majaribio kisima cha Mpela hicho ni cha Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo namhakikishia kwamba manufaa kwao pia yapo. Ahsante.

Na. 60

**Ukosefu wa Maji Mufindi**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Mufindi ni moja ya Wilaya inayochangia pato la Serikali kwa kiasi kikubwa; na kwa kuwa, mapato hayo hutokana na mashamba makubwa ya chai na miti ya mbao yanayozunguka Vijiji vya Sawala, Kitiro, Kufio Mpanga na Kibao:-

(a) Je, Serikali inatambua kuwa, pamoja na uzalishaji mkubwa unaofanywa na wananchi wa vijiji hivyo, wananchi hao hawana maji ya bomba yaliyo safi na salama?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha mradi wa maji ulioharibiwa na ujenzi wa barabara iendayo *SPM*-Mgololo mwanzoni mwa miaka ya 1980?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, naomba kwanza kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Vijiji vya Sawala, Mbaya, Kitiru, Lufuna, Mtwango na Kibao vipo katika kata ya Mtwango na Tarafa ya Ifwagi, Jimbo la Mufindi Kusini.Vijiji vinne vya Sawala, Lufuna, Mtwango na Mpanga vilipatiwa maji ya bomba kwenye miaka ya 1972. Chanzo cha maji kilikuwa ni kijito cha Nyamalala na maji yalikuwa yanasukumwa kwa mitambo ya kutumia dizeli kwenda kwa watumiaji. Kutokana na ongezeko la watu, vijiji hivyo vinne vilipanuka na kuwa jumla ya vijiji saba vya Sawala, Mbaya, Kitiru, Kufio, Lufuna, Mtwango na Kibao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu maswali (a) na (b) ya Mheshimiwa Mbunge Malangalila, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa pamoja na uzalishaji mkubwa unaofanywa na wananchi wa vijiji hivyo kwamba hawana maji ya bomba yaliyo safi na salama. Wakati wa kipindi cha ujenzi wa barabara iendayo kwenye kiwanda cha Mufindi *Southern Paper Mills* itokayo Mtwango hadi Mgololo mabomba ya maji ya vijiji vya Sawala, Mbaya, Kufio, Kitiru na Mtwango yaliharibiwa. Mnamo mwaka 1999 Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilifanya tathimini ya mradi huo ambao makadirio yake yalifikia shilingi 356,409,000. Hata hivyo fedha kwa kipindi hicho hazikuweza kupatikana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vijiji vilivyoathirika na ujenzi huo vikiwemo Sawala, Mtwango na Kibao vimeingizwa kwenye mradi itakayohudumiwa katika mwaka huu wa fedha 2006/2007. Wizara yangu inapenda kushauri Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi iingize vijiji vilivyobakia katika Kata hii kwenye awamu itakayofuata. Kwa hali hiyo nina hakika kabisa Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya vijiji tayari vitahudumiwa na maji safi yatarudishwa.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Mjini kwa sasa pamoja na kwamba Ziwa Tanganyika liko nusu kilomita hakuna maji. Naibu Waziri anaweza kuniambia sasa tatizo hili la watu wa Kigoma Mjini litatuliwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Mjini ipo karibu na Ziwa Tanganyika. Nakumbuka nilijibu swali hili kipindi kilichopita kuelezea mikakati ya Wizara yangu kuhusu huduma tutakayotoa katika Halmashauri ikiwemo miradi ya maji safi na maji taka. Programu hii inaendelea miradi ipo kwa wafadhili na kwa sasa hivi bado mradi huu haujaanza namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tuweze kuendelea na mradi huo. Lakini hata hivyo pia namwomba aje Ofisi niweze kumpa taarifa kamili za mradi wake huo kwamba huduma imefikia kiasi gani?

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Ng'ong'ona, Tarafa ya Kikombo wamekuwa na tatizo kubwa sana la maji na ambalo linafanana na wananchi wenzao wa Mufindi; na taarifa tulizonazo ni kwamba kuna mradi wa maji wa chini ya Mkopo wa Benki ya Dunia ambao unashughulikia hivi sasa. Je, ni lini mradi huu utakamilika kwani wananchi hawa wanaendelea kuteseka kutokana na tatizo la maji?

**NAIBU SPIKA:** Kwa sababu Naibu Waziri anayajua hayo kwa kichwa namruhusu ajibu vinginevyo ningesema ni swali jipya. Mheshimiwa Waziri mwenyewe maana yake kompyuta zinatembea.

**WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya vijiji katika Wilaya zote Tanzania sasa hivi itaratibiwa moja kwa moja na Halmashauri za Wilaya mbalimbali. Kuna mradi ambao unafadhiliwa na *World Bank* ulitanguliwa na Wilaya 14 na mwaka huu unaenda katika Wilaya zote Tanzania nzima Halmashauri zitasimamia katika kuhamasisha wananchi kusanifu miradi hii lakini pia fedha zitapelekwa moja kwa moja katika Halmashauri hizo. Tulitegemea kupata fedha hizi mapema kabla ya wakati ule kukutana hapa.

Lakini kufuatana na taratibu za utoaji wa fedha hizo zimechelewa na tunatarajia kabla ya mwanzo wa mwaka wa fedha ujao tutapata fedha ambazo zimeahidiwa na wafadhili wakiwemo *World Bank* na *African Development Bank.* Sasa hivi taratibu zinafanywa na Hazina na mara tu pesa hizo zitakapotolewa zitapelekwa moja kwa moja katika Halmashauri husika. Kwa maana hiyo Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wahakikishe kwamba katika majimbo yao miradi ile ambayo tayari imeorodheshwa wawe wamewaandaa Wahandisi Washauri vilivyo ili fedha zitakapotolewa tu kazi ianze kwa ukamilifu na uaminifu tofauti na baadhi ya maeneo ambayo wamezitumia vibaya fedha hizi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea, swali namba 61 limefutwa na anayehusika kwa hiyo Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itajibu swali linalofuata. Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji

Na. 62

**Ajira katika Balozi zetu nje ya Nchi**

**MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ina Balozi zake nchi za nje ambazo zinahitaji watumishi; na kwa kuwa, kuna vijana wengi wanaohitaji ajira katika nyanja mbalimbali:-

(a) Je, utaratibu gani unatumika katika kuwaajiri wafanyakazi wa kawaida *(local staff)* katika Ofisi zetu za Ubalozi zilizoko nje ya nchi?

(b) Je, mwajiriwa anatakiwa kuwa na sifa zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Tanzania ina Balozi zake nchi za nje ambazo zinahitaji watumishi wenye ujuzi mbalimbali kutokana na mahitaji ya Ubalozi husika na ni kweli kuwa tuna Watanzania wengi wanaoishi katika nchi ambazo Balozi zetu zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika katika kuajiri wafanyakazi wenyeji *(Local Staff)* katika Balozi zetu za nje ya nchi ni kama ifuatavyo:-

(i) Balozi husika hutangaza nafasi zilizowazi kwenye tovuti, magazeti, ubao wa *visa* wa matangazo uliopo Balozini pia na vyombo husika vya uajiri katika nchi hizo ili kupata waombaji wa kazi inayotangazwa. Maombi huchambuliwa kulingana na sifa kwa kazi zilizotangazwa.

(ii) Hufanyika uchambuzi yaani *short listing* ili kubaini waombaji wa kusailiwa.

(iii) Mwombaji anayefaulu usaili huajiriwa kwa masharti ya *Local staff* au Watumishi wenyeji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, sifa anazotakiwa kuwa nazo mwajiriwa katika Balozi zetu nje ya nchi, ni kama zifuatazo:-

(i) Lazima awe mkazi halali wa nchi husika.

(ii) Lazima awe na kibali cha kufanya kazi katika nchi husika.

(iii) Mwombaji lazima awe na sifa ya kazi inayotangazwa, mara nyingi kazi zinazotangazwa katika Balozi zetu ni Ukatibu Mahususi, Udereva, Ukalimani, Utarishi na kazi nyingine kama hizo.

Mheshimiwa Katika mchakato huu vipaumbele hupewa Watanzania kama ilivyofanyika katika Balozi zetu za New York, Washington, Nairobi, Kampala, Kigali, Pretoria, London na Geneva kwa kuzitaja Balozi chache.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na sifa za mwajiriwa ambazo zimesemwa na kuainishwa; kwa kuwa waajiriwa wanaokwenda nje huongozana na baadhi yao na wake zao au waume zao.

Je, Wizara imewahi kutayarisha mafunzo ya aina kwa mfano *personal grooming* ambayo yanawawezesha kuishi katika maisha ya kihadhi ya kidiplomasia wakiwa katika nchi za nje?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maofisa wetu wengi wanaokwenda kufanya kazi katika Balozi zetu nje ya nchi huwa wanapewa mafunzo maalum au *crush program* katika Chuo chetu cha Diplomasia Kurasini kwa nia ya kuwawezesha kujua wadhifa na namna ya kwenda kuishi kule nje kama wake au waume wa Mabalozi na hata Mabalozi wenyewe.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH**: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa hivi kutokana na hali halisi ya utandawazi duniani na kuna umuhimu katika Balozi zetu kuwe na wataalam wa uchumi ambao wataweza kuisaidia nchi yetu kuleta wawekezaji. Je, Serikali haioni sasa kwamba kuna umuhimu wa kupeleka wachumi ambao wanasifa za kutosha kutekeleza yale yote yanayohitajika katika maswala ya uchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kweli tunaendeleza siasa au Diplomasia ya Uchumi katika Balozi zetu na mkazo hivi sasa unatiliwa katika kupeleka Maofisa ambao tunahisi wataweza kuzifanya kazi zile ambazo zinatakiwa kufanya. Kama hizo kujaribu kuhamasisha wenyeji wa nchi zile kuja kuwekeza Tanzania au kupata wafanyabiashara.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa kwamba ipo haja ya kufanya hivyo na kwa kweli hatua zipo mbioni za kupeleka wataalam wa uchumi wenye uzoefu na ujuzi wa mambo ya biashara katika Balozi zetu.

**YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa chombo hiki ni cha Muungano.

Je, wakati wa ajira mnaainisha kati ya Tanzania Bara na Visiwani wakati wote wanasifa zinazohusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni chombo cha Muungano. Kila wakati tunapofanya ajira, tunafuata taratibu za uajiri ambapo nafasi hutangazwa katika magazeti na kila mwenye

sifa lazima aombe kupitia katika matangazo hayo. Wote wenye sifa zinazotakiwa wanaitwa kusailiwa bila kujali kutoka Bara au kutoka Visiwani, na anayefaulu anaajiriwa. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu kwa sababu kama ilivyokwisha elezwa hapa ni kwamba sasa ni wakati wa utandawazi na waajiriwa lazima wawe na *qualifications* zinazohitajika.

Na. 63

**Ruzuku kwa Dawa za Mifugo**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitoa ruzuku katika mbolea na kuigawa katika Mikoa yote kwa lengo la kuboresha kilimo; na kwa kuwa, kwa upande wa ufugaji ni vema kama Serikali ingetoa ruzuku ya dawa muhimu za mifugo kwa lengo la kuboresha mifugo nchini.

Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutoa ruzuku kwa dawa za mifugo ili wafugaji wapate unafuu katika ununuzi wa dawa hizo na hivyo kuboresha ufugaji wao.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kama ifuatavyo:-

Kutokana na umuhimu wa mifugo katika uchumi wa Taifa na pia kutokana na gharama kubwa za dawa za kuogesha mifugo, Serikali imeona kuwa kuna umuhimu wa kutoa ruzuku kwa dawa za mifugo ili wafugaji wapate unafuu katika ununuzi wa dawa hizo na hivyo kuboresha ufugaji wao na kuleta tija.

Kwa kuanzia Serikali imeanza kutoa ruzuku kwa dawa za kuogesha mifugo ili kupambana na baadhi ya magonjwa muhimu ambayo ni yale yanayosambazwa na kupe hususan Ndigana Kali *(East Coast Fever),* Ndigana Baridi *(Anaplasmosis)*, Mkojo Mwekundu *(Babesios)* na Maji Moyo *(Heartwater)*. Magonjwa haya husababisha vifo zaidi ya asilimia 70 ya vifo vyote vya ng'ombe vinavyotokea kila mwaka na kusababisha hasara kubwa kwa wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Njia kuu inayotumika kwa wafugaji wengi kudhibiti wengi kudhibiti magonjwa haya ni ile ya kuogesha au kunyunyiza mifugo dawa inayoua kupe. Madawa ya kuua kupe ni ghali na yamepelekea mfugaji kushindwa kuyanunua na hivyo kuongezeka kwa vifo vya ng'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokana na hali hiyo mwaka huu wa fedha 2006/2007 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo.

Serikali imewekeana mikataba na makampuni manane (8) ambayo yananunua na kuzisambaza dawa za mifugo katika mikoa 18 ya Tanzania Bara ukiwemo mkoa wa Singida. Mikoa mingine ni Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Mwanza, Mara, Kagera, Rukwa, Mbeya, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Pwani na Lindi. Wafugaji wananunua dawa hiyo kwa asilimia 60 ya bei ya soko na asilimia 40 inalipwa na Serikali kama ruzuku.

Kwa kuwa fedha hiyo haitoshelezi mikoa yote ya Tanzania Bara, mikoa iliyobaki ambayo ni Dar es Salaam, Mtwara na Ruvuma itaingizwa katika mpango wa ruzuku kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo mazuri na azma ya Serikali kwa kuliona hilo. Pamoja na hao naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Singida na Wilaya ya Singida ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimeathirika sana na ugonjwa huu wa *Lift Valley Fever* na kwa kuwa hadi sasa Wilaya ya Singida imepokea dozi 28 tu ambazo hazitoshi kabisa kabisa kabisa. Je, ni lini Serikali itaongeza dozi ya chanjo ya *Lift Valley Fever?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo zimetenganishwa huku juu, lakini huko chini katika ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya, Afisa Kilimo ndiye huyo huyo Afisa Mifugo, ili kuwajibika na ili kupata ufanisi wa kilimo na mifugo, ni lini Serikali itatenganisha kofia hizi mbili pawe na Afisa Mifugo wa Mkoa na Wilaya na vile vile pawe na Afisa Kilimo wa Mkoa ana Wilaya. Ni lini Serikali itatekeza hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mkoa wa Singida ni moja ya Mikoa iliyoathirika na homa ya Bonde la Ufa. Ni azma ya Serikali kutafuta chanjo zaidi na pindi zitakapopatikana, Mkoa wa Singida utaongezewa pale itakapoonekana ni lazima kufanya hivyo. Tayari Serikali imeishaomba jumla ya dola milioni 12 kwa ajili ya kupambana na Homa ya Bonde la Ufa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kuhusu nafasi za Mtaalam au Afisa wa Mifugo na Kilimo kuwa ndiye huyo huyo katika Halmashauri halia ambayo inasababisha ufanisi kuwa mdogo. Serikali inalitambua hilo na katika mpango wa maboresho inaliangalia na kuona itakuwaje ili kusudi kilimo na mifugo ziweze kupewa nafasi inayostahili kwa kuwezesha wataalam wetu kutekeleza majukumu yao ipasavyo bila kuchanganya taaluma na majukumu.

**MHE.MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni kweli Serikali imetoa ruzuku na imeyapa makampuni yatakayosambaza dawa katika maeneo yote ya Mikoa 18 aliyotaja Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini, makampuni hayo hayafikishi dawa kwa wafugaji. Maduka yao yako Mikoani.

Je, Serikali haiwezi kutoa ushauri kwa makampuni hayo wafikishe dawa Wilayani, kila Wilaya wawe na duka la dawa wafugaji waweze kununua dawa karibu na wajue kwamba Serikali imetoa ruzuku kwa sababu mpaka sasa wafugaji hawajui kwamba kuna ruzuku iliyotolewa na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe wito kwetu sisi Wabunge wote, yale ambayo Serikali inayasema hapa, basi sisi ni wa kuwafikishia wananchi wetu kwa sababu wametutuma ili kusudi tuweze kuwawakilisha na kwa hiyo tuna wajibu wa kuwafikishia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Laizer, nafahamu kazi nzuri anayofanya kwenye Jimbo lake kwenye eneo la ufugaji na hili awaeleze vizuri tu, ana utaratibu mzuri wa kuwaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makampuni kutofikisha dawa, napenda kusema kwamba Wizara yangu itafuatilia ili kuhakikisha kuwa kama Serikali iliovyofanya kwenye mbolea kwamba ni lazima iwafikie wananchi, na sisi kwa upande wa mifugo tutahakikisha kuwa dawa hizi za kuogeshea mifugo zinawafikia wafugaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hata mbolea bado kuna matatizo!

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa ugonjwa huu wa *Rift Valley Fever* umetushika kwa ghafla sana mpaka tukafika mahali kama tunakimbia kimbia tu hatujui cha kufanya cha uhakikika kwa sababu ugonjwa huu ulikuwa haujapata kuitokea nchi yetu. Je, Serikali sasa haioni umuhimu, kwanza wa kuhakikisha kwamba katika sehemu za wafugaji majosho yanajengwa ya kutosha ili kuzuia ugonjwa huu usirudie tena?

Pili, haya makampuni ambayo wanayaleta yawe yanagawa dawa, makapuni haya yaorodheshwe kwenye vyombo vya habari na Halmashauri zetu zijue ili tukipata matatizo tunajua kwamba ni nani ameleta matatizo hayo? Mwisho, elimu ya suala hili la ugonjwa *wa Rift Valley* iwe ni elimu ya kudumu. Je, Waziri haoni umuhimu wa mambo hayo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, siyo kweli kwamba ugonjwa huu ni mara ya kwanza kuingia hapa nchini, mwaka 1997/1998 ulikuwepo. Pili, kama tulivyokuwa tukieleza kila siku, ugonjwa huu unakuja baada ya mvua nyingi na kwa hiyo sasa hivi tumejenga uzoefu na nina hakika miaka ijayo angalau *circle* yake ni kama baada ya miaka 8/10, tutakuwa tayari zaidi na

njia moja wapo ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba uogeshaji wa mifugo sasa hivi itabidi mahala ambapo kuna teteleka tufanye iwe ni lazima, sheria inaturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kuhusu makampuni, kwanza, safari hii wafugaji wenyewe ndio tutakaowapa kuponi za ruzuku. Kwa hiyo, kwa kutumia ngazi za uongozi anapotaka kwenda kununua dawa anapewa kuponi ya hiyo *percent* ambayo itakuwa ni ya ruzuku. Kwa hiyo, akienda kwenye ile *outlet* au kwenye duka lenyewe, analipia kiwango ambacho anatakiwa kukilipa yeye kama mfugaji na kuponi upande wa sehemu ya ruzuku. Lakini, pili, dawa zote na ufungaji wa dawa hizo juu yake kutakuwa na jina kamili la ile kampuni iliyopewa eneo hilo. Kwa hiyo, itakuwa ni rahisi sana kufuatilia pale ambapo kampubni imevunja masharti. Mkataba wetu na makampuni hayo umezingatia mambo yote ambayo yanaweza kuwa upenyo wa kutokutosheleza yale tuliyokubaliana nao.

Na. 64

**Kufanya Ufugaji Uwe wa Kisasa**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipozindua Bunge tarehe 30/12/2005 katika hotuba yake alisema yafuatayo kuhusu ufugaji nchini:- “Tutoke kwenye ufugaji wa kuhamahama na kuwa wafugaji wa kisasa”, na pia kuwa “yatengwe maeneo maalum kwa ajili ya mifugo”.

Je, utekelezaji wa maagizo hayo muhimu yenye kuleta mapinduzi ya ufugaji nchini umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi wa Desemba mwaka 2006, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Mifugo inayoweka taratibu za kuielekeza Sekta ya Mifugo kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambapo katika mwaka wa 2006/2007 baadhi ya mambo yaliyotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Jumla ya Hekta 1,893,000 zimeainishwa kuwa zinafaa kwa ufugaji katika Wilaya za Chunya, Kisarawe, Lindi Vijijini, Nachingwea, Rufiji na Mkuranga. Vijiji 33 katika Wilaya hizo vimewekewa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya malisho.

(ii) Zoezi la upimaji wa ardhi kwa ajili ya malisho ya mifugo linaendelea vizuri nchi nzima chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa mfano, kwa maeneo ambayo mifugo imehamishiwa hivi karibuni katika Mikoa ya Lindi na Pwani, jumla ya vijiji 6 vimepimwa katika Wilaya ya Nachingwea ambavyo ni Mtua,

Chindengenda, Kilimalindo, Nakegeli na timu iko Likwale inapima kijiji hicho. Vijiji 4 katika Wilaya ya Kilwa ni pamoja na Somanga, Matandu, Nangurukuru na Kilanje lanje. Vijiji saba (7) katika Wilaya ya Lindi Vijijini ambavyo ni Likong'o, Likwaya, Muungano, Nangulu, Mandingo, Mkwajuni na Mkwapa. Zoezi hili linaendelea katika Wilaya zingine.

(iii) Mabwawa mawili katika Wilaya za Kishapu na Mwanga na malambo 13 katika Wilaya za Chunya (1), Lindi Vijijini (2), Nachingwea (2), Kilwa (2), Maswa (2), Misungwi (1), Bariadi (1) na Longido (2), yako katika hatua mbali mbali za ujenzi.

(iv) Mashamba sita (6) ya malisho yameanzishwa na sekta binafsi katika Mikoa ya Tanga na Pwani na kuzalisha kibiashara marobota 25,000 ya hei.

(v) Aina mbali mbali ya mafunzo yametolewa kwa wataalam na wafugaji ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa zao la ngozi (washiriki 441), njia za asili za kuhifadhi malisho ya aasili (wafugaji 102 na wataalam 68) na udhibiti wa mbun'go na ugonjwa wa nagana (wataalam 18) ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto katika shughuli zao.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa niulize maswali madogo ya nyongeza. Katika majibu yake, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema katika maeneo yaliyotengwa baadhi yake ni Mikoa ya Lindi na Mtwara na baadhi ya wafugaji ambao wamepelekwa katika Mikoa hiyo ni wa kutoka eneo la Mbarali, Ihefu ambako kuna uharibifu mkubwa wa mazingira na mimi kama mwana-mazingira naunga mkono kuondoka kwa wafugaji hao huko Ihefu. Lakini, kule walikopelekwa hasa katika Mkoa wa Lindi na baadhi ya sehemu za Mkoa wa Pwani, si sehemu zenye mazingira mazuri kwa nyasi za ng'ombe kwa ajili ya kufuga. Majani ya sehemu zile yana *crude protein content* kidogo sana. Sasa ningependa kujua tathmini gani hasa ilifanywa hadi ukatokea uamuzi kwamba ng'ombe hawa wapelekwe Lindi kwenye ndorobo wengi sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali dogo la pili, kuhusu utengaji wa maeneo; Wilaya kama ya Kongwa ni Wilaya ndogo yenye wtu 300,000, tuna ng'ombe wengi, mbuzi wengi, kondoo wengi, punda, mbwa, paka, na kadhalika. Fursa ya kutenga maeneo hatuna kwa sababu tumebanana sana. Mheshimiwa atakubaliana nasi kwamba iko haja ya Ranchi ya Kongwa, sasa wananchi wakapewa ili tufuge kisasa humo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Kusini ikiwemo Mkoa wa Lindi, inafaa kwa ufugaji na ndio maana tangu enzi ya wamu ya kwanza ya Serikali kiliwekwa kituo cha udhibiti wa magonjwa kilichoko Naliendele ili hatimaye na maeneo ya Mikoa ya Kusini iweze kuingia kwenye ufugaji ikiwa tuna uwezo wa kudhibiti magionjwa, ndio maana kituo hicho kilitangulia mapemda. Maeneo mengi ya Mkoa wa Lindi yana malisho ya kutosha na yanafaa. Ni kweli kuna baadhi ya nyasi ubora wake siyo mzuri, baadhi ya majani mengine yana sumu, lakini wataalam wanayafahamu na njia za kukabiliana nayo wanazifahamu. Kwa

hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Job Ndugai, kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imetimiza azma ya muda mrefu ya kuona kuwa Mikoa ya Kusini ufugaji nao unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuikabidhi Ranchi ya Kongwa kwa Mamlaka ya Wilaya ya Kongwa. Serikali hata hivyo itashirikiana na Wilaya ya Kongwa kuhakikisha kuwa wafugaji wote, wananchi wote wa Wilaya ya Kongwa wanafanya ufugaji wa kisasa kama anaosema Mheshimiwa Mbunge ili kusudi wasihitaji maeneo zaidi ya ufugaji. Ufugaji wa kisasa hauhitaji kuomba maeneo makubwa zaidi kila siku. Unaweza ukafanya kitu kinachoitwa kwa kiingereza zero *grazing*. Ukiwa na ng'ombe wengi tu, unalima mashamba hayo hayo ambayo yanalimwa kwa sasa, yanaweza pia yakalimwa mashamba ya malisho na mfugaji yakawa na uwezo wa kuvuna yale majani ya malisho na kuweza kuwalisha mifugo wake wengi tu. Kwa mfano, heka 10 zikilimwa zinaweza zikamwezesha mfugaji kuzalisha malisho ya kutosheleza ng'ombe 150 kwa mwaka.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea! Ng'ombe wameishapata majibu ya kutosha na wafugaji bora mmeishaelezwa, tusiharibu utamu!

Na. 65

**Mikopo yenye Riba Nafuu kwa Vikundi vya Wanawake**

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKARI** aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake wa Pemba wanajitahidi sana kupambana na umaskini kwa kuunda vikundi mbali mbali vya ushirika *(SACCOS),* lakini tatizo linalowakabili ni ukosefu wa huduma za mikopo yenye riba nafuu na misaada hasa ile ya upatikanaji wa masoko ya bidhaa zao:-

Je, Seikali ina mpango gani wa kuwapatia mikopo hiyo na misaada pamoja na masoko ya uhakika kwa wajasiriamali hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakari, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya vyama vya ushirika vya akiba na mikopo upande wa Zanzibar siyo masuala ya Serikali ya Jamburi ya Muungano wa Tanzania. Vyama vya ushirika wa akiba na mikopo upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinaandikishwa chini ya sheria ya ushirika ya mwaka 1986 ya Zanzibar. Pia yupo Mrajis wa vyama vya ushirika Zanzibar ambaye ni tofauti na Mrajis wa vyama vya ushirika Tanzania Bara. Hivyo, tunamshauri Mheshimiwa apeleke suala hili kwa Mrajis wa vyama vya ushirika Zanzibar.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini napenda na mimi kumweleza kwamba mimi ni wa Muungano kwa sababu ni Mbunge, nimechaguliwa Pemba, lakini ni Mbunge wa Muungano. Kwa hiyo, nina haki ya kuuliza hata hapa kwa sababu natetea wanawake wote. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa licha ya mikopo ya benki mbali mbali kuwa na riba kubwa, lakini pia baadhi ya wanawake wajasiria mali wana uoga wa kukopa katika benki hizo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa elimu ya kuwatoa uoga hasa wale wa vijijini ili waweze kukopa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kuondosha tatizo hilo, wanawake wajasiriamali ni kuanzisha Benki ya wanawake. Je, mpango wa kuanzisha benki hiyo umefikia hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Swali la pili anajibu Mheshimiwa Sophia Simba. Uanze hilo kwanza!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ningependa kumjibu Mheshimiwa Faida Mohammed Bakari, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumjibu swali la pili hasa ambalo linazungumzia kuhusu benki. Ningependa kumfahamisha kwamba mchakato wa kuanzisha benki umefikia hatua nzuri na kwamba tumeishakuwa na kikao na Wabunge wanawake ama wale ambao wako katika Kamati ya Maendeleo ya Jamii na kuwafahamisha hatua ambazo tumezifika. Tunaamini kwamba benki itakapoanzishwa, wanawake watakuwa na sehemu ya kukimbilia. Benki hiyo, pamoja na kuwa ni benki itakayoanzishwa itakuwa ni benki ya biashara na haitakuwa *SACCOS*, lakini wanawake na wanaume wote wataruhusiwa kununua *shares* katika benki hiyo. Na benki hiyo itakuwa *unique,* ya aina yake kwa sababu tutakuwa na *department* itakayotoa ushauri wa kibiashara jinsi ya kutafuta masoko na jinsi ya kuanzisha bishara mbali mbali.

Kwa hiyo, nawashauri wanawake pamoja na wanaume wakati tutakapoanza kuuza hisa, wajitokeze kwa wingi kununua hisa kwa sababu benki hii inaanzishwa kutusaidia wanawake, lakini pia na wanaume wanakaribishwa kununua hisa. Ahsanteni sana! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza! Usibishane kuhusu habari ya Muungano, yeye ameuliza wanawake wanapata matatizo huko. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba yeye ni mmojawapo ambapo anaweza kuhamasisha wale wananchi namna ya kufanya mikopo na kutafuta maafisa biashara

ambao wanaweza kuwafanyia michanganuo na kuwatoa uoga wafanyabiashara hao. Tulimjibu swali lake kwa sababu tunajua yeye ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano.

Na. 66

**Masharti ya Mikoa – Elimu ya Juu**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeandaa mfuko maalum wa kuendeleza elimu ya juu kwa kuwakopesha wanafunzi, na kuwa dhamana ya mkopo ni Hati ya Nyumba au Wadhamini wenye uwezo, na kwa kuwa, asilimia kubwa ya wanafunzi hao hutoa katika familia duni kiasi kwamba, hawaaminiki katika jamii:-

(a) Je, kwa nini Serikali isilenge masharti na kuruhusu mwanafunzi ajidhamini mwenyewe baada ya kuanza kazi kwa sharti la kukatwa mshahara wake?

(b) Kwa kuwa, mwanafunzi kijijini hawezi kumudu gharama za Hati; na kwa kuwa Hati hazitolewi katika maeneo hayo. Je, Serikali haioni kuwa, huo mfuko utatumika au kufaidisha wachache waishio mijini au wenye uwezo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum napenda kwanza kutoa ufafanuzi mfupi tu ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sio kweli kuwa wanafunzi wanaotoka katika familia duni hawaaminiki katika jamii. Wanafunzi hawa wanaaminika kama walivyo watu wengine. Aidha, mikopo hii inawalenga wao zaidi ambao wana uwezo kielimu lakini hawana uwezo kiuchumi kugharamia masomo yao. Baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Tabora, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaotumika na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoa mikopo ni sawa na ule ambao unapendekezwa na Mheshimiwa Mbunge ambao unamwezesha mwombaji mkopo kujidhamini mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na taratibu za utoaji mikopo katika asasi za fedha na mabenki ambazo zinahitaji mkopaji kuwa na dhamana ya msingi (*primary security)* ambayo hupima uwezo wa huyo mkopaji kurejesha mkopo na dhamana ya ziada *(secondary security)* ambayo hutumika kama kinga ya mkopo iwapo mkopaji atashindwa kurejesha mkopo aliokopa, wakopaji wa elimu ya juu hujidhamini wenyewe kwa matumaini kuwa elimu wanayopata inawajengea uwezo (ujuzi na maarifa) wa kuwawezesha kurejesha mikopo waliyokopa baada ya kuhitimu masomo yao.

Mheshimiwa Spika, nyaraka zinazohitajika kuambatanishwa wakati wa maombi ya mikopo sio dhamana ya ziada bali ni vithibitisho vinavyosaidia kumtambua mwombaji na vingine vinasaidia kupima uwezo wa kiuchumi wa mwombaji. Kwa taratibu zilizopo mwombaji mkopo anahitajika kuambatanisha mojawapo tu ya vitambulisho vifuatavyo:-

Kwanza, kwa waombaji wasio na ajira:-

Barua kutoka kwa Mtendaji wa Kata au Halmashauri ya Kijiji/Mtaa.
Barua kutoka kwa kiongozi wake wa Dini.
Barua kutoka kwa Mdhamini.

Pili, kwa waombaji walioajiriwa:-

Nakala ya hati ya mali isiyohamishika.
Nakala ya hati ya malipo ya mshahara (*Salary Slip).*
Nakala ya hati ya bima ya maisha.
Taarifa ya Benki iliyothibitishwa kuhusu mwenendo wa akaunti ya benki ya mwombaji.
Uthibitisho wa udhamini kutoka kwa Kampuni binafsi, Asasi isiyo ya Kiserikali, au Kikundi cha Kijumuiya.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa waombaji kutoka mijini na vijijini wanaweza kukopa kutoka Bodi ya Mikopo endapo watakuwa tayari kujidhamini wenyewe na kuambatanisha Hati za utambulisho kama nilivyoeleza hapo juu. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuwezesha kila Mtanzania kuwa na maisha bora na kwa kuwa utaratibu aliousema siyo wote ambao wanaweza wakatimiza masharti hayo; je, Serikali haioni umuhimu wa kuwakopesha wanafunzi wote bila kujali madaraja utaratibu huo ambao unatumia sasa kwa kujali madaraja ya wanafunzi ambao wamefaulu vizuri, kwa mfano wanaokopeshwa sasa hivi ni wale ambao waliofaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza. Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo ni kuwapunguza wale ambao hawana uwezo na kuwekosesha kuwa na maisha bora kama walivyosema? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwanne Mchemba kwa sababu niliwahi kusoma kwenye gazeti kwamba anasaidia watoto yatima. Nafikiri pia huenda anataka kuanza kuwasaidia wanafunzi wa elimu ya Juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada pongezi hizo naomba nimjibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nafikiri sera ya uchangiaji katika nchi yetu, katika Wizara mbalimbali inaeleweka ikiwemo na elimu ya juu. Sheria ya Bodi ya mikopo ilipoanzishwa ilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza hii sera ya uchangiaji kwa Watanzania wanaofaulu. Lakini ambao hawana uwezo kifedha kama nilivyoeleza katika jibu langu la

msingi. Hata hivyo, bodi ya mikopo pamoja na Wizara kwa wakati muafaka na kwa wakati unaotakiwa kila mwaka inabidi kutafsiri sheria hii katika kutunga kanuni ambazo kutegemea na fedha iliyopo tunaangalia Watanzania waliofaulu na wahitaji kwa sababu nia yetu ni wale wahitaji kama nilivyosema.

Sasa katika hawa wahitaji waliofaulu fedha iliyopo inaweza ikalipia wangapi. *Criteria* hiyo ni muhimu kwa sababu fedha haiwezi kutosha kulipia wote walioufaulu ambao wamechaguliwa kwenda vyuo vikuu. Kwa hali hiyo, inabidi tuangalie na kwa mwaka uliopita wa fedha mwaka 2006/2007 tuliangalia wale wa *division one* kwa wavulana na *division one* na *two* kwa wasichana kutegemea na fedha ilivyokuwa inaturuhusu. Tutakumbuka mwaka wa fedha 2004/2005 wanafunzi wote walilipiwa asilimia 100. Pamoja na hiyo kuangalia *division one* na two tunaangalia ni kiwango gani tunachoweza kuwalipia. Kwa hiyo, hii inabadilika kila mwaka, siyo kitu cha kudumu kwa sababu ni taratibu tu za kutekeleza na kama nilivyosema zitategemea hali iliyopo ya fedha katika Wizara na katika Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kawaida Mheshimiwa Spika, anakuwa *liberal* hasa kwa maswali ya nyongeza. Mimi nimejitahidi nimekuwa *very strict,* bado maswali matatu yamebaki. Sasa nimejifunza kwamba tunajibu kirefu na tunauliza kirefu mno hatufiki. Kwa hiyo, kila siku wengine watakosa maswali. Lakini kitu kimoja cha kufurahisha hapa kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja anatoka upande wa kushoto kwangu anasema Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini huangalii kushoto, tukisimama kuulizwa swali la nyongeza hutuchagui. Kuna Mheshimiwa Mbunge mwingine ameandika kutoka kulia anasema Mheshimiwa Naibu Spika, huku kwetu kulia hutuoni kabisa. Kwa hiyo, jamani nawahakikishieni kwamba suala hilo limejifuta lenyewe. Hivyo, Mheshimiwa Spika, anaona pande zote. (*Makofi*)

Tunapenda kufurahi kwamba leo tumefikiwa na wageni, Mashehe wa Mji wa Dodoma wakiongozwa na Shehe Ahmed Zubeir, Kiongozi wa Msafara. Mnawaona wamekaa pale. Kwa hiyo, ni Mashehe katika mji wetu wa Dodoma wameona waje washirikiane na sisi katika kipindi hiki cha maswali wameletwa na Mheshimiwa Madeje. Karibuni Waheshimiwa Mashehe. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Hatujawaona.

**NAIBU SPIKA:** Hamjawaona. Samahani Mashehe mnaombwa msimame ingawa mmeonekana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wengine, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu wanao wageni wao wapiga kura wa kutoka Sumve na Magu ni majimbo jirani. Naomba wasimame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Janet Kahama anaomba nimtambulishe Mheshimiwa Peter Kabisa ambaye nafasi yake amechukua Mheshimiwa Azan Zungu. Karibu sana Mheshimiwa Kabisa kuona ukumbi mpya wewe hukuuona huu. (*Makofi*)

Halafu Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma wanapenda tuwatambue wageni wao, Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa na Mjumbe wa UWT Diwani Amina Chimata, naomba msimame mliopo. Lakini kuna mgeni mmoja hebu Joachim. Joachim ni kitinda mimba wa Mheshimiwa Jenista Mhagama. Anasoma shule ya *Martin Luther* hapa Dodoma *standard four*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo anaomba niwatangazie wageni wake, Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Mbezi Luise, Mwenyekiti wa CCM kata ya Manzese na Mheshimiwa Mjumbe wa Halmashauri ya CCM Manzese, karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu tuna Mheshimiwa Nyaulawa anaomba tuwatangazie wageni wake waliopo hapa, Mwenyekiti wa CCM wa Mbeya Vijijini, alikuwa Mbunge miaka 15 iliyopita ,mimi namfahamu naomba asimame Mzee Mswila, naona ametoka!

Halafu naomba nitangaze kuhusu vikao. Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, anaomba niwatangazie wajumbe wake wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwamba leo tarehe 16/4/2007 saa sita mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati katika ukumbi namba 133, mnaomba mfike bila kukosa lakini mjue saa saba kuna Kikao cha CCM katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali Mheshimiwa John Cheyo, anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane tarehe 16 katika chumba namba 432 saa sita leo mchana. Kama nilivyosema Katibu Msaidizi wa Chama cha Mapinduzi anaomba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa saba.

Halafu Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda anaomba wajumbe wake leo tarehe 16 wakutane katika chumba 231 ghorofa ya pili jengo la utawala saa tano asubuhi.

Halafu Mheshimiwa Mkuchika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anaomba wajumbe wakutane leo tarehe 16 saa tano asubuhi katika chumba 219.

Mheshimiwa Spika, anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Kudumu, kwanza, Kamati ya Uongozi kukutana kesho saa saba na nusu kwenye chumba cha mkutano na kesho Jumatano, Kamati ya Huduma za Bunge, saa saba na nusu katika chumba hicho hicho.

Matangazo mengine ni kwamba juzi Mheshimiwa Spika, alitangaza Mheshimiwa Dunstan Mkapa, alipotelewa na binti yake kule Morogoro. Anafurahi kutangaza kwamba binti huyo amepatikana. Kwa hiyo, anamshukuru Mheshimiwa Spika, kwa kutangaza kwa sababu amepatikana katika Wilaya moja huko Mvomero. (*Makofi*)

Tangazo lingine Profesa Msolla amefiwa na mdogo wake profesa Msola mwingine. Kwa hiyo, nafikiri wana maziko leo Iringa. Lakini alifiwa Dar es Salaam. Pia tumeambiwa tutangaze kwamba Mheshimiwa Ponsiano Nyami, amefiwa na baba yake

mzazi. Mazishi yatakuwa leo huko Nkasi. Nadhani hili kwa utaratibu wetu ofisi itafanya hiyo kazi. Baada ya hayo matangazo nafikiri Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na hoja iliyopo mbele yetu. (*Makofi*)

***Miswada ya Sheria ya Serikali***

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 (The Prevention and Combating of Corruption,** *Bill, 2007*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Tunao wachangia 12 na tunatarajia kwamba asubuhi hii tumalize kuchangie halafu jioni Waziri anayehusika aweze kutoa maelezo kwa hoja zilizotolewa na tuingie kwenye kazi nyingine.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache juu ya Muswada wa kuzuia kupambana na rushwa. Lakini kabla sijafanya hivyo naomba nisahihishe jina langu siyo Geoffrey ni Godfrey.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niungane na wenzangu ambao tayari wameshachangia Muswada huu. Ninaamini kwamba wamechangia mengi na pengine tusiwe na mapya sana lakini mimi nitajitahidi walau yale ambayo hayakusemwa sana niyasemee kwa kifupi sana.

Niishukuru Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi na katika uchumi wa nchi yoyote ile duniani. Naishukuru sana kwa maana hiyo Serikali na Wizara pamoja na watalaam wake. Lakini pia, kwa sababu na mimi ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuchangia katika Miswada naomba nitumie fursa hii basi kumshukuru sana jirani yangu ndugu yetu, Mtutura Abdallah Mtutura ambaye nadhani ametoka kwanza kushinda kwa kura nyingi kule Tunduru kwa maana hiyo kukiletea Chama cha Mapinduzi heshima kubwa sana katika Bunge letu. Lakini pia tunashukuru na wale wenzetu ambao walikwenda huko Tunduru na kuungana na wenzetu wa Tunduru kwa ajili ya kukipigia kampeni Chama cha Mapinduzi na kwa maana hiyo, kuwezesha huu ushindi mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumze machache kuhusu Muswada wenyewe. Jambo la kwanza, mimi naomba nizungumzie ubovu wa mikataba. Mikataba mingi ambayo Serikali imekuwa inaingia kwa kweli ni mibovu. Mimi nilikuwa nafuatilia ziara ya Mheshimiwa Rais, moja alifanya huko nchi za Scandinavia. Mheshimiwa Rais alinukuliwa na vyombo vya habari akisema kwamba tunaingia kwenye mikataba mibovu kwa sababu pia inaonekana watalaamu wetu wanaojihusisha na kuingia mikataba hawana sifa nzuri, kwa maana nyingine ni kwamba *they are incompetent*. Sasa kauli hiyo kama ni ya kweli kwa sababu ilinukuliwa na vyombo vya habari, mimi nadhani kwa kweli tupo mahali pabaya sana. Tunahitaji kufanya jitihada za dhati za kuhakikisha kwamba mikataba inayoingiwa haiwi mzigo wala haiharibu uchumi wa taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nishauri katika hili kwamba tusione aibu kuwatumia watalaamu wetu wa vyuo vikuu na wengine katika maeneo

mengine ambayo hawapo Serikalini, wanaweza kutusaidia sana. Tuna watalaamu wa mikataba mabingwa vyuo vikuu, tuna watalaamu wengine wazuri maeneo mengine ambao wanaweza kuwa pia wakaisaidia Serikali katika kuhakikisha kwamba mikataba inayoingiwa ni mizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nilikuwa na mtazamo pia mwingine tofauti na kama alivyosema Mheshimiwa Rais, kwamba watalaamu wetu inawezakana kwamba *they are incompetent.* Mimi siamini sana, kwamba tunao wataalamu wazuri. Lakini kinachotusumbua hapa ni hizi *ten percent* katika mikataba ndicho kinachotusumbua sana. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiria wale wanaoingia mikataba ikiwa itabainika kwamba mikataba mingi ni mibovu kama ambavyo sasa tumeshabaini na Mheshimiwa Rais amesema mara nyingi, mikataba ya madini mingi ni mibovu. Tumeshashuhudia mkataba *wa ATCL* ulikuwa mbovu, mkataba wa *Net Group Solution* ulikuwa mbovu. Kwa hiyo, mimi naamini watu wanaoingia kwenye mikataba hii wao ndiyo waadhibitiwe. Adhabu ambazo zinazopendekezwa kweli kwenye Muswada huu kwa kweli ni ndogo.

Watu wataendelea ku-*relax*, watu wataendelea kupata hizi *ten percent* kwa sababu kwanza wanajua wana fedha na jeuri hiyo ya fedha ndiyo itakayowafanya waendelee kuingia mikataba mibovu wakijua kwamba hata Serikali ikijua hakuna hatua zozote ambazo zinaweza zikachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la rushwa ya ngono. Rushwa ya ngono ni udhalilishaji wa utu wa mtu. Ni uzalilishaji wa haki za binadamu hasa akina mama na wasichana. Hawa ndiyo kwa kweli wanaokumbwa na rushwa ya ngono. Sasa mimi nilikuwa nafikiri ili kuondoa jeuri ya pesa kwa hawa watu ambao wanaweza wakatumia rushwa ya ngono na kwa kweli siyo udhalilishaji wa utu wa mtu lakini pia ni wana *abuse professional* kwa sababu watu wengine wanaopewa kazi hawana sifa kwa sababu tu mtu amepata ngono basi anafikiri huyu anastahili kupewa kazi hiyo wakati kimsingi anakuwa hana sifa zile ambazo anastahili kuwa nazo. Mimi nilikuwa nafikiri katika maeneo kama haya kunatakiwa adhabu ziwe kali sana. Nchi nyingi za Kiarabu na nyingine za Kikomunisti hakuna rushwa huko. Wale ambao wanajihushwa na rushwa wanapopatikana hunyongwa. Kwa maana hiyo rushwa kwao wanaogopa kuingia vinginevyo ni *risk* sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi si muumini sana wa adhabu ya kifo kwa sababu ukimnyonga mtu au ukimpiga risasi bado hujamfundisha. Nilikuwa nafikiri tuwe na adhabu kali za vifungo ikiwezekana hata hawa wafungwe maisha yao yote. Hapo ndipo wengine wanaweza kujifunza. Tatizo moja katika nchi hii tunaoneana haya. Nani amfunge paka kengele ndiyo tatizo kubwa. Kwa hiyo, kumekuwa na kuonea haya kwingi kwa sababu aliyefanya kosa au aliyetuhumiwa ni mwenzetu, kwa maana hiyo, hatuwezi kumfunga. (*Makofi*)

Mimi nilikuwa nataka nishauri yanapotokea kwa mfano masuala haya, kwa ujumla kiundwe chombo kingine ambacho inawezekana katika Serikali kiwe *independent* cha kufuatilia. Kwa mfano zimefanywa *interview*, *interview* hizi zimefanywa kihalali? Je, waliopata kazi hizi wana sifa halali zile zilizotangazwa? Mimi nadhani hili linaweza

pia likasaidia. Itakapobainika kwamba wale ambao wameingia au hawana sifa zinazostahili, basi na wenyewe pia wachukuliwe hatua kali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ningependa kulisemea ni juu ya rushwa ndogo na rushwa kubwa. Ni kweli Waziri alipokuwa anawasilisha Muswada alipata tabu sana ku-*define* rushwa na bado hakuna *definition* moja ya rushwa. Kwa maana hiyo, mimi naona rushwa ndogo na kubwa nilikuwa nafikiri zipimwe kutokana na madhara yake. Naomba nitoe mfano, daktari anaweza akadai shilingi 10,000 tu kwa ajili ya kumtibu mgonjwa. Lakini kwa sababu mgonjwa hana fedha daktari huyu hamtibu mgonjwa na anapoteza maisha. Mimi hii ningeifikiri ni rushwa kubwa sana kwa sababu madhara yake ni makubwa sana. (*Makofi*)

Ni tofauti na Afisa wa Ardhi ambaye anamdai mtu anayeomba kiwanja rushwa ya shilingi 500,000, amemnyima kiwanja kwa sababu mtu huyu ameshindwa kutoa shilingi laki tano. Madhara yake siyo makubwa kama vile madhara ya kutaka tu rushwa ya shilingi 10,000 lakini ambayo inapoteza maisha ya uhai wa mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia niseme kwamba watu watakaosema uongo au watakaotoa taarifa za uongo, hapa nataka kusema pia kwamba watu ambao watasingiziwa kuwe na utaratibu mzuri wa kuwalinda. Kwa maana hiyo, wale ambao watatoa taarifa za uongo watatoa taarifa ambazo wao wenyewe pengine hawana uhakika, pengine na wenyewe kwa sababu wapewe rushwa na wenyewe wahesabiwe kwamba ni wala rushwa na adhabu kali pia zichukuliwe dhidi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie suala jingine kwamba mahakamani sasa hivi kupotea kwa mafaili kumekuwa nayo ni *fashion*. Mafaili yanapotea mahakamani bila utaratibu na unaweza ukajiuliza hivi mafaili haya yanatembea? Hivi mafaili haya yana miguu? Vyovyote vile wanaohusika ni wale ambao wapo mahakamani. Mara nyingi mafaili ambayo yamekuwa yanapotea mahakamani au hata mikononi mwa wanaochunguza kesi zenyewe mimi nilikuwa nadhani na hawa wenyewe wahesabiwe kwamba ni wala rushwa kwa sababu wamehusika katika kupoteza mafaili haya, siyo bure wamepewa fedha ndiyo sababu wakapoteza. Mimi naamini mafaili haya kama nilivyosema hayatembei na kwa vile hayatembei ni wahusika wa taasisi hizi watakuwa wamehusika. Kwa maana hiyo pia na wenyewe sheria iwatambue kwamba ni wala rushwa vile vile na hatua kali dhidi yao zichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwa sababu wenzangu wamezungumzia mengi, ninaomba niseme jambo la mwisho kwamba kama tunataka kweli kabisa kutokomeza rushwa katika nchi hii, kwanza tunatakiwa tuwe na utashi wa kiasi *(political will)*. Bila hili tutakuwa sawa na kupiga gitaa na tunaowapigia gitaa ni mbuzi na mbuzi hawa hawawezi kucheza hili gitaa. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana upande wa viongozi kuwe na utashi wa kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka niseme kwamba viongozi tuliokuwa nao siku za nyuma walikuwa kielelezo sahihi sana katika kupambana na

rushwa katika nchi hii. Wote tunajua Mheshimiwa Mwalimu Nyerere, alivyokuwa kielelezo yeye mwenyewe mtu safi na jinsi alivyokuwa anapambana na rushwa.

Lakini pia Zanzibar Mheshimiwa Rais wa wakati Abeid Amani Karume, alivyokuwa mkali kwenye masuala ya rushwa na kwa maana hiyo watu hawakuwa wanacheza. Lakini zaidi wengi tunamkumbuka Marehemu Sokoine alivyokuwa mtu mwenye nidhamu, mwenye busara, lakini mkali sana kwenye masuala ya watu ambao walikuwa wanatumia fedha za nchi hii bila utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu waliwahi k utupa magunia ya fedha jinsi alivyokuwa mkali wakati huo Mheshimiwa Edward M. Sokoine. Kwa hiyo, mimi nadhani tunataka tuwe na viongozi wa aina hiyo. Viongozi wa aina ya Nyerere, viongozi wa aina ya akina Karume, viongozi wa aina ya Sokoine. Bila hivyo hatutaweza kupambana na kumaliza tatizo la rushwa hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naiomba sana Serikali suala la kujuana, suala la kuoneana haya, lisiwepo tena na huu ndiyo ugonjwa mkubwa sana katika nchi hii. Tunatunga sheria nzuri, lakini utekelezaji wake ndiyo tatizo kubwa. Kama nilivyosema ma faili ya wakubwa yatapotea lakini mafaili ya akina Zambi, kina Kasusura hayo hayawezi kupotea, yatapatikana.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tuwe na utashi wa kiasi, viongozi wawe tayari, vinginevyo tutapitisha hii sheria nzuri, watu wamekaa hapa wanazungumzia mambo mazuri ya kuishauri Serikali lakini utekelezaji wa sheria hii tunaweza tukaona kwamba hautakuwa mzuri na kwa maana hiyo, Watanzania wakatulaumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba nichangie hayo na mimi niseme kwamba kwa kweli naunga mkono hoja lakini naomba sana utekelezaji. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika hoja hii muhimu ambayo umuhimu wake unafahamika na Watanzania kwa sababu rushwa au tuseme ufisadi ndio tatizo kubwa linaloikabili nchi hii.

Kwanza, ningeanza na *definition* yaani ya kutafsiri hilo neno. Kwa sababu hili neno rushwa tukiangalia vizuri katika hizi *dictionary* inaonyesha kwamba rushwa kwa kingereza ni *graft* kile kitendo cha kumpa mtu fedha ili akupe haki hako. Lakini neno *corruption* lina maana pana zaidi. Lina maana ya ule uozo wote ambao sasa ndiyo unaofanya taifa lishindwe kwende mbele kwa sababu ni pamoja na rushwa kama hizo zinazozungumziwa kama rushwa za ngono, au tuseme ufisadi unaoendelea kule kwenye Halmashauri mbalimbali. Ule mfumo ambao unazalisha kwa mfano watu wanaoitwa vibaka, machangudoa, watoto wa mitaani ni uozo mzima wa mfumo mzima. Hili suala halikuanza leo kwa sababu unaona hata Serikali ya Mkoloni kwenye mwaka 1958 tumeambiwa ilikuwa imesha-*notice* kwamba hii rushwa/ufisadi ni tatizo, wakatungia sheria.

Mwalimu Nyerere katika Historia ya Tanzania anaonekana kwamba alilivalia njuga na alipambana nalo kwa kila hali na pia hapa ningependa pia tumkumbuke Mheshimiwa Sokoine, kwa jinsi alivyoweza kujitoa kwa hali na mali mpaka hata uhai wake kwa nchi kupambana na hili suala.

Sasa kilichotokea baadaye ni kwamba baada ya hawa viongozi kuondoka katika nchi hii, yaani kuondoka kimwili, sasa ndio wale ambao walikuwa wanapenda ufisadi wakaona kwamba ni wakati sasa wa kubadilisha ikiwa ni *turning point*. Kwa hiyo, tunaona sasa ile *turning point* ni kwamba mfumo uliopo ni wa kulinda ufisadi kwamba sasa hata vyombo vinavyoundwa kama *PCB* kinakuwa kama ni chombo cha ku- *fashion* na siyo cha kuweza ku-*combat* kama vile ambavyo tunaelezwa. Sasa tuangalie ni kwa nini mimi kwa mtazamo wangu naona kwamba kwa sababu tumekuwa na *confusion* yaani mfumo gani ambao sasa unaendelea. Kwa mfano, suala la mfumo wa ubepari unafahamika kwamba mfumo wa ubepari ni nini na unafanyaje shughuli zake , ni utaratibu mzima unafahamika kihistoria. Kuna mfumo wa ujamaa ambao pia unafahamika kwamba taratibu zake zikoje na mifumo yote miwili inachukia ufisadi.

Kwa hiyo, tukiangalia historia tutaona kwamba nchi za kibepari zenyewe kama Uingereza, Marekani zinachukia huo ufisadi na wamepambana nao kiasi kwamba wameweza kuendelea baada ya kuwa wameudhibiti. Nchi za kijamaa vile vile tukiangalia *China, Korea, Vietnam* wanachukia huu mfumo na kwa kweli wamepambana nao ndiyo maana wameweza kupata maendeleo. Lakini sasa kwa Tanzania huu Mfumo tunaukumbatia na inaonyesha kwamba Serikali haina nia madhubuti ya kupambana na rushwa katika nchi hii ndiyo maana mambo mengi yanafanyika kwa usiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Wabunge watambue kwamba tutakuja kuhukumiwa na historia vibaya sana kwa sababu sisi tunakuwa pia ni sehemu ya huu mfumo wa kulinda rushwa/ufisadi. Kwa mfano, mimi sioni mantiki ya Waheshimiwa Wabunge, kuwa tunateuliwa kushiriki katika bodi mbambali za mashirika ambayo hayo mashirika kwanza mgogoro mkubwa sasa hivi ni mikataba na hiyo mikataba ndiyo imesababisha ile rushwa kubwa katika nchi hii inakuwa sasa ni tatizo kubwa. Lakini Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda tunakaa mle. Ningependa Serikali ijaribu kuchunguza kwa mfano ukichukulia kama *NBC* au *TANAPA* Serikali ichunguze jinsi wanavyogawana ile *bonus* na unakuta Wabunge wapo humo. Sasa itakuwaje, Wabunge hao kweli wanaweza kusimamia vizuri masuala ya kupambana na rushwa kama wao wanakuwa tena ni sehemu ya vitu kama hivyo.

Serikali imekuwa na usiri mkubwa kuhusu mikataba, ambayo ni kilio chetu Bungeni. Sasa *role* yetu sisi ya kusimamia ipo wapi kama hatuwezi kuihimiza Serikali ilete hiyo mikataba hapa Bungeni. Suala kama la rada, suala la *Richmond* Wabunge, tunashindwa kulijadili kwa sababu tunaogopa kwamba tunaweza tukaonekana tunaipinga Serikali. Lakini Mbunge yeyote wa Chama chochote ambaye ni *back- bencher* una sababu gani ya kutopinga *cabinet* kwa sababu wewe humo mle, kazi yako wewe ni kuwakilisha wananchi na sisi tumetumwa kuja kuwakilisha wananchi. Sasa ile kujipendekeza kunakusaidia nini, kwanza, kutakugharimu wewe kura zako maana hili

Bunge litaonekana lilikuwa ni Bunge ambalo lilikuwa dhaifu zaidi, kwa hiyo, wote hapa mwaka 2010 hakuna mtu atakanyaga humu, itasaidia nini? *(Makofi)*

Ni bora tuwe pamoja na wananchi wetu ambao hao ndiyo wanaotuleta humu. Jambo lingine ni kuhusu *management* ya fedha katika nchi yetu. Tayari mmeona mambo yanayojitokeza ni kwamba fedha nyingi ni zile ambazo zinapotea. Tuchukulie kama suala la elimu fedha za MMEM zimeliwa sana. Lakini Serikali haichukui hatua yoyote pamoja na wananchi kupiga kelele. Suala la MMES unaona kwamba limefikia mahali ambapo Serikali sasa inakwenda jukumu lake la kujenga mashule ambalo sasa lile limewekwa kwa wananchi.

Kwa hiyo, wananchi sasa ndiyo watakaojenga mashule badala ya Serikali. Lakini hatuelewi ni kwa sababu gani, maana michango imekuwa ni ya lazima badala ya hiari. Sasa kama ni kodi ya maendeleo imerudi, basi wananchi waambiwe kwamba sasa kodi inatozwa, kwa hiyo, wanajenga mashule kwa migongo yao. Vinginevyo Serikali inawajibika kujenga mashule, madeni yalishakopwa. Sasa hayo madeni ambayo tunalipa, yalienda wapi? Hizi fedha ambazo zimekuja mpaka jana zinafanya kazi gani. Kwa hiyo, ningependa kuwatahadharisha Wabunge kwamba kwa kukumbatia mfumo wa rushwa ambao unakataliwa na nchi zote za kibapari na za kijamaa ni kuliangamiza Taifa letu na hakuna atakayefaidika kwa sababu hii ni *time bomb,* wananchi wanafuatilia na wanazidi kuelimika. Kinachofuata sasa wote hapa tunakuja kufukuzwa kazi na itaonyesha wazi kwamba sisi ndiyo tuliokuwa tunakumbatia rushwa katika hiyo *historical period* tuliyopo sasa hivi.

Suala lingine ambalo ningependa kushauri, ni kuhusu namna ya kupambana na rushwa yenyewe. Kweli sheria mbalimbali zinaweza kutungwa. Lakini haziwezi kutekelezwa kama ule utashi wa kisiasa haupo. Tunaweza kuangalia jinsi ambavyo nchi hata za jirani zimeshughulikia hili suala. Nchi ya Kenya baada ya Serikali ya NARC kuingia imejitahidi kwa kiasi kikubwa na inaonyesha kwamba walikuwa wana dhamira ya kweli ya kupambana. Nchi ya Malawi, watu wanaacha hata mambo ya kuabudu vyama, wanaamua kurudi kwa wananchi na kupambana na rushwa. Kwa hiyo, inaonyesha wazi kwamba inawezekana. Lakini kama utashi haupo ndiyo tunaona nchi kama Nigeria pamoja na hii ya kwetu kwamba sasa rushwa imekuwa kama ni kitu cha kawaida lakini kitu ambacho kitakuja kutugharimu sana.

Jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la kulazimisha wananchi kufanya kazi za nguvu yaani *force labour* ya kuwa fedha ambazo zinatakiwa kutimiza au kufanya kazi hiyo, zimechukuliwa kwa njia ya rushwa. Kwa mfano, sasa masuala ya kulazimisha wananchi kujenga mashule ambalo ni jukumu la Serikali hii ndiyo ingesababisha wananchi wakapambana na mkoloni kwa sababu ili waweze kuwa huru. Sasa itafikia mahali wananchi waanze kulamizishwa wajenge mabarabara, waanze kulazimishwa wajenge hospitali. Waanze kulazimishwa kujenga hata miradi ya maji kwa sababu Serikali inakwepa jukumu lake ili kulinda masuala ya ufisadi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi ya kusema kwa sababu inafahamika wazi kwamba rushwa ipo Tanzania na huu mfumo unalindwa na Serikali. Na Waheshimiwa Wabunge wanaamua kuwa sehemu ya huo mfumo. Sasa hili ndilo ambalo tuliangalie tulibadili ili kusudi tuweze kufanya kazi ya wananchi, ambayo ndiyo iliyotutuma kufanya hapa. Tuangalie ile mikataba yote iletwe hapa tuiangalie. Hii ndiyo kazi yetu ya usimamisi.. Kama Serikai inakataa basi tusiingie humu Bungeni. Kwa sababu sasa tuna maana gani ya kuingia humu Bungeni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Kuhusu Utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mhh! Kuhusu utaratibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 50, kifungu cha 7(viii), kwamba ni marufuku Mbunge kutumia lugha ya kuudhi. Wakati Mheshimiwa Wangwe akijadili hoja ya rushwa alisema kwamba Waheshimiwa Wabunge hapa wanajipendekeza, nadhani neno hilo siyo zuri kwa wale waliowachagua wengi wataona kwamba hawatendewi haki. Naomba afute usemi wake. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu.......!

**NAIBU SPIKA:** Sijakuita. Mimi sijamaliza hili la kwanza. Mheshimiwa Wambura kuhusu ile kwamba uondoe usemi wako kwamba wanajipendekeza.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Kiswahili ni lugha yangu ya tatu, huenda hilo neno nilikuwa na maana ambayo Mheshimiwa *Chief Whip* hakuipata vizuri, lakini nilikuwa namaanisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wasijirahisi. Kwa hiyo, hili neno nalifuta. Lakini nasema.....!

**NAIBU SPIKA:** inakuwa *even worse* tumekuelewa!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hiyo hiyo, kwamba Wabunge wamepewa uhuru wa kuzungumza na sidhani kama ni sahihi kwa *Chief Whip* mara kwa mara kuingilia uhuru huo wa Wabunge. Hoja ambayo ameizungumza Mheshimiwa Chacha muda mfupi uliopita aliizungumza Mheshimiwa Mzindakaya juzi, na akasema kabisa kwamba Wabunge wanaogopa kuzungumza kwa sababu ya kusubiri kupewa uwaziri na *Chief Whip* hakuzungumza hicho kitu. Lakini ni kwa sababu Mheshimiwa Chacha anatokea CHADEMA, Chacha anatokea upinzani, ndiyo inakuwa kazi ya *Chief Whip* kuzuia Wabunge wa Upinzani kuongea.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Naibu Spika, hili ulipige marufuku ili tuwe huru kuzungumza ndiyo kazi iliyotuleta hapa. Watu wametuchagua tuje kuzungumza hawakutuchagua tuje kukaa kimya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto kazi ya kulinda mazungumzo humu ndani inafanywa na Mheshimiwa Spika au Naibu Spika. Kwa hiyo, naelewa wakati gani

inasemwa nini, ndiyo maana anaendelea kuongea kwa sababu sikuona kama kitu cha ajabu sana. Mpeni muda wake. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hilo suala umeliona na Wabunge wote wameliona.

**NAIBU SPIKA:** Sasa unaendelea kujadili.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kwa hiyo, mimi sitakuwa na mengi ila nasisitiza kwamba Waheshimiwa wote tuwe kitu kimoja, tuache mambo ya vyama humu Bungeni, tushikamane kama Wabunge wa wananchi, ma-*back bencher* tuangalie hii Serikali inafanya nini, vinginevyo wananchi radhi zao zitatumwagikia sisi kwa sababu sisi ndiyo tuliochaguliwa kuja kuangalia mambo yao hapa Bungeni. Sina mengi ya kusema nashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba niungane na wenzangu kwanza kutoa rambi rambi kwa aliyekuwa Mbunge kwa Bunge hili Tukufu, Dr. Aaron Chiduo na kwamba basi tumwombee kwa Mwenyezi Mungu ili roho yake aweze kuiweka mahali pema Peponi. Amen!

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu tunaoujadili ni Muswada ambao kwa kweli ukiuangalia kwa haraka haraka unaweza ukadhani ni Muswada ambao una utata. Lakini ukiuangaliea tena kwa wepesi wepesi unaona kwamba ni Muswada ambao ni vema tukauzungumza vema kwa maslahi ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni mdudu. Rushwa siku zote imekuwa ni chanzo cha matatizo katika jamii. Marehemu hayati Baba wa Taifa, aliwahi kusema kwamba rushwa ni adui wa haki na kwenye vyama vya siasa tukasema kwamba hilo ni sahihi na tukathibitisha. Lakini rushwa inafanyika katika mazingira ambayo mara nyingi ni usiri na pengine yanahitaji kufanyiwa kazi kuweza kuthibitika kama ni rushwa. Rushwa unaweza ukafananisha na ngono. Wanaofanya ngono ni watu wawili, kuthibitisha kwa rushwa vile vile inakuwa ni tatizo. Lakini kupitia Muswada huu nadhani ni muda muafaka kwa Watanzania kwanza, kujaribu kuangalia mantiki ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa haraka haraka nimeona ni Muswada ambao kwanza unafaa kwa sababu unafuta sheria ya mwaka 1971 ya PCB, lakini vile vile Muswada umekuwa shirikishi kwanza kwa sababu umehusisha wadau mbalimbali. Lakini katika Muswada huu napenda nigusie mambo yafuatayo:-

Kama Waheshimiwa Wabunge tujikumbushe kwamba Mbunge una kazi gani. Kazi ya Mbunge ya kwanza ni uwakilishi anaokuja kufanya ndani ya chombo hiki. Lakini kazi ya pili ni kutunga sheria na kazi ya tatu, ni kuisimamia Serikali. Sasa najaribu kuangalia nini dhamira ya Muswada huu. Mheshimiwa Rais wakati wa ufunguzi wa Bunge hili tarehe 30 mwezi Desemba 2005 aliweka bayana dhamira yake na Serikali ya Awamu ya Nne ya kupigana na rushwa. Dhamira ambayo sote inatusukuma

tuzungumze kwa mustakabali wa Taifa hili. Ukizungumza rushwa hatumwangalii mtu, kwa sababu katika mazingira ambayo kuna rushwa ukimwona mtu kanonanona kidogo unasema kwa sababu ya rushwa. Katika mazingira haya tunakuwa tunatiliana mashaka, huyu anakula rushwa, huyu hali rushwa na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mzindakaya juzi alisema kwamba kuna Waziri mmoja amempa *notice* bado haja-*respond,* mimi nadhani labda kama kweli anaweza kufanya hivyo, basi angetuambia ni Waziri gani. Kwa sababu haya mambo ya kusema nimempa fulani, fulani bado haitupi *spirit* ya kupigana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuujadili Muswada huu kwa kuangalia ni kwa namna gani Serikali inapaswa kuheshimu Muswada na hasa kwa kuangalia kwamba kumekuwa na mianya mingi sana ya rushwa. Mheshimiwa Jaji Warioba, aliainisha mianya ya rushwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ikazungumzia namna gani ya kukabiliana nayo na ikaweka mkakati wa kupambana na rushwa na sasa dhamira hiyo ya kisiasa bado ipo kwamba tunapambana na rushwa. Lakini ukiangalia kwenye ripoti ya Mkaguzi Mkuu ambayo ameiainisha vizuri sana, kuna Wizara, Idara za Serikali na vyombo mbalimbali ambavyo vimeshindwa kutumia fedha vizuri, bado tunasema kwamba Maafisa Wahasibu watachukuliwa hatua za kukatwa mapato na mishahara yao na baadhi ya sehemu. Huu ni utani, hivi kila mwaka mamilioni yanakuwa yanapotea tunasema kwamba tutawa-*charge* tutawa-*surcharge* hawa Maafisa Wahasibu, bado dhamira ya kupamana na rushwa haitoshi. Lazima tuongeze kasi ili tuone ni namna gani tunaweza kupambana na rushwa.

Kupitia Muswada huu nadhani kuna haja ya kuainisha kabisa kwamba Maafisa Wahasibu wote ambao wanakutwa wametumia fedha vibaya za umma, basi wachukuliwe hatua kama ni wala rushwa. Bila kufanya hivyo, hatuwezi kupambana na rushwa itakuwa ni rushwa nadharia. Tungependa kupambana na rushwa katika misingi ambayo kweli inaondoa suala la usiri na mambo mbalimbali. Leo hii ukiingia mtaani hata Watanzania wanasema bwana kuna rushwa, kuna rushwa. Rushwa gani, watasema mikataba mibovu. Rushwa gani mambo ya *Richmond*. Rushwa gani mambo ya *IPTL*, rushwa gani mambo ya *ATC*. Rushwa gani mambo ya *NBC.* Ni mambo mengi yanazungumzwa lakini bado sisi kama Bunge na kama Serikali hatujachukua hatua zozote madhubuti za kupamabana na watu ambao wamehusika kwa namna moja au kwa namna yoyote ile na suala hili linalozungumzwa la mambo ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inakuwa kama ni kitendawili, kila leo watu wanazungumza mambo ya rushwa. Watasema rushwa. Lakini hatua za makusudi bado hazichukuliwi. Juzi juzi hapa iliundwa Kamati ya Mheshimiwa Ndugai ambayo ilitoa mapendekezo ya jinsi gani ya kuweza kuboresha utendaji kazi wa Bunge. Lakini mpaka leo hii sijui Kamati hii imefichwa wapi? Ripoti yake hatuioni, na sasa bila kuboresha Bunge, inakuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa sababu rushwa yenyewe pamoja na kwamba Bunge likiwa na meno itasaidia kuweza kupambana na rushwa. *Independence of the Parliament is the paramount in fighting against corruption.* Sasa kama Bunge letu bado litakuwa katika hali hii bado tuna tatizo kubwa sana kwamba namna gani tupambane na

rushwa. Na kama tuheshimu mihimili mitatu, iweje leo Bunge lisipewe yale mamlaka yake ya kibunge ambayo hata Katiba inasema. Mimi nilikuwa nashauri kwamba kwa hili lazima tuweke dhamira kweli kweli isiwe dhamira ambayo ni nadharia. Tuweke dhamira vitendo, siyo nadharia ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mifano michache tu. Ukiangalia mifano nchi ya Rwanda, Rwanda wamepambana na rushwa kweli kwel ndiyo maana uchumi wa Rwanda unasonga mbele. Ukikamatika au ukisikika kwamba umekula rushwa Rwanda uwe ni nani, Rais mwenyewe anakuita na anakuambia hapo hapo. Unakwenda na maji, kama ni adhabu basi unapata adhabu inayostahili. Lakini leo hii hapa Tanzania hebu tujiulize ni wala rushwa wangapi na hasa rushwa zile nene, hata mmoja ameshakamatwa na kuadhibiwa kikamilifu.

Mimi naona kama bado tunafanya kama utani. Ni vema tujaribu kuona ni namna gani sasa Serikali kupitia Muswada huu tunadhibiti suala la rushwa. Hii TAKUKURU ni chombo ambacho tumekiunda. Tusipokipa mamlaka ya kuwa *independent* na kwamba kifanye kazi zake zaidi kwa uangalifu na kwa umakini bila kuingiliwa na chombo kingine chochote cha Serikali au namna yoyote ile hakitaweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *DPP* ni suala la Kikatiba, lakini ni vema basi tuainishe kwamba ni kwa namna gani huyu Mkurugenzi wa TAKUKURU naye analindwa katika kutekeleza wajibu wake. Taasisi nzima lazima iweze kuhuishwa, analindwa katika kutekeleza wajibu wake. Taasisi nzima lazima iweze kuhuishwa, na iweze kuboreshwa, vinginevyo bila kufanya vile tutakuwa hatufanyi kazi. Hawa watu watafanya kazi ambayo itakuwa haina tija yoyote kwa Taifa hili tutaweka mapesa mengi kwa taasisi hii lakini bado malengo ya kupambana na rushwa yatakuwa bado hayajakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona faini ni vichekesho, hivi mtu amekula rushwa nene, unamwambia alipe shilingi milioni 3 au milioni 10 au 15 *maximum,* hivi kweli tunaitendea haki nchi hii? Kuna haja ya kuangalia. Nchi zingine ukila rushwa, hata Marekani, ukila rushwa maana yake adhabu yake wewe moja kwa moja kufilisiwa, na kufungwa. Sasa sisi hapa kwanza ukila rushwa unaonekana mtu wa maana katika jamii. Kwa sababu wala rushwa wengi ukiwaona wanafanikiwa, na jamii wala haiwakemei. Kwa hiyo, wala si suala la Wabunge peke yake, hata jamii ishiriki kikamilifu katika suala la kukemea juu ya rushwa. Bila kuwa shirikishi katika suala la rushwa kuanzia kwenye jamii na kwenye taasisi na vyombo vyote bado suala la rushwa litatusumbua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie vile vile suala zima la dhamira za kisiasa. Mheshimiwa Rais ana dhamira nzuri sana. Lakini nikiangalia ukisikiliza vyombo vya habari, Taasisi za Dini, wanasema Mheshimiwa Rais wanaomshauri hawamshauri vizuri. Hana Wasaidizi wazuri. Sasa jamani huyu Mheshimiwa Rais, sisi sote tuna wajibu wa kumsaidia katika masuala ya utekelezaji wa majukumu ya kitaifa.

Hapa tunapoangalia kwamba ni nani anawajibika zaidi ni sisi sote tunapaswa kuwajibika zaidi. Rushwa ina athari kubwa sana kwa jamii yote. Na mimi ningependa kusema kwamba kwa nchi ya Kenya wao rushwa wamezoea ni kama kuhamisha mfuko mmoja huku kuingiza huku, hivi kama ni fedha. Lakini uchumi wa Kenya unakua, rushwa wanakula na uchumi wa Kenya unakua. Lakini sisi hapa kwetu hawa wanaokula rushwa sijui zinahamishwa zinakwenda nje, hatuzioni! Si bora basi zibaki hapa, walau zibaki hapa zijenge uchumi wa nchi. Maana yake utasikia zipelekwe kwenye benki za huko nje na kadhalika. Lakini wenzetu wa Kenya wakila rushwa wanajenga uchumi wao. Ningeshauri kwamba sasa ni muda muafaka tujaribu kuangalia Muswada huu kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia *Schedule of Amendments* kwa kweli imejaribu ku-*incorporate* mambo mengi, imesema kuhusu *powers* za *DPP,* muda wa kushughulikia majalada na kadha wa kadha. Mimi nadhani kuna haja ya kuboresha kidogo kwamba bado *Director General* wa TAKUKURU apewe nafasi ambayo hawezi kuingiliwa katika maamuzi au utekelezaji wa shughuli zake za kiutendaji. Kuhusu suala la marekebisho ya kimsingi mimi nafikiri kuna haja ya kuangalia kwa sababu chimbuko la rushwa vile vile tusikatae jamani vyama vya siasa ni sehemu ya chimbuko la rushwa. Vyama vya siasa vyote. Sasa tuangalie kwamba sheria mama inasemaje, na katika sheria hii tujaribu kuainisha kwamba ni namna gani huyu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU naye ajaribu kuingia kwenye vyama vya siasa katika kuangalia kwamba namna gani mwenendo mzima wa masuala kisiasa unavyoendeshwa hapa nchini. Tumpe nguvu hiyo ya kuweza kushiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba tuepuke mashinikizo, kama kuna shinikizo juu ya sheria kama hizi za Miswada kama hii tuepuke, wenzetu kama Uingereza wao walitunga Sheria yao ya kwanza mwaka 1906. Ikafanyiwa marekebisho mwaka 1916 mpaka leo hii wanaitumia hiyo hiyo. Na Sheria yao ni kali kweli, ukila rushwa Uingereza, si Waziri Mkuu si nani unahojiwa na vyombo vinavyohusika. Wala siyo siri. Sasa ninaomba na sisi katika Muswada huu tutumie nafasi kuipa meno Taasisi yetu ya TAKUKURU.

Lakini ukiangalia Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumekwenda mbele kwa vitu vingi sana. Hata sisi katika Muswada huu tumefanya marekebisho haya na tunaleta hapa Bungeni, ni moja ya nchi ambayo imepiga hatua katika masuala haya ya kupambana na rushwa. Ndiyo maana ukiangalia katika ile orodha ya nchi zinazotumika katika mambo ya rushwa sisi tuko nafuu kuliko baadhi ya nchi zingine katika Bara la Afrika. Lakini jamii yetu ndiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Mwanri aliizungumzia hapa juzi.

Mzee mzima huyu aliizungumza sahihi kabisa akaweka falsafa yote ya mambo ya rushwa na hasa kuainisha suala zima la uchumi wa nchi hii. Ninashauri kwamba Watanzania sasa ni nafasi yetu na kila Mtanzania ana wajibu wa kujaribu kujenga suala zima la maadili. Kwa sababu rushwa inatokana vile vile na maadili ya nchi.

Ukipenda rushwa hata ungependa namna gani, rushwa haina kipimo. Utapenda kula rushwa nene, nene, nene, nene, nene! Lakini kama maadili ya Watanzania

yatajaribu kubadilika itasaidia kupambana na rushwa. Hapa katika Muswada huu hatumwangalia sijui Waziri, au nani hapana ni sote *collective* tujiangalie kwamba tuna wajibu wa kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa lengo la kutaka kuunga mkono hoja hii. Kwanza, naipongeza Serikali kwamba imeweza kutuwasilishia Muswada huu katika kipindi ambacho ni muafaka. Ni wakati ambao tunahitaji kuwa na sheria yenye kulenga kuzuia rushwa lakini na kukusudia kuondokana na rushwa. Kwa hiyo, makusudio ya Muswada kwamba ni kutaka kuona Tanzania inakuwa huru bila kuwa na rushwa ni lengo ambalo mimi naliunga mkono sana, kwa hali hiyo naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa ni kitu ambacho ni kipana sana na hakika hata tafrisi yake ni pana sana, inapenya na inapita katika maeneo mbalimbali. Lakini vyovyote vile mimi nasema rushwa inaendelea kuwa fedheha, ni aibu, ni unyanyaji, ni udhalilishaji na hakuna mahali popote ambapo rushwa kwa namna yoyote ama kutolewa au kupokelewa ama mtu kuiomba au kitendo chochote kile anachokifanya ambacho kinaashiria rushwa kwamba kinaweza kupewa sifa. Chochote kile kitakachofanywa kitakuwa kinaashiria aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa najaribu kutafakari sana Muswada huu ulipotoka na hata wakati tunautafakari kwamba hivi hasa ni sababu gani ambazo zimesababisha kuwe na chanzo cha rushwa. Hakika viko vyanzo vingi sana. Baadhi ni vile ambavyo ipo hofu ya jamii ama watu wanaopata huduma wanakuwa na wasiwasi kwamba inawezekana mimi sitapata huduma nzuri. Kwa hiyo, mtu anaona afadhali atangulize pesa kusudi pesa ile imsaidie yeye kupata ile huduma nzuri. Lakini lipo eneo lingine ambalo ni ubinafsi. Mtu anakwenda kuingia mkataba wa ajabu ajabu kusudi apate pesa nyingi afaidike afanye masuala yake mwenyewe nje ya kipato chake. Sasa huo ni ubinafsi. Lakini lipo eneo lingine ambalo ni umaskini tu na hakika niseme mimi wakati mwingine naona pengine ni ujinga wa watu kutokufahamu. Kwa hiyo, mtu anajikuta anajiingiza katika rushwa ndogo ndogo za vitu vidogo vidogo ambavyo vinaitwa chochote kwa msingi ya kwamba afaidike hasa na kitu chochote cha maana lakini hakika anajikuta amekwishajiingiza katika uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa tulikuwa tumefikishwa mahali ambapo kila mmoja alifikiria kwamba pengine apate ile huduma, ama hata kama haina maana, hata kama ni mzuri lakini anatangulia kuwa na mawazo kwamba labda mimi niende kule nitangulize kwanza labda sijui niite kujisafishia nafasi ya kufanikiwa. Hali hii ndiyo ilikuwa imefikia mahali hapo. Sasa kwa Muswada huu kuja mimi naamini kabisa kwamba hali yetu itaweza kuwa ni nzuri na vyombo vyetu mbali mbali vitaweza kuwa ni safi. Wasi wasi uliokuwepo kwa wananchi kwenda kusajili kesi zao Mahakamani badala ya shilingi mia tano wanatozwa elfu tano mpaka elfu hamsini. Kesi zinacheleweshwa, mtu anaona aendelee kuwa mahabusu, dhamana zinakataliwa na mambo mengine, yote haya ni mlolongo ambao ulikuwa unasababisha msukumo wa kuona kwamba vitendo vya rushwa vinakithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema sisi wananchi wa Tanzania, viongozi na wasiokuwa viongozi kwa namna mbalimbali ndani ya madhehebu ya imani zetu mbalimbali, ndani ya vikundi vyetu mbalimbali, makundi yetu mbalimbali, ndani ya mikusanyiko yoyote, sisi lazima tulenge katika vita ya aina moja. Lazima tukubaliane

kwamba lazima sisi wote tuichukie rushwa. Na ni lazima tuikatae rushwa na tuhakikishe kwamba katika mapambano haya ya vita hii ya kupambana na rushwa ya kuhakikisha kwamba tunaikomesha sisi wote, lazima tuhakikishe kwamba tunakuwa kitu kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema rushwa ndogo ndogo, na rushwa kubwa kubwa mimi kwangu sioni kitu gani ambacho naweza kusema kwamba hiki kina madhara kidogo, hiki kina madhara makubwa. Mimi nasema rushwa kama rushwa ina madhara makubwa sana. Kwa sababu zile rushwa zinazoitwa rushwa ndogo ndogo wenzangu wamewahi kuzijadili, zina madhara makubwa sana kwa matokeo ya jamii yetu kwa ujumla. Zimesababisha vifo visivyokuwa vya lazima, vimesababisha watu waliokuwa na haki wasipewe haki zao. Zimesababisha watu kugeuza maneno wakatoa ushuhuda hata hawakuwa kwenye tukio. Lakini kwa sababu tu hana haki anajua amepewa kitu fulani basi anasonga mbele kwenda kutoa ushuhuda ambao haukuwa sawa sawa. Kwa hiyo, hakuna rushwa iliyo nzuri. Rushwa kubwa na ndogo lazima tuzipige vita zote sawa sawa na kwa nguvu kuhakikisha kwamba tunaziondoa. Imani iliyokwisha kujengeka kwamba tanguliza kitu fulani ama omba kitu fulani ili kuweza kutenda , ama huduma uliotakiwa kuitenda au kupokea huduma uliyotakiwa kuipokea. Hiki kitu ndiyo tutaweza kukifisha kama kweli tutakuwa tumesimama pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema ili tulifanikishe hili basi tunatakiwa tupate elimu ya kutosha. Elimu ya kutosha bila kuchoka. Elimu hii, Serikali iipitishe katika vyombo vyake vyote ya kuhakikisha wananchi wanalisikia hili. Kila mmoja ambaye anapata nafasi ya kuzungumza na wenzake lazima ahakikishe kwamba hili jambo analisemea. Na ni lazima tunapolizungumzia jambo hili tulione kabisa ni aibu. Iwe ni aibu kuona kwamba wewe unataka kudai hongo ama rushwa ya namna yoyote ama wewe unajiandaa kupokea hongo rushwa kwa namna yoyote ile ama wewe unajiandaa kutoa iwe ni aibu. Sasa katika aibu hizi mimi nilivyokuwa nikijaribu kuzifikiria nilipotazama Muswada nikatazama lile eneo ambalo linatoa makosa na adhabu mimi nikaona pengine labda sikuweza kusoma na kumaliza vizuri kwa sababu sikuwa na Muswada wenyewe mpaka nimeuomba jana, ikawa sasa pengine sikuutafakari vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipoangalia mimi nimekuwa natazama ni wapi ambapo huku mtoa rushwa yaani anayekwishathibitisha kwamba sasa amejishirikisha na hongo imedhibiti ni wapi anapoaibishwa? Kwa sababu yeye analiabisha Taifa, anaaibisha jamii, yeye anaaibishwa wapi? Ni lazima huyu mtoa hongo au anayethibitika naye aaibishwe katika jamii ya Kitanzania lazima aaibishwe. Aaibishwe kwa kuhakikisha kwamba katika adhabu anazopewa iwe ni kutaifishiwa mali yake, iwe ni kufungwa, iwe ni kutoa faini lakini lazima achapwe viboko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viboko hivi ni aibu, kwa huyu ni mtu mzima, anaweza kuwa kiongozi aliyepewa mamlaka ya kuchaguliwa, amepewa mamlaka ya kuteuliwa, amepewa mamlaka ya kuheshimiwa na mamlaka yoyote ile iliyompa nafasi. Huyu akichapwa viboko ni aibu kubwa kweli kweli, kwa hiyo, hii aibu itamfanya sasa yeye na jamii nyingine waweze kuogopa.

Lakini basi mimi nasema kwamba, anayethibitika na rushwa, pia lazima jamii imtengee, huyu ni mbovu sana, ni aibu sana ni kitu cha hatari sana katika jamii. Sasa hivi *Rift Valley* imetikisa nchi watu wameogopa kula nyama, na hii habari ya rushwa itikise nchi, jamii ione kabisa mtu ambaye ameshiriki katika vitendo vya rushwa, lazima jamii imetengee. Jamii inamtenga vipi, kama huyu alikuwa ni mfanyakazi, maana yake afukuzwe kazi, kama huyu alikuwa ni mfanyabiashara anyang'anywe leseni, kama huyu alikuwa ni kiongozi asitishwe uongozi wake anyimwe haki ya kuendelea kuomba ile nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili haya yaweze kufanyika yanatakiwa yafanyike katika jamii ambayo hakika, kwa kuzingatia sheria na taratibu, yote yanatendeka kwa haki. Isije ikafanyika hila ya kutaka kumwangamizamtu, kutaka kumkomesha, kutaka kuona kwamba basi kusudi huyu ifike mahali ionekane yeye amehusika na vitendo vile vya rushwa.

Kwa hiyo, kuwepo na mjadala uliotosheleza na uchunguzi unaotosheleza ili kuweza kumtia hatiani mhusika. Kwa sababu adhabu hizi zitakuwa ni adhabu ambazo hakika zinalenga kukomesha kwamba jambo hili likome tuache kulisikia kabisa, iwe ni Tanzania, hakika iliyo *free from corruption*. Kama tunataka Tanzania *free from corruption* lazima tuwe *serious* na kuhakikisha kwamba hatua zozote ambazo zinachukuliwa na mwananchi mmoja mmoja na vyombo vilivyopewa mamlaka na watu waliopewa mamlaka lazima wahakikishe kwamba wanatenda haki bila kuonea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengi ambapo rushwa inatokana na mazingira, tunao mahakimu wachache kwa mfano, inachukua muda mrefu sana mwananchi aliyekwenda kuitaka haki Mahakamani kuipata, ni moja ya eneo ambalo Serikali lazima ijidhatiti kuona kwamba hivi inaongeza vipi mahakimu ili wananchi wapate haki zao haraka wanapozipeleka haki zao mahakamani. (*Makofi*)

Eneo lingine tunaliona lipo katika hospitali, huduma za hospitali ni hafifu sana, wahudumu wa huduma hizi ni wachache sana wakiwa madaktari, wataalamu ni kwa vipi mwananchi anaona mtu wake anataka kukata roho, mtu wake anahitaji huduma ya haraka, *operation* inatakiwa, *theatre* imeajaa wanasema vyombo hamna yeye afanye nini? Inabidi atoe pesa kusudi mtu wake apate huduma haraka. Hapa Serikali inatakiwa iboreshe huduma hizi haraka, kusudi iweze kuendana na Muswada huu kuona kwamba huduma zile ambazo zinakwenda kutaka kumhudumia mwananchi ni lazima ziwe bora zaidi.

Sasa hivi kazi kubwa tunayoifanya ya kujenga shule zetu za kata ni zoezi zuri sana tunalifanya, lakini mimi naomba Serikali iendelee ku-*monitor* na kuhakikisha kwamba shule zetu za kata zinakuwa nzuri sana tusifanye sasa Maafisa Elimu na wengine na wenye mamlaka ya kuamua mtoto aende shule gani, wakalazimika kukimbia shule fulani kwenda shule fulani, watatota rushwa, kwa sababu wataona kwamba akisoma shule ile hatapata huduma, wala elimu nzuri, kwa hiyo, ni vizuri ampeleke katika shule nzuri. Itakuwa ni *cloud*, ili kuhakikisha kwamba hakuna msongamano basi inatumika njia nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema haya Serikali yetu ikiyazingatia ikaweza kuyasimamia na sisi wenyewe tukaona kwamba tunasimama katika kuhakikisha kwamba hakika tunaisaidia Serikali yetu kuona kwamba inaondokana na rushwa na tunakuwa na taifa lililo uhuru. Mimi naamini tunaweza tukapiga hatua nzuri na Muswada huu ukaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tunapitisha sheria nyingi hapa Bungeni, lakini ukitazama utekelezwaji wa zile sheria, limekuwa ni tatizo. Mimi naomba Muswada huu sasa utoe mamlaka ya kuona kwamba tunatathimini mafanikio yake baada ya kipindi fulani ili mwananchi mwenyewe ambaye hasa ndiye tunayemlenga, basi aweze na yeye kuwa na hakika na kujibu kwamba sasa rushwa imepungua na kipindi fulani aseme sasa kweli rushwa hakuna. (*Makofi*)

Lakini katika vyombo vilevile wenzetu tunawapa madaraka ya kwenda kuingia katika mikataba mikubwa inayotoa haki inayokwenda kusimamia jina la nchi yetu, ni lazima na wenyewe wawe ni wenye maadili kweli kweli mazuri ya kuonyesha kwamba kila wanachosimamia ni kwa manufaa ya nchi yetu. Wenzangu wametoa mifano ya viongozi waliotangulia akiwemo Baba wa Taifa, Marehemu Sokoine, Marehemu Karume, wote hawa tazama wamekwisha kuiaga dunia. Lakini tunajifunza nini kwa? Ni heshima gani tunayowapa le? Ni kuendelea kuwa na Taifa ambalo linarushwa baada ya wao kuondoka. Mimi nafikiri tusiwaogope wao tunatakiwa kusimamia maadili mazuri. Kwa sababu tabia njema na mwenendo mzuri ndiyo ambao utakaoweza kujenga Taifa letu, lazima kila kiongozi na kila mwananchi na kila mmoja mahali alipo kila mtoa huduma anayejua kwamba pale alipo anatakiwa kutoa huduma ama ya kuajiriwa, au ya hiari, lazima aitoe kwa kiwango kinachostahili na bila kutafuta visingizio vyovyote. Na yule ambaye anaweza kuwa ameshindwa sasa kufikia vile viwango, wananchi wenyewe watoe taarifa kwamba fulani ndiye mwenye matatizo kwenye eneo letu. Kwa hiyo, utafutwe utaratibu wa kuwashirikisha wananchi katika ku-*asses* mienendo ya viongozi wetu au viongozi wao, toka muda kwa muda kama njia ya kuweza kuona kwamba tunapunguza tatizo hili la rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo pia naliunga mkono ni suala zima la kulipa Bunge nafasi yake. Inawezekana katika maeneo fulani fulani, Bunge linakuwa ni zito kutoa maamuzi, mimi naomba katika hili silioni kama kuna tatizo lolote la kuachia Bunge kulipa nafasi uwezo wa kujitegemea, kutekeleza Ibara yaliyo ndani ya Katiba ya kuhakikisha kwamba Bunge linaisimamia Serikali. Mimi sioni kama kuna tatizo lolote, pengine tu kama kuna mahali pamecheleweshwa, parekebishwe tu ili jambo liweze kufanyika, kwa sababu ni kweli Bunge lipo, na Bunge lina nafasi yake. Sasa inatakiwa litumie nafasi yake na hasa katika masuala haya ambayo ni magumu yanaondoa heshima ya nchi yetu, yanaondoa heshima ya Watanzania yanashusha hadhi yetu, ni mahali pazuri ambapo mimi nafikiri basi Bunge lingeweza likapewa heshima yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaporudia kukushukuru nimependekeza kabisa kwamba wanaojihusisha na rushwa wapewe adhabu, waaibishwe, wapigwe viboko, na kila Mtanzania ajihusishe katika vita hii, asiwepo anayemwonyesha mwenzake kidole,

vingine vinamwangalia akadhani yeye hahusiki, ili katika umoja huu ndipo hakika tunapoweza kupambana na rushwa na tukaweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru, ahsante sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika Muswada huu wa Rushwa. Lakini naomba nitamke mapema kwamba sitaunga mkono hoja hii kutokana na upungufu mkubwa ambao upo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu hata tukiangalia tu katika tafsiri ya maneno, hapa tunazungumzia, *key term,* rushwa. Pamoja na kwamba tunasema rushwa ni pana, kwa hiyo, haina *definition* ya uhakika. Lakini bado kuna yale mazingira ya rushwa ambayo yalipaswa kabisa yaelezwe yawe *defined*. Kwa mfano *corrupt practice* ni zipi hazijaelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikiendelea ni kwamba kuna suala la *informal* na *Whistle blower*, katika *definition* wanasema kwamba "*informer includes a person who in good faith response for the commission of an offence to the bureau and includes a whistel blower"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Waziri na wasaidizi wake, wengi wanaelewa lugha ya Kiingereza, na hata tukienda kwenye *encyclopaedia* tunapata *definition. Informer* ni mtu ambaye ni *agent* ambaye analipwa, hiyo inaeleweka. Lakini *whistle brower* huyu halipwi, na mara nyingi anakuwa kwenye taasisi, kwa mfano, tunakumbuka kuna kipindi Dr. Mwakyembe alieleza alivyokuwa *NBC* ni namna gani alivyokuwa *Whistle blower*, hakuwa *informer*. Kwa hiyo, tunaomba hizi tafsiri ambazo naamini Wizara inazielewa vizuri, waziweke vizuri ili wananchi waelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba pia niendelee. Suala la *DPP* limeongelewa kwa kirefu sana, na hata jana kwenye *kipima joto* kimeonyesha wazi, asilimia 65 ya wananchi wanasema hapana, na ninaamini mpaka tunapomaliza huu Muswada hicho kipima baridi kikirudiwa nadhani asilimai 98 itasema *DPP* asihusishwe kwenye taasisi ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hilo nisiliongelee kwa sababu Wabunge wengi wameliongelea. Lakini nasema pia hata kama imeshindikana tunaambiwa *TRA*, wao mashitaka yao hawapitishi kwa *DPP*, kwa nini hili la rushwa tunalipeleka kule? Na je, *TRA* wao walitumia kifungu gani cha Katiba kumtoa *DPP* katika mashitaka yao. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea kwenye suala zima la Ibara ya 14 ya Muswada huu ni suala lazima la *transparency*, ukurasa wa 15. Nikisoma kile kifungu kinasema The *Bureau shall on or before 31st March, in every year, by such late date as the President can allow, submit to the President a report on is activities in the previous year.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa naona kwamba, Ibara hii inatofautiana kabisa na Ibara ya 4 ambayo inasema *information* iwe *disseminated* kwa wananchi. Sasa kama Rais anapelekewa, sisi wananchi tunapataje, wananchi wa kawaida achilia mbali Wabunge wanapataje hii taarifa? Kwa hiyo, nilikuwa naomba basi kipengele hicho, kiongezwe kwamba *and the same to be tabled before the Parliament*, ili sisi Wabunge tuweze sasa kuelewa hiyo ripoti, na sisi ndiyo tutaweza kuwaeleza wananchi wetu. Vinginevyo ikibaki kwamba inapelekwa tu kwa Rais bado umma wa wananchi utakuwa hauelewi ripoti hiyo. Lakini Tanzania imeridhia mikataba mingi, pamoja na mikataba hiyo ni ule wa Umoja wa Mataifa, na ule wa *Africa Union*, naomba niusome, ili tuone ni jinsi gani, hii taasisi inataka kukiuka mikataba ambayo nchi yenyewe imesharidhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba nisome, *transparency and access to information should be adopted in the bill* na hii ya *Union Convention* inasema hivi. Hii ni *article 9* ya AU ambayo inasema, *each state party shall adopt such registration and either mention to give effect to the right of access to any information, that is required to assist in the fight against corruption and related offence.* Hiyo ni *AU.* Lakini pia tukiangalia *the United Nations Convetion Against Corruption, Article 7, 4 provides that each state party shall in accordance with a fundamental principal of its domestic law and avoid to adopt maintains and strength any system that promote transparency and prevent conflict of interest. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazungumzia suala la *conflict of interests*, hii TAKURU ipo chini ya Waziri na chini ya Ofisi ya Rais, mimi naamini Waziri sio malaika wala Waziri sio Mungu, kwa maana hiyo anaweza na yeye akafanya makosa. Kama Waziri muhusika anafanya makosa amekutwa anatumia rushwa, je, hii TAKURU itawezaje kumdhibiti, itawezaje kumchunguza Waziri ambaye ni bosi wao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza kwamba, ni lazima TAKURU au TAKUKURU sasa hivi, ipewe *operational independence* yaani uhuru wa utekelezaji. Ili waweze kuwadhibiti watu wote hakuna mtu ambaye yuko *above law whether* ni Waziri au ni nani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hii taasisi ipatiwe uhuru wa utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie suala la uteuzi wa wafanyakazi ambalo linajumuisha pia na Mkurugenzi wa hii Taasisi. Tunavyoona uteuzi huu kwa kweli hauko sahihi, kwamba ni ridhaa ya mtu mmoja.

Kwa hiyo, nafikiria kuna umuhimu wa hawa watu wawe *vetted*, kama ilivyo kwa majaji. Hata ukisoma kwenye Katiba yetu Ibara ya 110(2)(3) inaonyesha ni jinsi gani majaji wanateuliwa na jinsi gani wanaondolewa. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwa taasisi muhimu kama hii basi ni lazima pia kuwe na utaratibu ule ule ili kufuata haki, kwa sababu labda tutoe mfano. Kwa mfano, kama Rais ndiye anamteua huyu mtu, na labda kuna tatizo limetokea kwenye ofisi ya Rais, hivi si inakuwa rahisi tu huyu Rais kumfukuza kazi mtu huyu? Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kuwe na taratibu ambazo

zitakuwa kikatiba kabisa ili huyu mtu awe huru kufanya kazi zake. Hiyo taasisi ni nzito, kwa hiyo, naomba tuipe meno ili iweze kufanya kazi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee tena Ibara ya 7, kuonyesha kazi za hii taasisi ambayo moja wapo inasema kwamba itakuwa inashughulikia tu masuala katika mashirika ya umma, mashirika binafsi na mashirika ya Serikali. Sasa mimi nashindwa kuelewa, hivi vyama vya siasa au mashirika ya kidini na hapa nitajikita zaidi kwenye mashirika kwa sababu naona haya ya kisiasa labda yanaweza yaka-*dilute* Muswada mzima, na nashukuru pia Mashehe wapo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba mimi…!

**NAIBU SPIKA:** Wameshaenda.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mkatoliki, lakini pia naamini kuna dini nyingine za kikristo na za kiislamu. Tumekuwa katika kuchangishana, kujenga kigango ni kanisa dogo, inachukua mwaka. Lakini sasa hivi kuna makanisa makubwa sio tu Dar es Salaam, sehemu nyingi, na unaambiwa kanisa hili ni la mtu fulani, yaani la mtu binafsi amejenga. Sasa tunajiuliza hizi pesa kweli zinatoka wapi? Kwa hiyo, mimi naomba kujua ni kwa nini mashirika ya dini pia hayajaainishwa katika kipengele hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nataka kuchangia, ni kuhusu Madaraka ya Bunge. Wiki iliyopita mambo mengi yaliongelewa lakini kubwa likawa ni hili la madaraka ya Bunge kwamba Bunge letu halina meno, wengine wakasema lina meno ya *plastic*, wengine wakasema linahitaji meno ya chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda mimi niungane kabisa nisema kwamba Bunge letu halina meno, lakini nikiangalia Katiba ambayo tumeambiwa ndiyo *supreme* unaona kabisa ni jinsi gani Wabunge wanapaswa kuwa na meno, kuna meno lakini naomba kujua ni kitu gani kinafanya Wabunge wasitumie meno? Ukiangalia kifungu cha Ibara ya Katiba 63(3) (d) na hasa kile cha (e), tumeona kabisa kwamba rushwa nyingi ambazo wanasema ni zile rushwa nene, zipo katika mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi toka nimekuwa Mbunge sijaona mkataba hata mmoja umeletwa Bungeni lakini kifungu cha (d) naomba nikisome, kinasema, "kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano, na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kujua hii kazi ya Wabunge ambayo ni kujadili na kuridhia imeporwa na nani? Na huyo mtu ana madaraka gani kuliko Katiba? Mimi nilikuwa naomba Waziri atakapokuwa analeta majumuisho atuambie ni kwa sababu gani Bunge la Jamhuri ya Muungano, halijadili mikataba wala kuridhia Mikataba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ambacho nataka kuongelea ni kuhusu ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu. Tunaambiwa kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja tu Serikali ya Tanzania, imeweza kupoteza shilingi bilioni 700. Nadhani wananchi wananisikia, wanaelewa, bilioni yaani ni sifuri tisa, unaweka 700 halafu unaongeza sifuri tisa, huko nyuma, kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vyuo vya elimu ya juu wanafunzi wengi wamekosa mikopo, wanateseka, lakini kwa wanafunzi tulionao Tanzania ambao ni chini ya 50,000 wangepewa walau shilingi milioni moja tu, wangekuwa wametumia shilingi bilioni 50 tu wakati tuna hasara ya shilingi bilioni 700 kwa mwaka mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana tuone ni kwa nini huu upotevu wa hela umetokana na nini? Na Mkaguzi wa Mahesabu anasema kwamba upotevu huu unatokana na uzembe, anasema ni uzembe na kutokujua sijui mahesabu. Lakini tunaangalia, kama bilioni 700, ukitoa bilioni 50 hizo za wanafunzi, tunabaki na shilingi bilioni 650, bilioni 650 barabara zetu ni mbovu mno, huduma za afya hakuna, shule ndiyo hizo. Kwa hiyo, mimi naamini kama kweli, hii sio rushwa basi nilikuwa naomba Waziri atuambie inawezekanaje Serikali ipoteze shilingi bilioni 700 kwa mwaka mmoja, wakati wananchi wanaendelea kulalamika.

Lingine ambalo lilichangiwa lilikuwa ni suala la *culture*, kwamba walau watoto wafundishwe *culture*, utamaduni kwamba rushwa ni mbaya. Lakini hata kama unamfundisha huyu mtoto kwamba rushwa ni mbaya wakati sisi wakubwa tumeingia madarakani kwa kwa rushwa wengi. Sasa huyu mtoto hata mkimfudisha na wakati anaona *reality* kwa sababu tunasema *practice what you preach*, sasa kama tuna *preach* tusipambane na rushwa wakati tuna *practice this is the contradiction*.

Kwa hiyo, mimi naona kwa kweli, Muswada huu bado, una *gaps* nyingi na nitamwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia ni jinsi gani atauboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kuliongelea ni suala zima la bodi kufutwa, mimi sijaelewa ni kwanini bodi imefutwa. Kwa sababu kama hakuna bodi hii taasisi inaripoti wapi? Na ninaamini hata wale wabia, wadau waliokuwa wamehojiwa wametoa maoni yao, hawakusema ile bodi ifutwe, ilikuwa iboreshwe tu ili labda waongezwe watu wengi. Kwa sababu ilikuwa wale watu wanne wote wanahusiana na *state*, lakini hao wawili ndiyo *private companies* na *civil organization*.

Kwa hiyo, tulikuwa tunasema kwa nini wasihusishwe watu wengine, kwa nini Waziri ameondoa ile bodi, na kuondoa kwake kunamaanisha kitu gani? Kwamba hawakuwa makini wakati wanauandaa au waliweka tu kama kiini macho? Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuambiwe hii taasisi itakuwa inaripoti wapi kama bodi haipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani kwa hayo niseme kwamba siungi mkono hoja, mpaka hapo tutakapoambiwa na Waziri kama ataendelea kufanya *amendment* kwa haya au labda itarudishwa, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, sasa nina matatizo ya muda, Mheshimiwa Arfi unaweza kutumia dakika hizi kumi tu? Kwa sababu wengine itabidi waachwe tu.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu ambao upo mbele yetu. Awali ya yote kwa ruhusa yako ninaomba nifanye utangulizi ufuatao kabla sijajikita katika muswada na hususani Ibara ya 4, *part four.* Nakumbuka kwamba nilipata kusikia habari za nzige muda mrefu sana na sikumfahamu nzige kabisa.

. **NAIBU SPIKA:** Tunategemea huyo nzige anahusika na Muswada, kama hahusiki usiendelee.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Anahusika. Nataka kwenda kwenye kifungu cha 4 lakini naomba nianze na utangulizi kwa ruhusa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikimsikia huyu nzige kwa miaka mingi sana na sikumfahamu nzige mpaka baadae nikaja kumjua kwamba anafanana na panzi lakini anafanya uharibifu mkubwa sana.

Huyu nzige liliundwa Shirika la Kimataifa ambalo lipo mpaka sasa hivi linaitwa *International Red Locust Organization.* Kazi yake Shirika hili ni kupambana na nzige, lakini Shirika hili linaendelea kuwepo na nzige wanaendelea kuwepo wameshindwa kuwamaliza nzige. Kwa nini wameshindwa kuwamaliza nzige, ni kwa sababu wanakuja kuwaangamiza nzige wakati tayari wameshataga mayai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati wote wanawasubiri nzige wanapotaka kuanza kuruka ndiyo wanakuja kunyunyizia dawa ya kuangamiza wakati nzige amekwishataga mayai na mwakani tena kuna kuwa na *epidemic* ya nzige. Kwa hiyo, zoezi hili linaendelea kuwepo mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana kwamba ndani ya Bunge hili kuna lugha imezoeleka sana mara nyingi ama Wabunge au Mawaziri wamekuwa wakisema kwamba mafanikio katika yale ambayo wanaelezea yanatokana na sera nzuri ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake na mimi ninachotaka kusema ni kwamba rushwa imeendelea kutunzwa kama hili Shirika la Nzige linavyoendelea kuwatunza nzige na Chama cha Mapinduzi na Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu unapotaka kumtafuta nyoka usiku usimulike mbali anza kumulika kwenye miguu. Kwa bahati mbaya sana Wabunge tumekuwa tukinyoosha vidole vyetu kuwasema watu wengine. Tumesahau yale maandiko yanavyosema “tunaangalia vibanzi kwenye macho ya wenzetu tunasahau boliti ndani ya macho yetu.” Tusidhani sisi Wabunge tupo wasafi kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napitia taarifa ya *Afro-Bolometer* na *REPOA*. Taarifa hii imo ndani ya mtandao kwa maana hiyo ni kwamba watu wote wanaoingia kwenye mtandao huo wanasoma taarifa hii. Si Watanzania peke yao ni dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa hii kuna kura za maoni, wananchi wa Tanzania wanasema kwamba asilimia 38 ya Wabunge ni *corrupt* na asilimia 44 ya Madiwani ni *corrupt*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa hizi tusidhani kwamba sisi ni wasafi sana. Lakini ukija kuutazama muswada huu ambao umewasilishwa mbele yetu hakuna mahala popote unapogusiwa rushwa ndani ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitaunga mkono hoja hii kama kipengele cha rushwa katika siasa hakitawekwa. Moja ya sababu iliyonifanya nitoke ndani ya Chama cha Mapinduzi ni rushwa. (Makofi)

Ndiyo maana nimesema kwamba Chama cha Mapinduzi na Serikali yake wanaendelea kuikumbatia hii rushwa na itaendelea kuwa tatizo. Ni lazima tuanze kujitazama wenyewe kwa kuweka Sheria ambayo itadhibiti rushwa ndani ya uchaguzi. Najua na bahati nzuri Ndugu zangu Wabunge wa CCM wanafahamu mdudu rushwa anavyowasumbua na hususani katika kura za maoni. (*Makofi*)

Sasa hivi wanajaribu kutengeneza *mechanism* ya kuondokana na tatizo hilo. Lakini si kwamba rushwa hizi zinatoka hiki chombo hakioni au hakifahamu. Lakini ilifikia mahala chombo kinachosimamia rushwa TAKURU ilishindwa kufanya kazi na sijui kwa nini? Kwa sababu hili lilikuwa wazi mno. Lakini hakuna hatua zinazochukuliwa kwa sababu tu inagusa chama kinachoongoza Serikali na kwa sababu Taasisi hiyo ni sehemu ya Idara ya Serikali inashindwa kushughulikia matatizo hususani yanayowagusa viongozi tukiwemo pamoja na sisi Wabunge.

Kwa hiyo, ninashauri ni lazima kiongezwe kifungu katika *part four* ya Muswada huu itakayogusa suala la rushwa katika uchaguzi. Tusilifumbie macho, kama kweli tunataka kupambana na rushwa katika nchi hii lakini vinginevyo tutakuwa tunawatizama madaktari, majaji, polisi na mabwana afya na kadhalika, sisi tunajisahau.

Tuanze kwanza kwa Wabunge, ni namna gani Wabunge wanaingia ndani ya Bunge kwa ajili ya kuja kutunga sheria na kuisimamia Serikali. Mbunge anayetoa rushwa kuingia Bunge hawezi kuisimamia Serikali kuzuia rushwa, tunajidanganya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufike mahali sasa tujitizame kwamba tunatanguliza maslahi na mustakabali wa Taifa letu kwanza na sio vinginevyo. Suala la rushwa lina hadithi ndefu na wala sina sababu ya kurudiarudia, lakini jitihada zote hizi na sheria nyingi zilizotungwa na Tume kadha wa kadha zilizoundwa na zilizoanzishwa kwa mujibu wa sheria za Bunge, zimeshindwa kuleta tija inayotakiwa ya kuweza kuondokana na tatizo la rushwa. Rushwa katika nchi hii imeanza kuzungumziwa toka mwaka 1966 mara tu baada ya kupata uhuru, mwaka 1971 ikatungwa sheria ya kuzuia rushwa, mwaka

1975 ikaanzishwa *Anticorruption Squad*, mwaka 2001, Tume ya Kudumu ikabadilishwa na kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na baadaye *Anticorruption Squad* ikabadilishwa na Taasisi ya Kuzuia Rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni jitihada zinafanywa za kubadilisha kanzu, lakini Shekhe ni yule yule. Tunabadilisha majina tu lakini hatuna utashi wa kweli wa kupambana na rushwa. Rushwa sasa hivi ni zaidi ya miaka 40 tunaipigia kelele toka mwaka 1966, *forty years,* lakini ukija kuangalia taarifa za Taasisi ya Kuzuia Rushwa, kwa bahati mbaya sina kumbukumbu sahihi, lakini kwa kadri tunavyosoma taarifa za mikoa mbalimbali kuhusu Taasisi ya Kuzuia Rushwa wanapokea taarifa nyingi sana, wanazifanyia kazi taarifa chache sana, wanazopeleka mahakamani ni kidogo sana. Hii ni kutokana na kwamba labda hawana watumishi wa kutosha au kuna rushwa ndani ya taasisi yenyewe ya zuia rushwa, au yapo matatizo mengine ya kiufundi ambayo yanataka yatazamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitaunga mkono hoja hii kama kipengele cha rushwa katika siasa kitaingizwa hasa katika *section* ya 42. Kikiongezwa kipengele cha rushwa nitakuwa tayari kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niuongelee Muswada huu ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamesema mengi sana na wamesema mambo ambayo yapo. Hili suala la rushwa kama walivyosema wenzangu, rushwa ni adui kweli, ni adui mkubwa sana na ninavyoona mimi rushwa inakua kila baada ya awamu. Awamu ya kwanza ilikuwa na rushwa, awamu ya pili ikaongezeka. Kwa hiyo, inaongezeka kila wakati. Lakini sheria zimewekwa katika awamu zote na ndio hizi tunazidi kuziweka mpaka sasa, lakini hawa wala rushwa ni watu na ni wenzetu na nadhani ni mtu aliyeko madarakani ndio anaweza akala rushwa. Mwananchi wa kawaida hana rushwa yoyote ya kula, bali yeye ndio anatoa rushwa na kwa hiyo, anaiuza haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba, hili suala la rushwa hatukuangalia kwa mapana zaidi kwamba imeleta umaskini kwa wananchi kwa kiasi gani. Mimi sipendi kuingia kwenye mambo ya siasa kama mwenzangu alivyosema kwa sababu hiyo asilimia 36 kuna Wabunge walioingia humu Bungeni kwa ajili ya rushwa. Sidhani asilimia 36 ni Wabunge wa CCM, ni pamoja na wao waliofanya tathmini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika kwamba wanapotoa rushwa hata wana-CCM mnawapa rushwa. Kwa hiyo, wana-CCM wanaweza kuwa mashahidi wenu kwamba na nyie mmetoa rushwa kwa sababu hamuwezi mkajua kwamba huyu ni mwana-CCM au ni nani. Kwa hiyo, ningependa kutofautiana kuachana na jambo hilo la asilimia, lakini napenda kusema kwamba haki ya wananchi imepokonywa na rushwa.

Nikitoa mfano ni kwamba, katika halmashauri zetu, mimi sijawahi kuona fedha za barabara zilizofanya kazi kikamilifu. Kwanza siyo barabara zinajengwa kule bali ni mitaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanaharibu zaidi barabara kuliko ilivyo. Hivi ukitengeneza barabara, usipotoa matoleo ya maji itakuwa ni nini? Itakuwa ni mitaro pande zote! Lakini hakuna mtu anayekuja kukagua na Madiwani wakilalamika, mla rushwa yoyote katika halmashauri anapandishwa cheo, au anahamishwa au anasimamishwa kwa muda na baadaye anarudi kazini. Kwa hiyo, nasema kwamba wanaowafuga walarushwa ni Serikali! Katika uongozi huu, umejaa ushemeji, undugu, urafiki, mwenzangu, mwenzetu! Hiyo ndio inafuga rushwa *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba, hakuna kitu ambacho mimi ninachukia kama rushwa. Kama haki ya wananchi wakikosa waporwe haki zao, mimi nisingekuwa na msamaha kabisa hata kama ni ndugu yangu amekula rushwa, siwezi kabisa kuvumilia. Kwa hiyo, wananchi wanapopata matatizo kwa ajili ya mtu mmoja kuneemeka, inanipa shida sana. Mimi namshukuru sana *Auditor General* alipoleta mahesabu haya katika ukaguzi wa mahesabu. Nimeyapitia yale makabrasha kwa kweli nikamwombea Mungu, amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hivi, haya mahesabu katika Wizara, upotevu wa hela katika Wizara na Halmashauri zetu, hivi hakuna kiongozi mwingine ambaye angegundua kabla? Waziri yupo kila siku katika Wizara yake, anasubiri kuletewa mabilioni ya fedha zilizopotea katika Wizara yake, hajawahi kuona wala hajawahi kusikia. Kwa upande wangu inanipa shida sana! Wala siyo hiyo tu, mnapata malalamiko ya walarushwa katika Wizara zenu mnakaa kimya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kusema kwamba kwa kweli tutapitisha sheria mlizoleta, lakini naogopa kusema kwamba hata hii Taasisi ya Kuzuia Rushwa inaweza ikafanya kazi, lakini wanaweza wakasimamishwa.

Mimi bado nina imani na hiyo taasisi kwamba inaweza ikafanya kazi vizuri na kama mlivyosema kwenye sheria hii kwamba wasiingiliwe, ningependekeza zaidi kungekuwa na mahakama yao kwa sababu wakipeleka katika mahakama hizi, yeye si anafanya upelelezi anapeleka mahakamani, inawezekana pale mahakamani ikawa *delay* miaka 30 au baadaye ikawa *delay* miaka miwili mtu anarudishwa kazini, analipwa na haki zake. Sasa umefanya nini? Na akija atawakomoa wale atakaowakuta kwamba mmefanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili suala la hii taasisi iwe ni taasisi inayojitegemea kabisa na ipewe mamlaka, isiwe ni kutafuta upelelezi tu, iwe na upelelezi na isiingiliwe na mtu yeyote na ninaomba iwe chini ya Ofisi ya Rais, isiwe chini ya Wizara nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia rushwa katika nchi hii kama wenzangu walivyosema, ni vigumu sana kupata ushahidi na haiwezekani ikapatikana ushahidi kwa

sababu wote hatuchukui rushwa, kwa sababu Mkurugenzi angethibitisha rushwa katika Halmashauri yake ingepatikana kwa urahisi sana kwa sababu yeye ndio Mkuu anayesimamia Halmashauri hiyo. Lakini Mkurugenzi ndio wa kwanza kukataa kwamba mtumishi katika Halmashauri hajala rushwa, yeye ndio mtetezi wa kwanza! Sasa nani mwingine atathubutu tena kwenda kutoa ushahidi? Kwa hiyo, ni vigumu sana wao kupata ushahidi, kwani wanakuwa ni kitu kimoja.

Mkiangalia majengo katika maeneo yetu, ni wananchi ndio wanakagua majengo wenyewe na wahandisi wapo, hii asilimia 10 ipo, kila Mbunge anafahamu hapa kwamba kuna asilimia 10 inayotembea katika mikataba yote inayowekewa katika Halmashauri. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba nakubaliana kabisa na sheria zilizoletwa na ninaomba tuzipitishe, lakini isiwe tunapitisha sheria ambazo hazifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe, naomba kwanza nitoa pole kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo na ningeomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Aidha, ninapenda kumpongeza ndugu yangu Mtutura A. Mtutura kwa kuchaguliwa na kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa najaribu kujiandaa kuchangia Muswada huu, nilidhani kwanza nijiridhishe kwa tafsiri ya nini maana ya rushwa. Katika kujaribu kutafuta nini maana ya rushwa, nilikwenda nikafika mahali ambapo sipati mwisho wake. Lakini ninaweza kusema maneno machache ili yaweze kusaidia kama yanaweza yakasaidia katika kuboresha Muswada huu. Binafsi ninaiona rushwa kama inatokana na msukumo wa utamaduni, tabia, hulka au desturi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu rushwa ni kama roho na mla rushwa hata kama angekula vipi, hawezi kuridhika kwamba sasa ametosheka na sasa amefika mwisho wake. Lakini tujiulize, tunaposema tunatunga sheria kwa ajili ya kupambana na rushwa tunamtungia nani? Nadhani tunajitungia sisi wote kama Watanzania ambao tunawajibika kwa nchi yetu baada ya kuona kwamba mambo hayaendi sawasawa na hasa sisi viongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize wenyewe, hapa utasikia mtu anasema wewe unafanya kazi sehemu mbaya, lakini fulani anafanya kazi kwenye sehemu nzuri yenye marupuru, hakuna marupurupu mengine zaidi ya rushwa! Kwa hiyo, rushwa ipo ndani yetu na ni vyema wote tukadhamiria kwa dhati kabisa kama ambavyo Rais wetu ameonesha dhamira ya dhati kupambana na rushwa ili tuweze kumsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, rushwa kwa haraka inaombwa kwa njia mbili. Kuna njia ya moja kwa moja na mimi nimependa niite *direct way* ya kuomba rushwa, lakini ipo nyingine *constructive,* yaani ile ya moja kwa moja ya *direct way* mtu anakwambia nipe kiasi fulani nikusaidie kukupa huduma fulani. Lakini hii *constructive* ni kwamba ni *indirect,* hakuombi, lakini ama anachelewesha kukupa huduma unayostahili, ama

anazembea kukupa huduma unayostahili, ama anategea kutoa huduma unayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ingekuwa vyema ikawekwa katika eneo ambalo kama ikitokea, basi mtu huyo anashawishi mtu atoe rushwa na hivyo iwe ni kosa. Kwa hiyo, katika orodha ya makosa yaliyotajwa kutoka *section* 15, mimi ningependekeza kwamba kama mtu anahitaji *file* kwa ajili ya kesi yake, kitendo cha kumzungusha siku ya kwanza na siku ya pili ionekane kwamba unashawishi akupe rushwa kama hakuna sababu za msingi. Kama mtu anahitaji *file* kwa ajili ya kudai mafao yake kwa ajili ya kudai kiinua mgongo chache akatoka huko mkoani akaenda Dar es Salaam akakaa pale siku tatu, wiki, mwezi hata hilo *file* hajalipata na wala hajashughulikiwa, basi Ofisi hiyo inatumia njia hiyo kwa ajili ya kutaka kupata rushwa, ielezwe katika sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini labda sasa nijielekeze katika kazi ya kutunga sheria ambayo ndio kazi kuu ambayo ilisababishwa nikachaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kibakwe. Kazi ya kutunga sheria ni kazi moja na ndio tunayoifanya hapa, lakini sisi kama Wabunge, hatuishii na kazi hiyo tu ya kutunga sheria. Nikirejea katika Ibara ya 63 ya Katiba inaeleza kwamba Bunge linazo kazi kadhaa na inasema kabisa kwamba Bunge ndicho chombo kikuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kwa niaba ya Wananchi kimepewa wajibu wa kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapouangalia huu muswada, ninaona tuna ile *role* tu ya kuishauri Serikali, sijaona *provision* inayotoa *role* ya kuisimamia Serikali. Kwa mfano, Wizara fulani inakula rushwa, mimi Mbunge ninajua au Bunge linajua, lina-*provision* gani katika ku-*execute* ile *oversight function* ya kuisimamia Bunge katika muswada huu?

Ninadhani sisi kama Bunge ni vizuri tukawa na *provision* na nafasi inayotufanya na sisi tuweze kuilazimisha Serikali au kuweza kuielekeza katika kuteleza wajibu wetu wa kuisimamia Serikali katika muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi nilipata bahati ya kwenda Uingereza. Tulipofika kule, tukashiriki katika semina mbalimbali. Miongoni mwa jambo la msingi sana ambalo nilijifunza kule ni namna ambavyo Bunge linapewa mamlaka ya kutosha ya kuisimamia Serikali.

Kwa mfano *Controller and Auditor General* wa Uingereza ni *Officer* wa Bunge. *Is an Officer of the Parliament* na nikashuhudia *proceeding* moja, walikuwa wanaita wao *Doctor Sources Intelligence* ambapo Bunge lilimwagiza Mkaguzi akague kuhusu hiyo *scandal*. Lakini sina hakika kama hapa sisi Bunge tunasikia *Richmond,* tunasikiasikia tu, ni lini na ni wakati gani? Au tunasubiri nini? Kwa sababu hata wao kwa mfano Uingereza Bunge liliagiza Mkaguzi Mkuu aende awaletee taarifa baada ya kuona *there is an out play of public* kwamba wananchi wanapiga kelele, sasa na sisi kwa kusikia wananchi wanapiga kelele hivi, hatuwezi kuwa *provision* ya kusema kwamba sasa tunataka mahali fulani pachunguzwe kwa sababu pana rushwa. Pangepatikana *provision* ya namna hiyo, mimi ningeupenda sana huu muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda sasa nijielekeze tena katika eneo lingine ambalo nimeona pia niweke mambo sawasawa, katika *section* 2 (1) tumesema sheria hii itatumika katika Tanzania *mainland*, kwa sababu *amendment* zimekuja mara nyingi, sina hakika kama kwenye *schedule of amendment* kama imeondolewa, lakini inasema sheria hii itatumika katika Tanzania Bara. Lakini ukienda kwenye *section* 42 (2) na 43 na nyinginezo inasema mali itakayotaifishwa itakuwa ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria hii inatumika Tanzania Bara. Mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikitaifishwa, hapa ninahisi kuna *contradiction*. Ningeshauri sheria hii itumike Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ni kwamba nilipokuwa najaribu kuangalia madhumuni ya muswada huu ambao utafuta sheria ya mwaka 1971 ya TAKURU, unakuja siyo tu kwa sababu wameamua tu kuuleta, umekuja ukiwa una *spirit* yake na *spirit* yake ni kufanya hii Tume iwe *independent* na tumesema katika *independence* hiyo iweze ku-*investigate* na iweze ku-*prosecute*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sheria yenyewe inasema Mkurugenzi ata-*investigate,* lakini atakapokuwa anataka ku-*prosecute* ni lazima afuate maelekezo ya *DPP*. Hapa ninapata tatizo la *independence*. Kama unamtaka mtu awe *independent* halafu unasema atafuata *direction* za mwingine ninapata tatizo kidogo la huo ukubwa wa *independence.* Ninafahamu kwamba Mkurugenzi wa mashtaka Katiba inamtaja kwamba ndiye mwenye mamlaka katika *section* 59 (b) (2), anasema Mkurugenzi wa mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini, ninafahamu. Lakini kwa sababu ya madhumuni ya muswada huu kwamba tunataka chombo hiki kiwe *independent,* basi ningedhani *DPP* awekewe mipaka fulani katika kushughulikia kesi hizi za rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutambue kwamba *DPP* huyu ana mamlaka, ana *discretion* ya ku-*enter nolle prosequi* kumfutia mtu akasema hana kesi ya kujibu, sasa ndio umepeleka kesi kwake unataka kibali chake, *direction* yake anasema mimi nina-*enter nolle prosequi,* huyu Mkurugenzi tumemuweka kwenye majaribu. Tunazungumza *power in dependence,* sasa tuseme kabisa katika hii sheria kwamba Mkurugenzi atakuwa hana mamlaka ya ku-*enter nolle prosequi,* tuseme wazi.

Lakini pia tumesema kwamba *direction* yake mimi nadhani hili neno katika hii *section 7* unaposema *the subject to the direction of the DPP prosecute offences under this act,* mimi nadhani tusiseme *subject to the direction*, ingenoga zaidi tungesema, *"with his or her concert",* tuseme kwa *concert* yake na hiyo *concert* nayo tuiwekee *boundary* tuseme hiyo *concert* yake itakuwa tu kwa muda na kama haja-*react* katika kutoa *concert,* basi iwe *implied* kwamba ametoa *concert* ili Mkurugenzi aendelee na *prosecute*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa nichangie pia ni kwenye adhabu. Kwenye adhabu tumesema sehemu nyingi tu kwamba iwe ni Shilingi milioni saba, isizidi miaka mitano, tuweke ile ya chini. Tukiacha *discretion* kubwa hapa katika adhabu tunawaingiza majaribuni Majaji na Mahakimu. Kwa nini tusiseme tu kwamba aanzie kutoa faini kama ni kuanzia milioni moja na isizidi milioni saba na

tusiseme adhabu ya kifungo iwe kuanzia mwaka mmoja, kwa sababu huku chini hakuna, mpaka sasa litatokea kosa ambalo limeingiza nchi katika hasara kubwa halafu Hakimu anasema mimi ninamwadhibu huyu mwezi mmoja, tutasemaje? Kwa hiyo, tungeweka hapa ikakaa hivyo, ingekuwa ni nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imezungumza juu ya kwamba hii Tume ina uwezo wa kuingia hata kwenye sekta binafsi, lakini mimi nadhani ingeonyesha *express* kwamba anaingiaje? Amesema ataingia tu katika kushauri na kutoa elimu, lakini haijasema kunapokuwa kuna harufu au tatizo la rushwa Mkurugenzi awe na mamlaka ya kuingia na kuchunguza kwa mfano kampuni fulani, basi Mkurugenzi aambiwe kwamba ana uwezo wa kuingia mpaka kule ndani na akachunguza na akaweza kujua kinachotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja baada ya marekebisho hayo kufanyika. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige na msemaji wa mwisho ni Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu.

Kwanza kabisa, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala, naomba kumfikishia salamu za pongezi Mheshimiwa Mtutura kwa ushindi mkubwa alioupata na pia kwa niaba ya wananchi walewale nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya Dr. Aaron Chiduo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Muswada wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa katika maeneo yote mawili. Kwanza nitazungumzia japo kwa haraka kidogo ni namna gani tutaweza kupambana na rushwa kwa mafanikio halafu pia nitazungumza ni kwa namna gani tunaweza kuzuia rushwa kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumza kuhusu dhamira na mimi naamini dhamira, *resolve determination* ndiyo dawa ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu sioni kama kweli tunahitaji sheria kila wakati. Kuna sheria ambazo tunazo kule nyuma ambazo zinaweza kuyafanya mengi ya haya tuliyonayo, lakini hata baadhi ya vipengele ambavyo vipo kwenye sheria hii au kwenye hii *Bill* ambavyo inapendekezwa, vimekuwa *covered* kwenye sheria nyingine ambazo zimetangulia. Kwa mfano, Sheria Na. 9 ya mwaka 1983 inayozungumzia suala la Uhujumu Uchumi, inaeleza kabisa kwamba *embezzlement* ni suala la uhujumu na kwa maana hiyo, kuna vipengele ambavyo vinaweza vikatumika na kwenye *Bill* hii, tumeweka kama *Section 30* kwa ajili ya kuzungumzia kitu kilekile.

Kwa hiyo *embezzlement* imekuwepo na Sheria ya Uhujumu imekuwepo haijatekelezwa. Kwa hiyo, hata hii *Bill* tutaipitisha lakini pia kama ilivyokuwa Sheria ya

Uhujumu Uchumi, matatizo yatabaki palepale. Hata ukiangalia pia, kwa mfano Sheria ya Maadili ya Viongozi kuhusu mali, uangalie utekelezaji wake, nao una matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kifupi, ninaomba Serikali ielewe kwamba kinachokosekana katika kupambana na rushwa ni dhamira ya dhati kabisa. Ninasema hivyo kwa sababu nyingine kubwa mbili kwamba rushwa siyo rahisi kuithibitisha na kwa sababu siyo rahisi kupata ushahidi na inakuwa ni ngumu kwa sababu wote wawili, yaani mtoaji na mpokeaji wa rushwa wanakuwa hatiani kwa mujibu wa *Bill* tuliyojadili, ukiangalia *section 17* inasema kwamba yule mtoaji wa rushwa ana hatia na *Section 18* inasema yule anayepokea ana hatia.

Katika mazingira hayo, hatutapata ushahidi kwa sababu hawa wawili watakubaliana na watapeana kwa siri na hakuna mwingine atakayekwenda kutoa ushahidi dhidi ya mwingine na mazingira kama hayo ndiyo hatari sana hasa kwenye rushwa kubwakubwa ambazo zinaumiza zaidi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kifanyike? Nilikuwa nafikiri na kuiomba Serikali sana tufanye mambo mawili. Kwanza, tutumie ushahidi wa mazingira kuchukua hatua, lakini pia tusikilize wananchi kupitia kwa Wabunge wao na pia kupitia kwenye Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maamuzi mengine hayahitaji ushahidi, kwa sababu mazingira yanaonesha kwamba kuna tatizo. Ninafikiri bado kuna hatua zinaweza kuchukuliwa bila hata kuhitaji ushahidi. Ninasema hivyo kwa bahati nzuri kwamba, sehemu kubwa ya walarushwa hasa zile rushwa kubwakubwa ni Viongozi Waandamizi wa Serikali na wengi kasoro wachache sana kwa kweli ni wa kupata kazi ile siku moja na kuikosa kesho yake. Sasa huhitaji kwenda Mahakamani.

Kwa mfano, wananchi wanapiga kelele kwamba kuna matatizo Idara ya Wanyamapori katika mazingira kama hivi, tujiulize kwamba hivi kweli hakuna Watanzania wengine wanaoweza kufanya kazi kama hiyo ambayo kwenye Idara hiyo inalalamikiwa? Hivi kufanya mabadiliko katika Idara hiyo inahitaji sheria hii ya *PCB*? Ni mtu mmoja tu mwenye kuweza kuamua kwamba *okay*! Tunafanya *appointment* ya mtu mwingine na hivyo inakwenda mpaka kwenye maeneo mengi tu, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Wakurugenzi wa Mashirika mbalimbali kama *NSSF, PSRC* wote hao ni wa kuteuliwa. Sasa kwa kuwa tunakosa ushahidi wa kuwapeleka Mahakamani, mazingira yanatosha kuwabadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Marehemu Baba wa Taifa aliwahi kusema kule nyuma kwamba yeye alipata shida sana kwa sababu kulikuwa na wasomi wachache na kwa maana hiyo alikuwa ana- *struggle* kuangalia watu, kwa hiyo ndiyo maana alikuwa analazimika kwa nyakati nyingine kuhamisha kutoka hapa kwenda huko. Sasa hivi wasomi wako tele na hao tulioko hapa Bungeni naamini ni wachache kuliko walioko huko nje. Kwa hiyo, naamini kwamba hakuna tena ugumu wa kuwapata Watanzania wenye kuweza kufanya kazi mbalimbali hasa zinazohusu uteuzi kuweza kusimamia maeneo mbalimbali ambayo yana matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzungumza sana rushwa kwenye mikataba kwa mfano, mimi nafikiri ni kui-*promote* kwa sababu kwa mtu ambaye ni mgeni na anasikia kulikuwa na matatizo kwenye mkataba wa *IPTL*, *ATC* na Mkataba wa Madini, halafu hakuna chochote kilichotokea. Kwanza anapata hisia kwamba kwenye Mikataba kuna rushwa na hakuna sheria au hatua zinazochukuliwa dhidi ya hawa ambao wanatuhumiwa. Bahati nzuri kila wakati tukio linatokea katika muda *specific* ambapo kuna mtu ambaye anakuwa *responsible.* Sasa ukimwona mwenzio aliyeshiriki kwenye Mkataba wa *IPTL* leo anapeta tu na wewe leo ndiye umeteuliwa kuwa kwenye eneo hilo, *the best thing you can do is to look the best way this guy manage to survive and you do the same* na hiyo inatokea.

Sasa nilifikiri tuta-*corrupt* hata wasio-*corrupt*. Sisi tunasema kwamba ukitaka nyuki wahame kwenye eneo fulani, basi usipoteze muda na hao wengine. Ukimgonga yule Malkia basi. Mimi naamini ukichukua hatua kwa Afisa wawili au watatu, basi naamini kabisa kwamba huku wengine watafuata. Sasa hivi hata wengine wanaambukuzwa *embezzlement* zinazotokea, sijui Hati Chafu kwenye Wizara mbalimbali, Halmashauri na kadhalika.

Kwetu sisi Wahasibu, unaona wenzako ambao wako kwenye Idara ya kuwa na *interface* na wateja wanasemekana wako kwenye Idara nzuri walioko *front office* ndiyo wanaweza ku-*negotiate* mambo ya *contracts, now what you do* wewe kama Mhasibu sasa, mtu wa *back office* na unaona wenzio wote ni Wakurugenzi wa Fedha, mnakutana kwenye *Management Meeting,* lakini mwenzio kila siku amebadilisha saa, leo amevaa labda ya laki mbili na wote ni Wakurugenzi na mshahara na ngazi ziko sawa?

Sasa unachoweza kukifanya na wewe unacheza na vitabu *and books always balance and that happens,* kwa hiyo, Mhasibu na yeye anacheza na vitabu, lakini chanzo kimetokana na yule ambaye amekula kule kwenye mkataba, basi na mimi nakula kwa ku-*balance* vitabu vyangu. Hatutafika mwisho! Tuchukue hatua inapostahili, tusikwepe jukumu kwa kutafuta vipengele tumpe sasa *PCB* afanye nini na nini. Lakini *PCB* hateui na wanaokula rushwa wengi ni wale ambao wana nafasi za kuteuliwa, anaamua na kusaini mikataba kwa niaba ya nchi. Kwa mazingira hayo, *we can take actions* kuhusu watu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kupendekeza kwamba tuwe na uwezo wa kuchukua hatua na ninaamini kwamba hayo matatizo yatapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa ni kwamba tujaribu kuwasilikiliza wananchi. Suala la kupuuza wananchi mimi linaniumiza sana. Vyombo vya Habari vinaandika na kuandika, hivi kweli Serikali haijui kwamba wananchi hawakuridhika na uuzaji wa nyumba za Serikali? Hivi utaendelea kuwabishia wananchi hawa milioni 36, ninyi Baraza la Mawaziri watu 60 mnasema kwamba *36 million Tanzanians* wanawa-*complain* kuhusu jambo hili kweli hawana *point*? Tusikilize wananchi.

Nasema kuna matatizo kwenye Idara ya Wanyamapori, kwenye uuzaji wa nyumba za Serikali, Mikataba ya Madini na kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 1983 Kifungu cha (2) (a) na (g) kinasema kabisa kwamba suala la Madini na suala la umeme ni mambo yanaitwa *Necessary Services* na mtu akiingia mkataba wenye kuiuza nchi katika maeneo hayo ni Mhujumu Uchumi. Enzi zile za mwaka 1982 na 1983 nafikiri mambo yangekuwa tofauti. Kwa hiyo, nafikiri tupate tu hiyo *commitment* na *determination,* naamini mambo yatabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilifikiri lingefaa zaidi tutafute namna ya kupunguza ugumu wa upatikanaji wa ushahidi Mahakamani kudhibitisha tuhuma za rushwa na nilifikiri kwamba tumbane zaidi yule anayepokea kwa sababu katika maeneo yaliyo mengi mpokea rushwa ndiye anakuwa amemshawishi yule mwingine na kuna rushwa nyingine ambazo ni za lazima. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba mtuhumiwa awe ni yule anayepokea rushwa, yaani tuseme kwamba mwenye hatia ni yule anayepokea *at least temporarily* tumwache huyu anayetoa ili aweze kuthibitisha kwamba kweli nilimpa. Bila hivyo, kama wote wawili wana hatia, mimi nitakwenda kutoa ushahidi gani? Mimi niseme kwamba nilitoa! Huyu naye aseme kwamba alipokea! Sasa tuko ndani ,basi apatikane mmoja wa kusaidia kuthibitisha kwamba kweli mwenzake ana hatia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri tujaribu kurekebisha vipengele vya Sheria mbalimbali ambavyo vinatoa *loophole* hasa vinavyotoa nafasi ya maamuzi kwa mtu mmoja. Kwa mfano, ziko Sheria nyingi na hili litasaidia sana katika kuzuia rushwa. Ukiangalia Sheria Na. 24 ya mwaka 1997 Sheria ya *VAT* kifungu Na. 12 kinasema kwamba: "Waziri ana mamlaka ya ku- *amend the schedule* ambayo inahusu *exemptions* kwenye *VAT*." Katika mazingira kama haya, Waziri, yaani *The Minister, a person can amend the schedule* na kwa maana hiyo, katika mazingira ambayo anaona inafaa anaweza akapitisha uamuzi kama huo. Nilifikiri maamuzi kama hayo yanayomlenga mtu mmoja kufanya uamuzi, ni vizuri yakaangaliwa.

Sheria Na. 30 ya mwaka 1973 kifungu 112 kinachohusu *Road Traffic Act* kinasema kwamba: "*The Minister may exempt a person or persons from the provisions of this Act.*" Kwa maana hiyo, mtu anaweza akawa na hatia ya kukiuka Sheria ya Usalama Barabarani halafu Waziri kwa *discretion* yake akasema kwamba anamu- *exempt* mtu yule kutoka kwenye *provisions* za *Act* hiyo.

Sheria Na. 5 ya mwaka 1998 kifungu 10 cha Sheria ya Madini kinasema kwamba: "Waziri ana Mamlaka ya kusaini *Mining Development Agreements.*" Hii ni mikataba mizito na anaisaini peke yake. Katika mazingira kama hayo, kuna kifungu Na. 4 kifungu kidogo katika hiyo *section 10* kinasema kwamba kuna Kamati ya Ushauri ambayo Waziri anakuwa anashauriwa nayo, lakini halazimiki kuchukua ushauri huo, yaani ushauri unaotoka kwenye Kamati ile. *Clauses* zinawekwa kwa jinsi anavyo-*negotiate* yeye na yule Mwekezaji na hapo akishaweka *clause* kwamba *okay,* hakuna kipengele kinachohusu dola 200,000 kwenye Halmashauri inayozunguka mgodi, *that's it* na mkataba unakuwa umesainiwa na *we are done*. Sasa nilifikiri vitu kama hivi ni vizuri tukatoa mamlaka kwenye Kamati na siyo kwa mtu.

*Act* Na. 11 ya mwaka 2004 - *Income Tax Act Section No. 10* inasema: "Pia Waziri anaweza aka- *exempt income of a particular person from tax*" na pia inasema "*The Minister may amend the second schedule"* ambayo ni *schedule* inayohusu *exemption* mbalimbali. Kwa mazingira hayo na kwa mamlaka hayo aliyonayo Waziri, ninaamini kwamba ni matatizo.

Kwa hiyo, ili kupunguza, basi tupunguze Sheria hizi ambazo zinam- *point* mtu kufanya maamuzi kwa niaba ya nchi, mtu mmoja anakaa mezani London, anasaini mkataba kwa ajili ya milioni 36 za Watanzania. Mimi naamini kwamba *that is not fare* pamoja na kuwepo Kamati inayomshauri, lakini bado ninaamini kwamba kwa sababu *decision* ile na *negotiation* na *clauses* zitakazokuwepo kwenye *MDA* yeye ndiye ana-*negotiate.* Nafikiri hiki kipengele *is too harsh and this is not fare*. Sasa anapo-*negotiate* mtu mmoja nafikiri itakuwa na matatizo makubwa.

*Otherwise* nilikuwa nashauri, kwa ujumla turejee *report* ya Jaji Joseph Warioba, imeainisha Vyanzo vya Rushwa na ninaamini katika kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza sana. Lakini pia angalau tuboreshe pia mishahara ya wafanyakazi ili wale wachache ambao kwa sababu ya mazingira magumu ya kazi wanalazimika kuombwa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haina madhara kuunga au kutokuunga mkono. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Mheshimiwa Vita Kawawa ndiye msemaji wa mwisho katika hoja hii.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Kupambana na Kuzuia Rushwa. Rushwa ndiyo kikwazo kikubwa kwa kukuza uchumi wa nchi yetu, rushwa pia inadidimiza maskini na inaweka juu maisha ya watu maskini wengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia katika Muswada wa Kupambana na Fedha Haramu, nilitamka kuwa Sheria ya Rushwa ilikuwa bado ina mapungufu, lakini leo naishukuru Serikali imetuletea Muswada huu, tuupitishe na ninauunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *improvement* ya *Anti-corruption Policies* na *Program* zake *at National Level* zinatakiwa uelewa wa undani kabisa hasa katika kuangalia uelewa wa *Country Governance and Operating Environment*. Katika nchi nyingi ambazo zili-*establish Anti-corruption Agencies* hawakufanya *study* wala *analysis* ya *Country Governance and Operating Environment,* matokeo yake yalijionesha kuwa wali-*fail,* yaani walipata *ineffectiveness* katika *Anti-corruption efforts*. Hivyo mimi naamini kabisa *concern* ya Wabunge na wananchi isije ikatutokea hapa nchini kwetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, *analysis* hii inatakiwa ku-*examine various aspects* za *Political, Economical, Social and Historical Experience.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *Social and Political analysis* ni muhimu sana katika hili na ina nguvu kubwa katika matokeo mazuri ya hatua za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya urasimu wa baadhi ya Idara za Kiutendaji za Serikali, urasimu wake mwingine unatengeneza mazingira ya rushwa mpaka inafikia wakati makampuni na baadhi ya wananchi kuona kuwa gharama za rushwa ni moja ya gharama za biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tafiti zinaonesha katika nchi za Asia kuwa kuna makampuni ambayo yamekuwa yakitoa rushwa yamekuta yanatoa fedha nyingi na matokeo yake *they become inefficient* katika utekelezaji wake. *In reality,* hizi kampuni zina-*spend significant amount* katika ku-*negotiate* na urasimu na kuwa na mzigo mkubwa wa *capital* za uendeshaji wa shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Muswada huu ukishapitishwa, basi wananchi waelimishwe vya kutosha, kuwe na lengo la kumpa mwananchi uelewa hasa wa kutetea haki zake vizuri kuliko kuzinunua. Kama haki hizo watazijua watatumia njia ya kikatiba na ya kisheria katika kutetea haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vilevile na kuungana na wenzangu kuwa, kungekuwapo na *Parliamentary Oversight Board* ambayo ita-*develop system* ya *transparency* itakayosaidia kuzuia *abuses* mbalimbali za *favouritism* katika biashara na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa TAKUKURU ningeshauri wa-*strengthen by and multilateral cooperation* katika uchunguzi na mambo mengine ya *Legal proceeding* kwa ku-*develop system* ambayo itaendana na Muswada huu na kukazia *effectiveness* ya *Exchange of Information, Evidence* na *International Laws Enforcement Agencies* ambapo mahusiano yake yataleta utafutaji na upatikanaji wa *for fightable assets* pamoja na kuzi-*sees* na kuzirudisha nyumbani.

Lakini katika hili, kwenye Muswada huu Ibara ya 47 sura ya 6 ukurasa wa 33 haikuonyesha mahusiano ya *International Law Enforcement*, umeonyesha mahusiano na *Enforcement Agencies* zilizopo *within United Republic of Tanzania*. Sasa hili nilikuwa naomba na kushauri wataalam wakaliangalie na kulifafanua vizuri.

Vilevile ili kwenda sambamba na Muswada huu, nashauri na kuungana na wenzangu kwamba tufanye *review* ya sheria nyingine kama *Public Procurement Act* na *Mining Development Act* ya mwaka 1998 kwa kuangalia zile *excessive powers* ambazo wanazo *final authorities* ili tuweze kwenda sambamba na utekelezaji na uzuiaji wa rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata *Philosopher* Plato alisema, naomba nimnukuu: "*Party can never be well unless the hole is well*".

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, huu Muswada wachangiaji siyo kwamba wote walioomba wamepata nafasi, lakini wengi walioomba wamepata nafasi. Kwa hiyo, huyu ndiye atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

Mchana tukirudi tutampa nafasi, Waziri wa Katiba na Sheria kwanza dakika zake za kuchangia kama kawaida kwa sababu yeye siyo mtoa hoja, halafu ataitwa mtoa hoja, ndio tutaingia kwenye Kamati ya Bunge Zima baada ya mtoa hoja kujibu hoja.

Sasa basi, mbele yetu hapa kuna mapendekezo ya *Amendment* ya Muswada huu ya kutokana na Wabunge. Yapo mapendekezo mezani. Tunavyoona mezani, yaliyoletwa kwa utaratibu unaohusika siyo kwamba wameletwa mengi, kuna utaratibu wa kutoa taarifa siku mbili. Kwa hiyo, taratibu zote zimefuatwa.

Kwa hiyo, tunazo *amendments* tatu. Sasa *amendments* hizi tatu katika Bunge Zima tutakapofika katika kifungu husika, mwenye *amendment* atasimama na atapewa nafasi ya kwanza kueleza ni kitu anataka kufanyia *amendment* katika kifungu kile tutakachokuwa tunakizungumza.

Tutaruhusu majadiliano kutoka kwa Wabunge kwa sababu huyu atakuwa ametoa hoja ya kufanya mabadiliko. Tutajadiliana na Serikali, watajibu yale majadiliano yanayoendelea, tukifikia hapo, kama yule aliyetoa hoja ya *amendment* hakubaliani na maelezo, pale tutatakiwa kupiga kura.

Ikitokea kwa sababu yoyote ile *amendment* ya Mheshimiwa Mbunge imeshinda, kile kifungu kitakuwa kimechukua sura aliyoleta Mheshimiwa Mbunge. Kama kimeshindwa, basi tunaendelea na ile iliyopo kwenye Muswada wa Serikali. Kwa hiyo, hii muielewe. Tunapofika kwenye kifungu kile aliyetoa *amendments* hizi atasimama na kujieleza.

Kwa hiyo, tutakwenda na Mheshimiwa Mbunge mmoja na hoja yake ikikubalika kubadilisha kile kifungu, basi yule mwingine hawezi kubadilisha kile kingine, kama wote mnagongana humo kwenye vifungu na kama mnalingana ni vizuri mkakaa mkakubaliana vifungu kuliko kila mtu kusemea kifungu hicho hicho.

Kifungu kingine atasemea Mheshimiwa Halima Mdee, kingine Mheshimiwa Zitto Kabwe na kingine atasemea Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama katika kifungu hicho hicho, hamtaweza kujieleza vizuri. Mkipenda, ni kukubaliana kama mna *amendment* zinazolingana, basi ikawa hoja ya *amendment* zinazolingana.

Kwa hiyo, nimependa kutoa taarifa hii kwa sababu nimeyaona haya na upande wa Serikali, nina uhakika mnazo nakala hizi. Kwa hiyo, naamini kwamba tutakwenda vizuri mchana.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Kikao mpaka saa 11:00 jioni.

*(Saa 06:55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msemaji wa mwisho kwa Muswada huu kabla ya mtoa hoja ni Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora - Mheshimiwa Philip Marmo kuhusu Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, nami napenda nichukue nafasi hii kupitia kwako na kwa Bunge hili kutoa rambirambi zangu na za wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Hanang kwa familia na ndugu wa Marehemu Dr. Aaron Chiduo ambaye tulikuwa naye katika Bunge hili kwa muda mrefu na bila shaka busara zake zilikuwa hazina kubwa katika utendaji na utekelezaji wa shughuli za Bunge na za Serikali. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wa Jimbo la Tunduru na Mheshimiwa Florence Kyendesya aliyechaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM. Ni imani yangu kwamba tutashirikiana pamoja katika kutekeleza majukumu ya Bunge katika kuleta ustawi wa wananchi na wa Taifa letu kwa jumla. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo. Kanuni gani?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kanuni ya 55.

**SPIKA:** Kanuni ya 55.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba mchangiaji haruhusiwi kusoma. Sasa nilikuwa nasema, kama Mheshimiwa Waziri anasoma, ni vizuri akaenda kwenye *Ministerial podium* ili aweze akasoma, la sivyo akikaa hapo itabidi azungumze bila kusoma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sina hakika kama Mheshimiwa Waziri anasoma kwa sababu nipo mbali naye kidogo. Lakini nadhani yeye kama Waziri anayesimamia Sheria, anajua ni marufuku mchangiaji kuwa anasoma moja kwa moja. Kwa hiyo, nadhani anazo *notes* zake atazitumia ili kuendeleza mjadala. Ahsante sana. Naona anamsaidia mtoa hoja,

kwa hiyo, kama Mheshimiwa John Cheyo alivyoshauri, basi anakuja kwenye *podium.* Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo.

*(Hapa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katibua alikwenda kuzungumza kwenye Podium)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na ninamshukuru Mheshimiwa John Cheyo kwa kunikumbusha wajibu wangu kwamba naongea hapa kama Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni adui mkubwa wa haki. Bila haki hakuna amani wala maendeleo yoyote. Ni kutokana na ukweli huo tunapaswa kuilaani rushwa kwa nguvu zetu zote na kubuni mikakati madhubuti ya kutokomeza ikiwa ni pamoja na kutunga sheria kali ya kuidhibiti. Jambo kubwa zaidi ni kwa Watanzania wote kuichukia rushwa kwa sababu ni mzizi wa uovu. Madhehebu ya dini yana majukumu muhimu katika vita hivi. Nimeshuhudia jinsi Waheshimiwa Waheshimiwa wanavyochukia rushwa na hivyo kuwa mstari wa mbele katika kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wakichangia hoja ya Mheshimiwa Marmo, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia madaraka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa ni makubwa mno na wengine wameonesha wasiwasi kwamba uhusiano wa kiutendaji unaopendekezwa katika Muswada huu utapunguza uhuru wa kiutendaji wa TAKURU kama unavyoelekezwa katika Ibara ndogo ya (2) ya Ibara ya 5 ikisomwa pamoja na Ibara za 57 na 58 za Muswada kama zilivyopangwa upya.

Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamependekeza kwamba Ibara ya 59(b) ya Katiba ifanyiwe mabadiliko ili kupunguza mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ninakubaliana nao kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha TAKURU na kuondoa mianya yote ya kuififisha TAKURU katika vita dhidi ya rushwa, bado naona ni muhimu vile vile kutopunguza/kuondoa mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashitaka kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa haki inatendeka kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kwa ufupi falsafa au dhana ya mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kwa nini amepewa mamlaka hayo? Kulingana na ibara ya 59(b)(2) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini. Mamlaka haya anayatekeleza yeye mwenyewe, lakini anaweza kuyakasimisha kwa Maofisa walioko chini yake au kwa wengineo kama TAKURU wanaotekeleza kazi hizi kwa maelekezo yake. Neno "mashitaka" lina maana mashauri ya jinai na rushwa ni makosa ya jinai.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 59(b)(4) ya Katiba inaelekeza kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru katika kutekeleza mamlaka yake na hataingiliwa na mamlaka yoyote. Hata hivyo, anapaswa kuzingatia vitu vitatu ambavyo ni nia ya kutenda haki; kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki; na Maslahi ya umma. Hii ina maana kuwa hata mamlaka yake yana mipaka *(not absolute powers).*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mkurugenzi wa Mashtaka kisheria ndiye peke yake mwenye mamlaka ya kuendesha mashauri ya jinai nchi nzima. Taasisi nyingine kama TAKURU, Polisi, *TRA*, Uhamiaji, Maliasili, na kadhalika zinaendesha mashtaka kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashitaka kwa kibali maalumu chini ya Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka, sura ya 20.

Mamlaka haya ya Mkurugenzi wa Mashtaka hayatofautiani na nchi za wenzetu. Mfano ni nchi ya Uingereza ambayo sehemu kubwa ya mfumo wa Sheria zake ni sawa na wetu *(common law).* Uingereza inayo sheria inayompa Mkurugenzi wa Mashitaka mamlaka zaidi ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote kwa mujibu wa Sheria inayojulikana kama "*Prosecution of Offences Act 1879*" na mabadiliko yake ya mwaka 1985, sambamba na sheria inayojulikana kama *Crown Prosecution Services Act* ya mwaka 1986. Katika sheria hizi, kazi za upelelezi zipo chini ya vyombo vinavyofanya upelelezi na kazi ya kuendesha mashitaka ipo chini ya Mkurugenzi wa Mashitaka *(DPP)*. Mfumo huu wa Uingereza, hutumiwa pia na nchi za Canada, Marekani, Afrika ya Kusini, Uganda na Australia ukiacha tofauti ndogo ndogo zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waheshimiwa Wabunge wafahamu kwamba mashauri yote ya jinai, isipokuwa yale yanayoendeshwa katika Mahakama za Mwanzo, yanaendeshwa kwa jina la Jamhuri. Kwa sababu hiyo, Serikali imekasimisha mamlaka yake kwa Mkurugenzi wa Mashitaka. Mkurugenzi huyu anatokana na waendesha mashtaka au wanasheria waliobobea na wenye maadili mema *(integrity).* Kwa sababu hiyo, hatutegemei kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka atakiuka miiko ya umma katika utendaji kazi wake. Endapo atafanya tofauti na matarajio hayo, hatua stahiki zitapaswa kuchukuliwa na zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliotoa dukuduku zao kuhusu vipengele vya Muswada huu vinavyotoa mamlaka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, wameonesha hofu kubwa kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kuwa kikwazo kwa TAKURU kufanya kazi yake.

Dhana hii sioni kama ni sahihi. Kwanza, ifahamike kuwa TAKUKURU ni chombo cha uchunguzi *(investigation)*. Baada ya uchunguzi wao, inatarajiwa kuwa mtu mwingine ambaye hakuhusika katika upelelezi, lakini mwenye utaalamu wa mashtaka, anapaswa kupitia ushahidi uliokusanywa na kutoa ushauri wa kisheria. Tofauti na TAKURU ambacho kinaonekana kama chombo cha dola, kama Jeshi la Polisi, na kadhalika Mkurugenzi wa Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni taasisi za kiraia zaidi na ambao wanatarajiwa kutenda haki bila maslahi binafsi *(impartial).*

Kwa maoni yangu, hofu inapaswa iwepo pale ambapo TAKURU inaachiwa mamlaka yote, yaani imkamate mtuhumiwa, impeleleze na iendeshe mashtaka *(absolute powers)* na wenzetu wanasema "*Absolute Powers Corrupt and can easily be misused.*" Hii ina maana kuwa endapo hakutakuwa na mamlaka ya *"DPP",* basi kuna uwezekano

mkubwa wa haki kutotendeka. Zile *absolutes* tunazoogopa za *DPP* zinaweza zikahamia kwa TAKURU.

Hata hivyo, kwa sheria ya sasa, TAKURU wana mamlaka ya kupeleleza na kupeleka mashtaka mahakamani katika makosa mengi isipokuwa yale yanayoangukia katika kifungu cha 7, 9, 10 na 16 tu. Hata hivyo, TAKURU inaendesha kesi hizo kwa kibali maalumu cha jumla *(blanket certificate)* kilichotolewa kwa maofisa wa TAKURU na Mkurugenzi wa Mashtaka. Uwezo huo unaishia katika Mahakama za Mahakimu *(Magistrates' Courts).*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu hiyo ndiyo maana kwa sasa Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kutenganisha shughuli za upelelezi na kuendesha mashtaka *(yaani Civilianization of Prosecution)* kwa kuajiri wanasheria 150 na kuwaajiri baadhi ya waendesha mashitaka wa Polisi. Polisi watakaoingizwa katika mpango huu wataajiriwa na Mkurugenzi wa Mashtaka moja kwa moja. Mkakati utakapokamilika, nchi yetu itakuwa imetenganisha shughuli za upelelezi na zile za uendeshaji mashtaka na pengine kesi za kubambikizwa zitakwisha.

Mheshimiwa Spika, dhana hii inaendana na kanuni bora za utoaji haki. Inatia shaka kwa mtu mmoja huyo huyo atuhumu, apeleleze, akamate na kisha ashitaki. Haki siyo kwamba inatakiwa kutendeka tu, bali inatakiwa ionekane inatendeka. Hii ni kama ilivyo katika dhana ya mgawano wa madaraka *(separation of powers)*. Huwezi kuwa mshitaki na Hakimu wewe mwenyewe. Katika nchi zilizoendelea, mgawanyo huu uko wazi kabisa.

Nchini Marekani, kwa mfano, kuna waendesha mashtaka wa Wilaya *(District Attorneys).* Hawa ni raia na huchaguliwa kwa kupigiwa kura miongoni mwa Wanasheria waliobobea. Hawa ndio wenye majukumu ya kuendesha mashtaka katika wilaya zao. Wapelelezi kutoka Jeshi la Polisi au binafsi-wanapaswa kufanya kazi zao na mara nyingi wakisaidiana na Wanasheria wa Ofisi ya *Districrt Attorney* na kumpelekea yeye. Yeye ataamua kama shauri hilo alifikishe mahakamani au vinginevyo, kutegemeana na uzito wa ushahidi uliokusanywa. Kule Uingereza chombo kichonaitwa *Crown Prosecution Services* nao hufanya kazi kama *District Attorneys* wa Marekani.

Mheshimiwa Spika, wakati akichangia hapa Bungeni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, alieleza tatizo la mtumishi mmoja ambaye ametuhumiwa na kusimamishwa kazi kwa takriban miaka mitatu bila kupelekwa mahakamani. Kwa maelezo yake, TAKURU na Polisi wote wanatupiana mpira. Mamlaka pekee huru na ambayo ingeweza kupelekewa malalamiko hayo na kuchukua hatua mara moja ni Mkurugenzi wa Mashtaka. Mtumishi huyo angemwandikia Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliyopo mjini Tanga, Mkuruzenzi wa Mashtaka angeweza kuitisha jalada la upelelezi na kufanya uamuzi wa kumwondolea au vinginevyo, angeweza kuagiza TAKURU na Polisi kila mmoja awasilishe jalada lake kwa ajili ya uchambuzi wa ushahidi uliopo na kisha angefanya uamuzi ambao bila shaka usingechukua muda mrefu kama ilivyotokea hivi

sasa. Hivyo basi, badala ya kuyatilia mashaka mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wayaangalie mamlaka hayo kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika**,** dhana ya ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP's Consent)* haijaanzia hapa kwetu Tanzania. Dhana hii ipo duniani kote hasa katika zile nchi ambazo mashtaka yanaendeshwa na taasisi nyingine tofauti na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka.

Hapa Tanzania, yapo makosa mengi chini ya sheria mbalimbali ambayo yanahitaji ridhaa *(consent)* ya Mkurugenzi wa Mashtaka kabla ya mtuhumiwa kufikishwa mahakamani. Kwa mfano, makosa yote chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, Makosa ya Ugaidi, Makosa chini ya Sheria ya Uchawi, Makosa chini ya Sheria ya Fedha Haramu, Kulala na Maharimu *(incest)* na kadhalika. Hata Umoja wa Mataifa na Umoja wa Jumuia ya Madola unatambua dhana hii na ndiyo maana wanapoandaa sheria mfano *(model legislation)* wanawawekea kipengele cha kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka au Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kutoa kibali cha kushitaki ndiyo inayompatia Mkurugenzi wa Mashtaka fursa ya kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote nchini. Dhana hii haikuanza mwaka huu wala mwaka 2005. Ilikuwepo katika Sheria zetu kabla na baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Kwa mfano ilikuwepo katika kifungu cha 90(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka, Sura ya 20. Lengo la kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka (mara zote ni katika mashauri mazito) ni kuhakikisha kunakuwepo na uwazi katika utendaji na utoaji haki kwa kutenganisha shughuli za upelelezi na shughuli za kuendesha mashtaka, yaani, *"de-link prosecution function from the investigation function."*

Mheshimiwa Spika, mantiki kuwa:-

(a) kuepuka mashtaka ya kusingiziwa na uonevu kwa wananchi, yaani kubambikizia kesi;

(b) kupata fursa ya maoni tofauti juu ya mashtaka yaliyopo; na

(c) kujenga uwezo wa watendaji katika upelelezi na katika uendeshaji wa mashtaka hayo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika sheria ambayo inatarajiwa kufutwa, endapo Muswada huu utapita kuwa sheria, kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka hakihusu makosa yote ya sheria hii kama nilivyoeleza pale mwanzoni. Kifungu cha 57 kinatamka bayana kwamba makosa ya rushwa chini ya kifungu cha 15 hayahusiki na kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka. Kwa maana hiyo, makosa yote ya kuomba na kupokea Rushwa na makosa ya kutoa rushwa yanapelelezwa na kupelekwa mahakamani na TAKURU bila kusubiri kibali cha Mkurugenzi wa Mashitaka.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, dhana hii ipo katika nchi nyingi duniani. Sheria ya Kuzuia Rushwa ya Afrika Kusini, *(Prevention and Combating of Corruption Activities Act, 2004)* ina vipengele vinavyofanana na Muswada wetu huu. Kifungu cha 27 cha sheria hiyo kinatoa mamlaka ya kuamua shauri kupelekwa mahakamani kwa Wakurugenzi wa Mashtaka wa ngazi ya Taifa au Majimbo *(National DPP, Deputy National DPP na DPPs).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezo wa kuendesha mashtaka. Wasiwasi pia umeoneshwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka hana uwezo wa kuendesha kesi za rushwa ukilinganisha na TAKURU. Katika hili, ningependa kuwatoa wasiwasi kuwa Ofisi za Mkurugenzi wa Mashtaka kwa sasa zimeenea karibu Mikoa yote nchini. Ni katika Ofisi hii ambapo ndipo wako Mawakili wengi wamejifunzia kazi na baadhi yao kwenda kuanzisha ofisi binafsi. Pale ndipo Chuo cha Mafunzo na wapo Mawakili wa Serikali waliobobea.

Kwa sasa wapo Mawakili zaidi ya mia mbili na kupitia *civilianization programme,* wanatajiwa kuajiriwa Mawakili wapya 150. Sitakuwa nabahatisha nikisema kwamba TAKURU hadi sasa hawana Wanasheria waliobobea katika uendeshaji wa mashtaka wanaozidi 20. Inawezekana wapo watumishi wengi TAKURU, lakini, wengi wao hawana taaluma ya kuendesha mashauri ya jinai kama alivyo Mkurugenzi wa Mashtaka. Endapo kuna dosari za kiutendaji au upungufu wa mtu binafsi, hilo ni suala lingine na linaweza kutokea hata katika TAKURU.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, panapojitokeza ukiukwaji wa taratibu za ki-mashtaka na mwathirika kufungua kesi ya uonevu au *malicious prosecution*, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ndiyo hubeba dhamana ya kuandaa utetezi wa kesi ya madai husika kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mfano, kwa sasa zipo kesi za watu wanaodai kutotendewa haki na TAKURU ambazo Mkurugenzi wa Mashitaka ameziandalia utetezi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mfano ni kesi mbili za madai zilizofunguliwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mwanza mwaka 2006. Katika moja ya kesi hizi, mlalamikaji anadai shilingi milioni 350. Kimsingi, Katiba na Sheria hazimruhusu Mkurugenzi wa Mashtaka kutumia vibaya mamlaka yake. Pia zipo taratibu za *Judicial Review* ambazo zinaweza kuhakikisha kuwa Mkurugenzi wa Mashitaka hatumii mamlaka yake vibaya.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kueleza kwamba, katika kutekeleza kazi zake, Mkurugenzi wa Mashtaka anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo yaliyoainishwa katika Katiba:-

(a) Nia ya kutenda haki;

(b) Kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki; na

(c) Maslahi ya umma.

Kwa kuwa yeye ni mtumishi wa Umma aliyeteuliwa na kuapishwa na Rais, anaweza kuondolewa kazini endapo hatatekeleza kazi zake kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi nilioufanya umelenga kutoa ufafanuzi wa mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka na dhana ya kibali cha kushitaki au kuondoa mashtaka. Hata hivyo, kwa kuwa mashaka ni hulka ya binadamu na kwa kuzingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, Serikali itafanya mabadiliko katika ibara ya 57 kama ilivyopangwa upya ili kumpatia Mkurugenzi wa Mashitaka muda maalum wa kufanya uamuzi kuhusu kutoa kibali cha kuendesha mashtaka mahakamani na Serikali inapendekeza siku 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema kuwa katika kutokomeza rushwa, tuwe waangalifu tusije tukaleta adui mwingine hususan uonevu unaotokana na chuki, wivu na mambo yanayofanana na hayo. Kama nilivyosema *absolute power corrupts* na kwa hiyo, TAKURU hii ambayo tunategemea kupiga vita au kutokomeza rushwa ikipewa *absolute powers* bila *checks and balances* inaweza ikageuka tena kuwa taabu kama hivi anavyolalamikiwa *DPP*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kukushukuru tena, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na ninaiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ahsante sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora ambaye ndiye mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa katika siku hizi mbili za Muswada huu. Mheshimiwa Waziri karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu, naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa za Marehemu aliyekuwa Mbunge wa Gairo, Hayati Dr. Aaron Chiduo, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nipate kujibu hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakijadili Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mmoja wa Miswada iliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Hii ni ishara kuwa suala la kupambana na rushwa katika nchi yetu linapewa umuhimu mkubwa na wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, katika kuchangia Muswada huu, wameweka utaifa mbele na kuweka pembeni tofauti zao za kiitikadi. Naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuchangia hoja hii, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutaka kujua tafsiri na namna ya neno rushwa licha ya ukweli kuwa tafsiri ya rushwa inatokana na matendo au vitendo vya mtu binafsi.

Aidha, baadhi ya michango imelenga kwa namna moja au nyingine kwenye Sheria Mama, yaani Katiba ya Nchi. Kwa hali hiyo, Sheria hii haiwezi kuchukua nafasi ya Sheria Mama yaani Katiba. Hivyo, michango na maoni yote yanayohusu Katiba ya nchi yatazingatiwa wakati ambapo marekebisho ya Katiba yatakuwa yakijadiliwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wale wote waliochangia katika Muswada huu aidha kwa kuzungumza kwa maneno humu ndani au kwa maandishi kwa ushauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 57. Kati yao Waheshimiwa Wabunge 31 walitoa mchango wao kwa kuzungumza humu Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 26 walitoa michango yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua Waheshimiwa Wabunge hao, kwanza wale waliochangia kwa kuzungumza ambao ni Mheshimiwa Tatu Ntimizi - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Juma Njwayo na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. *(Makofi)*

Naona imechanganywa, lakini nafikiri Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi naye alikuwa amechangia Muswada huu na wengineo ambao kama sitawataja, naomba niseme kwamba majina yao yatakuwa katika *Hansard* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wale ambao walichangia kwa maandishi ni wafuatao:- Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Masolwa Masolwa, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Iddi Azzan, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Grace Kiwelu na Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo na Mheshimiwa Magalle Shibuda. Nimesahau kumtaja Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye alikuwa wa mwisho kuchangia katika Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilionesha wasiwasi wake kuhusu madaraka aliyopewa Mwendesha Mashitaka, yaani *DPP*.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mary Nagu amelielezea eneo hili vizuri sana na sisi kwa upande wa Serikali kama alivyosema Waziri wa Katiba na Sheria tumeona wasiwasi wa Waheshimiwa Wabunge na tutayafanyia kazi maoni yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pia ilitoa pendekezo la kuomba muda wa miezi sita toka Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kushika mali za watuhumiwa na kwamba miezi hiyo sita siyo mingi.

Sisi tunasema kwamba miezi hii sita siyo mingi sana kwa sababu ikumbukwe hapa tunaongea rushwa kubwa kubwa, yaani *grant corruption* ambazo zinahusisha nyaraka na vielelezo mbalimbali ambavyo kwa tafsiri pana, vielelezo hivyo navyo pia ni mali na vinashikiliwa. Ukizingatia kuwa mali hizi zinaweza kumhusisha mtuhumiwa au watuhumiwa ambao wakati wa upelelezi wako nje ya nchi na hivyo kukamilisha kutahitaji kupatikana kwao. Lakini pia kwa msingi wa kifungu hiki, kinakidhi mahitaji haya ya kuondolewa kwake kutodhoofisha uwezo na ustadi wa kupata ushahidi utakaoweza kutumika wakati wa kuendesha kesi mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliona kuwa adhabu zilizoainishwa katika Muswada huu aidha zina upungufu au hazilingani na makosa husika na kwamba adhabu ya faini ilingane na kosa. Serikali imelipokea pendekezo hilo toka awali na tulikuwa tumelizingatia.

Aidha, Serikali ilikuwa imepokea pendekezo la Kamati kuhusu umuhimu wa watumishi wa Idara, Wizara na Mashirika ya Umma kuorodhesha mali zao pindi wanapoajiriwa. Pendekezo hili kwa sasa linazingatiwa kwa watumishi wote wa umma kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kwa upande wa TAKURU nao wana utaratibu wa ndani kwamba watumishi wake uorodheshe mali zao na namna walivyozipata.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kambi ya Upinzani kupitia Msemaji wake, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma kwa mchango wake mzuri wa kuboresha Muswada wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imezungumzia juu ya kutokuwepo kwa tafsiri ya neno *'corruption',* yaani rushwa katika Muswada huu.

Hata hivyo, kwa mara nyingine napenda niseme kwamba neno *'corruption'* tafsiri yake kwa kweli ni ngumu. Duniani kote Sheria haitoi tafsiri hiyo na badala yake sheria husika hutamka matendo ya rushwa na ndiyo matendo hayo yanayoadhibiwa na siyo neno lenyewe.

Aidha, kulingana na *best practises* duniani, tafsiri ya leo ya neno hilo inaweza kuwa tafsiri finyu au potofu kwa mazingira ya kesho na duniani kote hakuna tafsiri moja inayokubalika ya neno hilo inayokidhi maana pana ya neno lenyewe. Hata katika Afrika Mashariki, majirani zetu Kenya rushwa huiita ufisadi, sisi tunaita rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia imetambua kuwa katika Muswada wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa kwamba kutakuwa pia na mchango wa umma. Maoni ya Kamati hiyo ili kulinda uhuru wa chombo hiki utamkwe katika Katiba ya Nchi, hili nalo linahitaji mabadiliko ya Katiba pia imepokewa na itafanyiwa kazi pindi mjadala wa Katiba utakapoanza hapo siku za usoni. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani ilipendekeza nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa ili iwe ya Kikatiba. Mkurugenzi huyo awajibike Bungeni. Hoja hii pia inagusa Katiba na Serikali inaipokea mpaka hapo mjadala wa Katiba, nayo pia tutaiweka maanani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilisema pia kifungu cha 12 hakielezi taratibu za kufuatwa na Maafisa wa Taasisi wa Kuzuia Rushwa wakati wa upekuzi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba katika kifungu hicho Maafisa wa Taasisi itakayoundwa wametamkwa katika Ibara ya sasa ya 4 ya Muswada na watakuwa na sifa ambazo ni sawa na zile za Afisa Polisi mwenye cheo cha juu cha Mrakibu Masaidizi wa Polisi; na kwa maana hiyo basi Maafisa wa Taasisi wataongozwa pia na Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai sura ya 20. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani ilihoji uwezo wa chombo kitakachoundwa kufanya upelelezi baada ya neno *investigation* kuondolewa katika marekebisho yaliyofanywa katika Kifungu cha 10(2). Napenda kuifahamisha Kambi ya Upinzani na Bunge kwa ujumla kuwa hoja hiyo imezingatiwa na kwa hiyo, ki fungu hicho kitasomeka kama ifuatavyo sasa. Naomba ninukuu: *"The Director General may assume investigation or prosecution commenced by the Police or any other law enforcement agency for an offence involving corruption."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani alizungumzia hoja ya kuwa kifungu cha 18 cha Muswada kinahusisha watumishi wa umma pekee. Napenda kutoa ufafanuzi kuwa suala hili limezingatiwa katika Muswada na sekta binafsi linatamkwa na Muswada huu. Kuhusu suala la Taasisi kuwekewa taratibu za utendaji na kutoa taarifa kwa jamii kupitia Kamati ya Bunge, napenda kurejea tena kwamba suala hili limezingatiwa na utaratibu utawekwa wa kutoa taarifa kwenye Kamati za Bunge husika.

Mheshimiwa Spika, pia ilitokea hoja kuhusu makosa ya rushwa katika siasa kutokuhusishwa katika Muswada huu. Kama nilivyoeleza hapo awali katika hotuba yangu ya kuwasilisha hoja. Wadau wengi walipenda Muswada huu ujumuishe vitendo vya rushwa katika siasa. Lakini baada ya kutafakari tumeona kwamba suala hili lisubiri mjadala wa Kitaifa kuhusu namna bora zaidi ya kushughulikia rushwa katika chaguzi za kisiasa hasa baada ya kurekebisha Sheria ya Uchaguzi yaani Sheria namba moja ya mwaka 1985, sura ya 343 na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, sura ya 258 ya Sheria zetu. Tatizo lililopo hivi sasa ni kwamba tunashughulikia matokeo yaani *consequences* badala ya chanzo halisi cha rushwa. Kuhusu namna ya kupokea michango na fedha za wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi, vyama vya siasa kupokea michango ya fedha lakini taratibu zake haziko bayana katika utaratibu wa sheria hizo kwa sasa. Kwa msingi huo kuna haja sasa ya kufanyia marekebisho sheria hizo kama kiini cha tatizo badala ya kutibu matokeo katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kufafanua hapa kwamba sasa hivi Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaandaa hadidu za rejea za mjadala wa Kitaifa wa namna bora za kuendesha chaguzi za dola na pengine baada ya mjadala huo kutakuwa na mapendekezo ya aidha, sheria mpya au kubadilisha Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 na ile Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijatambua michango ya Waheshimiwa mbalimbali nimeona nitoe maelezo machache kuhusu hoja ya Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, kuhusu nafasi ya Tanzania katika tathmini iliyofanywa na vyombo mbalimbali vya Kimataifa vinavyotathmini hali yetu ya rushwa. Tukiangalia kwa makini na tukijilinganisha na wenzetu katika Kanda, hali yetu sio mbaya kiasi cha kutisha lakini hii si lengo letu. Sote tutafahamu kwamba rushwa ni uchafu. Unapoishi ndani ya nyumba chafu usijilinganishe na mwenzako anayeishi katika nyumba chafu nyingine jirani, hufahamu pengine nyumba hiyo ina madirisha. Kwa hiyo, sisi tunapambana na rushwa kwa mazingira yetu na tumeleta sheria hii kwa ajili hiyo si kujilinganisha na nchi nyingine ingawa hii itasaidia pia kwa wale ambao wanatutathmini.

Pili, Wenyeviti wa Kamati za Bunge waliosafiri nchi mbalimbali wameona mambo mazuri, wameelezwa kwamba nchi zao hakuna rushwa. Mimi nisingependa lolote kuhusu hili. Lakini mimi naamini duniani hakuna nchi ambayo hakuna rushwa. Nchi walizotaja sisi tunahisi kwamba wametuingiza katika masomo makubwa katika sekta mbalimbali. Inawezekana nchi hizo zisihusike moja kwa moja, lakini kampuni zao zimehusika na pengine kwa kuwezeshwa na Balozi zao na nchi zao na hasara iliyotokana na zoezi hili ni kubwa sana. Nisingependa kuzitaja lakini ni nchi ambazo zina *score* ya juu sana katika alama za *transparency international* na zingine. Ndiyo hizo ambazo Wenyeviti wetu wameenda, tungewa-*brief* mapema wangeuliza maswali, mbona tunasikia kwamba kampuni zenu zinajihusisha kikamilifu katika eneo la rushwa katika nchi yetu na tuna taarifa kwamba ni Balozi na Serikali zenu zinawezesha waweze kurubuni watu wetu. Ningeweza kutoa mifano hapa lakini pengine si wakati muafaka wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Baadhi ya Wabunge katika hoja zao wamelinganisha na nchi jirani, kwamba uchumi wa nchi jirani pamoja na kusikia kwamba kuna rushwa, chumi hizo zinakuwa. Mimi narejea kusema kwamba hatuwezi kujilinganisha. Hatujui misingi ya nchi hiyo ni nini. Kama ni nchi ninayoifahamu misingi yake ya uchumi ilishajikita vizuri kuanzia miaka ya 1920, kwenye viwanda, kwenye mawasiliano na kadhalika. Kwa hiyo, tukipima utaratibu wa mapambano dhidi ya rushwa wa nchi jirani hatutafika. Kwanza kama ni nchi hiyo wanayoitaja kwa sasa inajitegemea karibu kwa asilimia 96 ya Bajeti yake. Sisi hatujafika hata asimilia 60. Hii ni ishara kwamba tunatofauti kubwa ya misingi ya uchumi wa nchi yetu na lazima mapambano ya rushwa Tanzania yazingatie mazingira ya Tanzania, si mazingira ya nchi yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kutambua michango ya Waheshimiwa Wabunge waliotoa hoja ya kutaka chombo kitakachoundwa cha Kuzuia na Kupambana na Rushwa kiwe huru ambao ni pamoja na Mheshimiwa Tatu Ntimizi aliyezungumza kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, aliyezungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Idd Azzan na pia Mheshimiwa James Lembeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea na kuahidi kuzingatia hoja ya kuwa ni Taasisi ya Kupambana na Rushwa kuwa ya Kikatiba na tutafanya hivyo katika mjadala wa kubadilisha Katiba utakapowadia. Serikali pia imepokea na inazingatia hoja ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu nafasi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kama alivyosema pale awali na baadae pengine tunaweza tukatoa tamko rasmi hapa. Lakini pamoja na maelezo hayo napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa umezingatiwa kwa kutamka bayana katika kifungu cha tano, kifungu kidogo cha pili kwa kuongeza maneno *operational independent,* tuna maana ya uhuru bila kuingiliwa na chombo chochote katika eneo la uchunguzi na katika eneo pia la kuendesha mashtaka kwa mashtaka ambayo yameidhinishwa na *DPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua mchango wa Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi kuhusu chombo kitakachoundwa kuwa na ofisi maeneo ya wazi na kuwajibika kutoa elimu kwa umma na kuwa na Ofisi ya Uhusiano. Hoja hii imezingatiwa na itahusishwa katika Muundo wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Napenda kusema kwamba hata sasa hivi karibu nusu ya Bajeti ya TAKURU inatumika katika elimu ya rushwa kwa umma. Kwa hiyo, kwa kuzingatia maoni ya Wabunge tutaimarisha eneo hili la elimu ya rushwa kwa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuhusu hoja ya kuongezwa kwa adhabu kwa watuhumiwa wa makosa ya rushwa ikiwa ni pamoja na maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala

kupitia kwa Msemaji wake Mheshimiwa Tatu Ntimizi na wale Wabunge wote waliotoa maoni yao katika eneo hili. Hoja hizi za kutoa adhabu kali zitolewe kwa wala rushwa, zimepokelewa na Serikali na imezingatiwa mkiona katika jedwali la mabadiliko tuliyoyafanya katika ngazi ya Kamati hivi karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwatambua Waheshimwa Wabunge waliotoa mchango wao wa kutaka Muswada uwe na kifungu cha kutoa mamlaka kwa taasisi hii ili kushughulikia vitendo vya rushwa katika chaguzi hiyo imetajwa na wengi na nisingependa kurudia tena na naamini kwamba sasa tumefikia mahala pa kusema bila wasiwasi kwamba Muswada huu usingeweza kutatua matatizo yote ya rushwa katika eneo la uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira, mafunzo na maslahi ya watumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Waheshimiwa Wabunge, wamependekeza taasisi itakayoundwa isitoe ajira kwa kutangaza badala yake wafanye kwa utambuzi yaani *spotting* au *vetting,* pia wapate mafunzo ya ndani na nje bila kuogopa gharama jambo ambalo litasaidia kuboresha utendaji wa taasisi. Aidha, Waheshimiwa Wabunge walipendekeza watumishi wapewe maslahi mazuri kwa kuboresha mishahara, kupatiwa nyumba za kuishi na usafiri ili kuboresha uadilifu kwa watumishi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja hizi zimezingatiwa na kwamba ajira ya TAKURU ilikuwa inazingatia toka awali upekuzi yaani *vetting* na katika Taasisi iliyoundwa tutazingatia utambuzi yaani *spotting,* pamoja na hayo watumishi wa taasisi wataendelea kula kiapo cha uaminifu kwa kazi zao na pia TAKURU iliyopo imeshaanzisha utaratibu wa ndani wa watumishi kutaja mali zao kama nilivyosema hapo awali ili kuboresha uadilifu na uaminifu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imepokea hoja ya kuboresha maslahi ya watumishi, kwa hakika kila inapowezekana Serikali imeongeza viwango vya mishahara ya watumishi wa TAKURU ili kuboresha utendeji wao wa kazi kadri hali ya fedha inavyokuwa inaruhusu na mimi nakubaliana na hoja kuwa usalama wa Mkurugenzi Mkuu na Maafisa wa ngazi za juu unafaa ulindwe Kikatiba hivyo suala hilo pia litazingatiwa wakati wa marekebisho ya Katiba yatakapowadia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue fursa hii kuwatambua wale Waheshimiwa Wabunge na hasa Mheshimiwa Mwenyekiti wa *APNAC* Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, ambao wamechangia kuhusu sifa za Mkurugenzi Mkuu na Maafisa wa ngazi za juu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, upatikanaji wao na usalama wa ajira zao. Napenda niwajulishe rasmi Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali imepokea maoni yao haya na kwa kweli inayafanyia kazi na nawahakikishia kwamba muda huu wote watumishi wetu walikuwa waaminifu na wamekuwa wakisaidia sana jamii na taasisi, na hadi leo hatujapata dosari yoyote kwamba wataalamu wetu wamekuwa na matatizo katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ambayo pia imeguswa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. Napenda kusema kwamba kimsingi uchunguzi wa kesi hii iliyomuhusu mtumishi kama alivyotaja Mheshimiwa Waziri ilishafikia hatua nzuri na ni mwezi wa nne mwaka 2004 kesi ilianza kusikilizwa na baadaye yalitokea mabishano ya kisheria ambayo yalisababisha jalada kupelekwa Mahakama Kuu Tanga. Jalada hilo lilirudishwa tena Mahakama ya Wilaya ya Pangani na hivi karibuni na tusingependa sasa kulijadili kwa sababu suala hili linasubiri uamuzi wa Mahakama. Naomba Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, avute kheri suala hili litaamuliwa na Mahakama, tusizidi kulifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumtambua Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuhusiana na hoja ya kuwa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa itakayoundwa kuachana na rushwa ndogo ndogo ya kukamata watumishi wa ngazi ya chini kwa njia ya pesa za unga na badala yake ishughulike na rushwa kubwa. *(Makofi)*

Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuwa Serikali imezingatia hoja hiyo hata hivyo kutokana na kero ya rushwa ya ndogo ndogo kumgusa mwananchi mmoja mmoja tena wenye kipato cha chini kabisa huduma zinazotolewa bure na Serikali na hivyo kushindwa kupata huduma hizo au kuzipata kwa usumbufu, ni busara pia tukashughulika nazo na pia Serikali kujijengea imani na wananchi kwa ajili hiyo. Kwa upande wa kupambana na rushwa kubwa kubwa jitihada za kujidhatiti ni pamoja na kuwa na Muswada huu. *(Makofi)*

Napenda pia kutambua mchango wa Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, katika eneo hili aliyetoa hoja kwamba kutaka Muswada huu utamke pia na Tanzania Visiwani badala ya ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba eneo la utawala bora si eneo la Muungano. Lakini kwa vile kosa la rushwa ni kosa la jinai kosa hili litakapotendeka katika eneo la Tanzania Zanzibar na linahusu watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au raia wa Tanzania Bara basi sheria hii itachukua mkondo wake lakini kama nilivyosema pale awali ni kwa sababu pia ya kushirikiana mamlaka mbalimbali ya nje na ndani ya nchi. Sasa hivi tunawasiliana na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi na tunatarajia kwamba na wao watatunga sheria kama hii na tatizo litakuwa limekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ilitolewa na Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba kuna haja ya kuboresha mahusiano ya vyombo vya upelelezi vya mashtaka ndani na nje ya nchi, pendekezo hili kwa kweli ni zuri na tutalizingatia katika jedwali la marekebisho kwa sababu makosa ya rushwa yatatendeka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania, ni vema kwamba sheria hii ikalitambua hilo.

Mheshimiwa Spika baada ya kusema hayo napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ya dhati na ya kina na endelevu na kama

nilivyosema tutayazingatia na nina hakika michango hiyo itatusaidia sana kwenye kutunga Kanuni za utekelezaji wa sheria hizi.

Kwa yule Mheshimiwa Mbunge ambaye ataona pengine hatujajibu hoja yake tunaandaa jedwali la kujibu hoja zote zilizotolewa na tahakikisha kwamba itawafikia wakati wowote baada ya Mkutano huu kuahirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 4

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kama Katiba ilivyosema kuna marekebisho kidogo ambayo nilileta mbele yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimeridhia *UN Convention,* imeridhia *AU Convention* katika rushwa, vile vile imeridhia *protocol* ya *SADC countries* kuhusiana na suala zima la rushwa. Sasa tukiangalia katika *clause 4 objective* ya rushwa imeelezewa katika dhana nyembamba sana, sasa kwa kuzingatia kwamba katika hizo *convention* zote tatu, *convention* mbili na *protocol* moja, *convention* kwa mapana nilishauri kwamba hizi zingeingizwa badala ya ile ambayo ilikuwepo na vile vile suala hili tuli-*raise* kwenye Kamati na Mheshimiwa Waziri akaonekana amekubaliana nalo kwa asilimia mia moja. Sasa labda wakati ananijibu aniambie kwa

nini alikubali halafu akaenda kukataa na kutakuwa na madhara gani kama hizi sababu tatu ambazo ni za msingi na zimeelezwa katika *convention* mbili na ile *protocol* moja ya *SADC* ambayo sisi tumeridhia zisiwekwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Halima Mdee, kwa jitihada zake anazozifanya katika kufuatilia mikataba hii ya Kimataifa.

Katika jedwali aliloleta Mheshimiwa Halima Mdee katika *clause* hii ya 4(1) yale yote aliyoorodhesha katika (a), (b) na (c) yeye ameyahamisha kutoka katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa kwa maana ya rushwa yaani *United Nations Convention Against Corruption* na hili jambo ni zuri kwa sababu sisi tumeridhia Mkataba ule wote na kwa nia nzuri, lakini kwa kufahamu kwamba si kwamba tumeridhia Mkataba wa Afrika kwa kupambana na rushwa na itifaki ya *SADC* dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeweza kuhamisha masharti yote ya Mikataba hii Muswada huu ungekuwa mgumu sana, tulichofanya ni kujaribu kufanya uhariri bila kupoteza malengo ya Mikataba hii na tumepanua wigo zaidi kwa sababu badala ya sisi kuhamisha, tumejaribu kutaja au kuchukua masharti yale, kwanza tuliyaweka kwenye *preamble,* halafu tukayaweka hapa lakini pia katika vifungu husika, tumejaribu *catch* ile dhamira halisi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa, badala mkataba neno kwa neno. Kwa sababu lengo letu ni kutekeleza dhamira ya mkutano, sio kuhamisha neno kwa neno.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, labda ifahamike kwamba hizi *convention* ukishasaini maana yake unazi-*domesticate*. Sasa Mheshimiwa anasema kwamba kuna maeneo ambayo yapo ambayo yanafanania kama hayo ambayo yanasema nime-*copy* na ku-*paste*.

Sasa labda aniambie ni maeneo gani ambayo yapo ili kunishawishi kwamba katika hiki kipengele ambacho mimi nahoji inawezekana vipo ndani ya vipengele ambapo mimi sijui. Lakini mimi kwa mtazamo wangu sijaona, na ndiyo maana nimerudia kumuuliza aniambie kungekuwa kuna madhara gani yangewekwa ukizingatia kwamba tumeridhia na ukisharidhia maana yake una *domesticate,* sasa hivi vipengele vitatu vina madhara gani sana yakiwepo hapo?

**MWENYEKITI:** Lakini Mheshimiwa Halima Mdee, tukisharidhia, si ndiyo tunafungwa na hivyo vyote? Maana yake tume-*rectify* huo mkataba. Sasa ni lazima turudie, ninavyoona *practice* katika Bunge na Mabunge yote nadhani, haturejei tena katika mikataba yote ya Kimataifa, kuhusu afya, kilimo na kuhusu mazingira yote tena tukapitisha sheria mpya tukinukuu neno kwa neno. Haitoshi tu kwamba sisi ni wanachama waadilifu, na mikataba hiyo inatufunga? Mheshimiwa Dr. Slaa ulikuwa na chochote cha kuongeza hapo?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina la kuongezea, kwanza nakubaliana na hoja yako pamoja na kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Halima Mdee, mkataba ule wa Umoja wa Mataifa unataka tu-*domesticate,* na tunapo-*domesticate* tunachukue ile *context* lakini labda niridhike na maelezo yako.

Sasa tatizo linakuja wapi? Tatizo linakuja kwamba katika kifungu cha 4(1) ambapo ni *objective* muhimu sana, kwa nchi inayopambana kabisa na suala hili gumu tafsiri ya neno *Good Governance* ni ngumu sana, na labda nieleze hapa kwamba mimi nimewakilisha Bunge lako hili Tukufu kwa miaka mitano na wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya tulichogombana daima ni *definition* ya *Good Governance* na nimeangalia kwenye *section* ya *interpretation* hakuna *definition* ya *Good Governance,* na ndiyo maana nilidhani kwamba maneno haya ambayo amependekeza Mheshimiwa Halima Mdee, yana-*capture* ile dhana nzima katika mapambano. Vinginevyo tumetoa neno ambalo hatukuli-*define* kama *Good Governance promotion and enhancement* sasa tuna-*promote* na ku-*enhance* kitu ambacho hatuja-*define* lakini hakina *objective* zake na tunakiweka kama *objective*.

Mimi nilidhani hapa kuna *definitions* kubwa inayohitaji kwa kweli wote tukae na *objective* moja inayoeleweka na kwa kuwa sehemu ya *preamble* kimsingi Mahakamani *preamble* haiendi kwa utaratibu wa kawaida inayoenda ni sheria yenyewe. Sasa nilidhani hii ni sehemu muhimu ambayo itatusaidia katika ufafanuzi wa taratibu zetu Mahakamani. Waziri angetusaidia, kuna madhara gani kuweka mambo haya wazi na haya mambo ambayo tunafikiri katika mapambano ndiyo silaha ya kwanza kabisa inayofafanua na kuonyesha kwa uwazi kila tunachotaka kukifanya. Madhara na nini kuyaweka japo ni kweli ulivyosema hatukopi kila kitu, na hapa hatukukopi kila kitu, Mkataba wa Umoja wa Mataifa, una *page* zaidi ya arobaini, na tumechukua hapa *paragraph* kama tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, sisi tumeridhia Mkataba huu na katika kuufanya uwe wetu kwa maana ya kuu-*domesticate*. Tuna-u-*domesticate* kwa mazingira yetu. Mkataba huu unavyotekelezwa na nchi mbali mbali, unatekelezwa kulingana na mazingira ya nchi husika, ndiyo maana sisi tulipoona tume-*catch* dhamira halisi ya Mikataba hii na tukifahamu fika kwamba kutakapotokea tatizo na sheria hii, Mkataba ule utajadiliwa hata Mahakamani.

Sisi tulikuwa tunakwepa kuhamisha neno kwa neno yale yote yaliyo katika Mkataba kwa sababu Mkataba malengo yake baadae ni kutuwezesha sisi tuutumie kwa mazingira yetu. Sisi Muswada huu tumeuleta ku-u-*domesticate* Mkataba wa Umoja wa Mataifa katika mazingira ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Na isitoshe, nadhani ukiusoma huu Muswada wote vizuri, kwa sasa nisingependa kuwahisha shughuli. Lakini kama Mwenyekiti, ningeweza kuwaambia muangalie Ibara ya 7 au Kifungu cha 7(e) ambayo inafanana kabisa na hii (b) anayotaka Mheshimiwa Halima Mdee. Inasema; *"Cooporate and collaborate with International Institutions,Agencies or Organizations in fight against corruption."* Ya Mheshimiwa Halima Mdee inasema; *"Facilitate and support Inter-Instituional coopotration and technical assistance and ta – ta – ta.* Yote ni mambo ya kushirikiana. *(Makofi)*

Mimi nadhani hakuna zito sana hapa na sikubaliani na Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba *preamble* siyo sehemu ya sheria. *Preamble* ni muhimu ingawa yenyewe huwezi kuiweka kama sehemu ya mashtaka, lakini *preamble* ni muhimu. Ukiisoma *preamble* ya Muswada huu ina nguvu sana; *"Tanzania to remain a corruption free state, adhering to the principals of freedom, equality, justice, brotherhood, peace*…Lo! Jamani, tunaweza kusema zaidi ya hapa!

Sasa nashauriwa kwamba *amendments* inabidi tuipigie kura ndiyo utaratibu ingawa mimi nilidhani wenyewe hawakui-*press further*. Mnahitaji tuipigie kura kweli! Mimi nadhani Mheshimiwa Dr. Slaa ninavyokufahamu ulivyo *reasonable,* nadhani jambo hili limekwisha! Ahsante sana kwa hiyo, hakuna haja! *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6, lengo lilikuwa ni *security of tenure*. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi mbele ya hili Bunge kwamba hilo suala analishughulikia, nina amini kwamba atanieleza sasa hivi ndani ya muda gani tutegemee kutakuwa na hayo mabadiliko ambayo yatapelekea huyu Mkurugenzi wa *PCB security* yake iwe imekuwa *provided* kwenye sheria.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru tena Mheshimiwa Halima Mdee kwa angalizo hili. Muda wote tumejaribu kurejea kwamba Taasisi hii ni Taasisi ya Serikali, ni Idara ya Serikali. Katika Idara ya Serikali kuna Ikama na taratibu ambazo zinajulikana. Nilikuwa nasema kwamba wakati wa mjadala wa mabadiliko ya Katiba, basi suala hili pia litakuwa suala ambalo litajadiliwa na wakati ambapo chombo hiki kitakuwa chombo cha Kikatiba. Kwa sasa taasisi ni Idara ya Serikali kama Idara zingine. Kwa hiyo, tunazingatia Ikama na *regulations* zilizopo. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi sioni haja ya kuambiwa kwamba suala hili kwa kweli lisubiri kwa sababu mbili, kwanza, si suala la Kikatiba. Kuweka *security of tenure* kwa maana ya kusema kwamba huyu Bwana akiteuliwa ataondolewa kwa sababu hizi na hizi...

**SPIKA:** Au huyu Bibi!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Au huyu Bibi! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haihitaji Katiba na tayari tuna mifano ya aina hiyo. Sheria ya *TRA* tuliyotunga ndani ya Bunge hili, inatoa sifa kama hizo hizo na kutoa *security* ya *tenure* na kueleza ni sababu zipi zinafanya Mkurugenzi wa *TRA* kuondolewa.

Mimi naamini kabisa kwamba *TRA* tumefanikiwa kwa sababu tuliwapa mazingira yanayofanya yule Bwana ajiamini kufanya kazi na naamini uzito wa taasisi hii japo haituletei hela kwa maana ya kutuletea hela, lakini inalinda hela zetu. Kwa hiyo, ni nyeti sawa na *TRA*. Nilidhani hapa tungeweza kuweka sifa zile zile kama tulivyoweka. Sasa Waziri hajanieleza kwa nini lingojee baadae wakati lingeweza kuwekwa hapa kama tulivyoweka kwenye sheria iliyounda *TRA*. Kwa *TRA* hatukuweka kwenye Katiba, tuliweka kwenye sheria na hapa ndio mahali pekee tungeweza kuweka hapa na ndio maana katika pendekezo la Mheshimiwa Halima Mdee, nadhani imeweka tu ni sababu zipi huyu Bwana anaweza kuondolewa na ndio *security of tenure* tunayoongea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Dr. Slaa tunatoka mbali sana, isipokuwa tu tumeingia kwenye nyumba hii kwa mabasi tofauti na huwa ana kumbukumbu sana na bila shaka atakumbuka tumejadili nini wakati wa semina ya *APNAC,* wakati tunawasikiliza wadau *(Public Hearing),* naye ni Mjumbe wa Kamati. Napenda nirejee niliyoyasema kwenye semina ya *APNAC* na wakati tukiwasikiliza wadau kwenye *Public Hearing* na kwenye Kamati kwamba chombo hiki kina historia ndefu ndugu zangu. Kilipoanzishwa mwaka wa 1975 kama *Anti-Corruption Scuard,* ilikuwa bado ni sehemu ya Polisi, sehemu ya *CID* na mpaka leo bado ina sura hiyo! Bado hatujafikia hatua ya kui-*detouch* kama chombo cha Kijeshi. Kwa hiyo, ni tofauti kabisa na *TRA* na ndio maana nasema itakapofika wakati wa mjadala wa Katiba tuondoe chombo hiki kama taasisi ya Serikali, iwe chombo cha Kikatiba kama *Human Rights Commission,* wakati huo haya yote tutayaorodhesha. Lakini kwa sasa, chombo hiki hatujaki-*detouch,* bado ni taasisi ya Serikali na ni taasisi ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, ukizingatia kwamba Muswada huu unakusudia kuiboresha sheria ya kupambana na rushwa na kwa sehemu kubwa sana tumepata maoni mazuri na ni Muswada ambao unaunda sheria bora zaidi, je, tusingesubiri hilo lengo analojataja Mheshimiwa Waziri ambalo siyo mbali sana?

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna *commitment* ya Serikali, basi hatuna sababu ya kubishana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo mazuri kabisa ya Waziri na kwa sababu kipengele hiki sikutaka kuondoa ile mantiki yenyewe ilivyo, ilikuwa ni maneno tu; *direction* na kuweka *consent,* basi mimi naomba marekebisho hayo niyaondoe. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE :** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Na mimi niungane na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kutokana na ukweli kwamba katika maelezo aliyoleta Mheshimiwa Waziri, yanaonyesha yamejibu kile ambacho kilizua hofu katika kipengele hiki. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8

**MHE. MOHAMED RiSHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wakati wa kuchangia, nilijaribu kugusia katika Kifungu hiki cha 8(4)(a) ambapo panasema mamlaka ya Mkurugenzi, ambapo inasema kwamba; "Pale ambapo Mkurugenzi Mkuu ataridhika kuwa kosa chini ya sheria hii linaweza kuwa limetendwa na mtu yeyote." Na wakati wa kuchangia katika Muswada huu nilizungumzia Ibara ya 56(3) ya Katiba yetu ambayo inazungumzia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatoshitakiwa baada ya kumaliza shughuli zake za urais. *(Makofi)*

Sasa mimi siyo mtaalamu wa sheria, lakini naona kama hapa Katiba na sheria kama zinagongana. Nikasema kwa nini tusiongeze hapa; "bila ya kuathiri Ibara ya 56(3) cha Katiba." Lakini naona hilo Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja hakuweza kulielezea. Sasa mimi swali langu kwa Mheshimiwa Waziri nauliza, je, hii haitoathiri kwa maana ya kuonyesha kwamba kuna mgongano wa sheria na Katiba katika suala hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba radhi kwamba hatukuweza kumfafanulia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ufafanuzi aliohitaji wakati akichangia Muswada huu. Kwanza niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge kwamba siyo vema kuandika kila kitu katika sheria kwa vile huwezi kubashiri huko mbele ya safari kutakuwa na nini. Sheria inakuwa ni *skeleton* tu, baadae nyama inawekwa na sheria ndogo ndogo na mazoea na mila na desturi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora zaidi maeneo mengine baadae wanaokuja waweze kuyashughulikia kwa kutumia mila na desturi badala ya kuandika andika katika sheria kwa sababu sheria haiwezi kubashiri huko mbele ya safari kutakuwa na nini. Kwa sasa alivyosema ni kweli na katika hali halisi ndio ilivyo na ndio mila na desturi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I think I have delivered the message*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nimekuelewa sana na kwa vyovyote vile hata zile sheria zilizoko kama *Penal Code* na kadhalika, hazitaji kila moja *exception* ya Rais. Zimeorodhesha mambo yote hayo, lakini inapotokea kwamba sasa utekelezaji, inabidi mtu arudi kwenye sheria mama na huo siyo mgongano hata kidogo, ni kwamba amelindwa kwa Katiba, basi! Lakini, hatuwezi kwenye kila sheria tukasema lakini ikifikia hapo usimhoji huyu, ukifikia hapo usimhoji huyu, sheria zitakuwa ngumu sana

kuandika. Nakubaliana na wewe, nina hakika Mheshimiwa Mohamaed Rished Abdallah, umeiona hiyo hali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 14

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza tu marekebisho madogo pale kwamba ripoti baada ya kupelekwa kwa Rais, ripoti nyingine iwe *tabled* mbele ya Bunge. Narudia hoja zile zile ambazo nilizieleza awali kwamba tunavyosaini hizi *Convention* na kuzi-*ratify,* ina maana kwa maana moja au nyingine kuna vitu ambavyo ni vya msingi tuviingize. Sasa ukiangalia *Article 3(3)* ya *AU Convention* na *Article 2(5)* ya *AU Convention* inazungumzia kabisa ushirikishwaji wa moja kwa moja wa umma katika masuala mazima ya kupambana na *corruption*. Sasa Wabunge wanapokuwa ndio sehemu ya uwakilishi wa umma, wana kila sababu ya kushirikishwa katika mchakato huo mzima. Vile vile nije katika Ibara ya Katiba ambayo ni Ibara ya 63(2) juu ya jukumu la Bunge kuisimamia Serikali. Tumekuwa tukilalamika kwenye michango yetu kwamba Bunge halina meno, Bunge linaburuzwa, kumbe ni sisi wenyewe ambao tunakuwa tunashiriki kufanikisha hicho kitu ambacho tunakuwa tunakilalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napendekeza kama kweli tuko *serious* kupambana na hili janga la rushwa, ni vizuri ripoti isiwe siri kwa sababu ripoti kupelekwa kwa Rais maana yake inaishia huko huko, ni mpaka hadi Rais mwenyewe awe na ule moyo wa kusema sasa hii ripoti niipeleke kwenye *public*.

Kwa hiyo, mimi hoja yangu inabaki vile vile kwamba kuna umuhimu wa kuongeza Bunge, ripoti iletwe Bungeni kwa sababu hii ni vita yetu sote. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri aniambie kwa nini anaona hii ripoti ikiletwa Bungeni, kutakuwa na

madhara makubwa sana na anafikiri ni vipi kama hii ripoti ikipelekwa kwa Rais, suala zima la kupambana na rushwa tunaweza tukalifanikisha? Nashukuru!

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kumjibu Mheshimiwa Halima Mdee, naomba nitoe maelezo ya aina mbili:-

Maelezo ya aina ya kwanza ni kwamba bado tunarejea kwamba tunaongelea juu ya taasisi za Serikali na tuna utaratibu wetu wa kuleta taarifa Bungeni. Hata sasa hivi tunapoongea, tunasubiriwa na Kamati za Bunge tutoe taarifa za vyombo hivi na katika Kamati mimi nilishasema mara kadhaa, hivi kuna dosari katika utaratibu huu wa sasa. *Is there any defect?* Kama kuna *defect, how do you like us to rectify it?* Kwa sababu kunakuwa na mjadala wa kina kabisa wa shughuli za vyombo hivi katika ngazi ya Kamati.

Pili, kwa kutambua yale aliyosema sasa kwa sababu tumeridhia Mikataba ya Kimataifa na tumekubali kwa dhamira safi yaliyoko kwenye Mikataba ile, ndio maana na yeye atakumbuka kama Mjumbe wa Kamati katika Ibara mpya ya 48, zile taarifa za fedha na masuala ya wakati bajeti kwamba *upon receipt* pale tumeongeza Ibara ndogo ya 4 katika Ibara ya 48: *"Upon receipt of the report, the Minister shall lay the report before the National Assembly during the sessions immediately following the date of submissions of the report.*. Hii ni taarifa ya fedha kama taarifa zingine ambazo tunazileta Bungeni na wakati huo, hamna Mbunge anayewekewa mipaka na huu utaratibu unakidhi hali ya sasa ya taasisi ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, kwanza, pendekezo lako sasa nimelisoma, naona lina kasoro hili. Unasema; "cha ku-*table* hapa Bungeni kiwe ni *executive summary." That is a further restriction!* Kwa hiyo sioni kama hii inasaidia sana. Afadhali hata hiyo anayoisema Mheshimiwa Waziri ina-*open the whole report* kuliko *executive summary, surely!*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

**ND. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Part 3* katika Muswada wa mwanzo imefutwa. Kwa hiyo, tunaanza na *Part 4* kwa maana ya kifungu cha 15. Lakini kabla ya hapo, Mheshimiwa Halima Mdee amewasilisha marekebisho ya ku-*reinstate* kifungu cha 15.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee, tulikuwa tumefuta hiyo ili kusiwe na Bodi kabisa, lakini naona una mawazo mengine. Hebu eleza!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudia dhana ile ile nzima, kwanza labda kabla sijaongea chochote, kwa sababu ni kweli Bodi ilikuwepo na mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati, hoja ilikuwa ni *composition* ya ile Bodi. Sasa labda ni vizuri tungepewa taarifa kujua ni kipi kilichopelekea ikafutwa kabisa kwa sababu hoja ilikuwa ni *composition* na tukasema kwamba kwa vile wote ni *Presidential*

*appointee,* itakuwa ni ngumu sana kufanya kazi zao kwa uhuru. Sasa ni kitu gani kilichopelekea hii Bodi kufutwa kwa ujumla wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nikirudia hoja zile zile za *convention* ya *Article 12* ya *AU* na *Article 13* ya *AU* inataka ushirikishwaji wa *NGOs* na jamii kwa ujumla. Sasa huu Muswada unavyokuwa unakuwa kama vile ni Muswada wa watu wachache, *at least* kwenye Bodi ndio ilikuwa ni fursa pekee kwa hawa watu wengine kupata nafasi ya kwenda kushiriki moja kwa moja na kushiriki *indirect*. Kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri aniambie, kwanza ilikuwepo na kwa nini iliondolewa, au ile hoja ya kutaka jumuiya za kiraia ziongezwe ndio iliwashitua sana, au vipi. Naomba anipe maelezo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Muswada huu ulichambuliwa kwa kina na taasisi mbali mbali. Mjadala wa wazi ulikuwa umeandaliwa na *APNAC* na ulihudhuriwa na wadau wengi sana. Katika mkutano huo wa *APNAC* mawazo yaliyoibuliwa mengi tena na viongozi wengine mashuhuri, nakumbuka Mheshimiwa Chipaka wa *TADEA,* Mheshimiwa Makaidi wa *NLD* na wengineo wakawa wanatuuliza, hivi chombo hiki kitafanyaje kazi! Hivi tunataka tuimarishe uhuru wa TAKURU au tunataka kuipunguzia uhuru? Na wengine wakaenda mbali, hivi Polisi utaiundiaje Bodi! Kwa sababu majukumu ya utendaji, majukumu yale *operational independence,* Bodi wala mtu yeyote hata Waziri hawezi kuingilia. Kwa hiyo, hata hii Bodi pengine kama ingekwepo, bado wangekuwa ni wateja kama wanahisiwa kwamba wanapokea rushwa. Hata Waziri alipo sasa hivi, anaweza kuwa ni mteja wa TAKURU kama anashitakiwa anakula rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mjadala huu ulikuwa ni mrefu na ilibidi tukatafakari upya, hivi Bodi hii kazi yake hasa nini, kwa sababu hatimaye Taasisi ya Serikali ina utaratibu wa ajira, utaratibu wa fedha na katika utendaji kazi wa siku hadi siku za uchunguzi na mashtaka, haiwezi kuingiliwa. Tukadhani basi, muda haujafika wa kuwa na Bodi kama hii, itakosa kazi na pengine ndio uhuru utakaohitajika kwa sababu sasa watakutana tu na *DPP* na uzoefu wetu wa miaka zaidi ya 40 kuhusiana na masuala ya rushwa ni mara chache sana kuna masuala yanamfikia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hali halisi wigo wa uhuru umepanuka zaidi na ndio maana pengine Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, akasema sasa uhuru huu baadae si unaweza ukatumiwa vibaya, pengine uwe na nafasi ya *DPP* hata katika mazingira mapya ambayo tumempa, akikaa na mashauri siku 60, basi aseme sababu au sheria ichukue mkondo wake. Sasa ndio ilipotufikisha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatukuishia hapa, Muswada huu ukiusoma sana, unatakiwa umilikiwe na raia na ndio lengo la kuleta Muswada huu. Sasa na pale kwenye *APNAC* na kwa wadau, kilichokuwa kinajitokeza ni kwamba Muswada kumilikiwa na wananchi, sio lazima kuwe na Bodi na ndio maana tunapoongea sasa hivi, bajeti ya Serikali, bajeti ya *Development Partiners* katika eneo hili ni bajeti kubwa na inaelekezwa kwa taasisi za kiraia inafuata taratibu na mikakati ambayo tumekubaliana Serikalini na wadau wa maendeleo na mkakati unaoitwa *The National Anti-Corruption Strategy Action*

*Plan* awamu ya pili *(NASCAPE II)*mwaka 2006 hadi 2011. Hapa ndipo tunataka kuunda chombo kinachoitwa *Anti-Corruption Forum,* hapa raia watapata nafasi ya kujadili kwa kina hali ya rushwa nchini, watajadili kwa kina mwelekeo wa nchi yetu katika mapambano haya na kadhalika. Kwa hiyo, tumeona bora kuwe na *Forum* ambayo itakuwa sehemu ya *NASCAPE II* na haya tuliyaongelea kwa kina nilidhani Mheshimiwa Halima Mdee pamoja na wenzangu wote watakumbuka kwa nini tumefikia hatua hii, ni baada ya kutafakari sana maoni ya watu mbali mbali na hali halisi ya taasisi hii kama taasisi ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Dr. Slaa, kaeni kwanza. Unajua mjadala huu unanikumbusha hadithi ya Bwana mmoja amebeba mbuzi begani halafu anataka kuvuka mto. Alipomfunga mbuzi kamba, akaambiwa yeye ni mkatili, alipombeba begani ili avuke mto, akaambiwa yeye ni mjinga kweli, mbuzi ana miguu minne halafu wewe unambeba begani! Alipofika kwenye mto anataka kumpa mwanaye ndiye abebe mbuzi, wakasema wewe ndiyo mkatili kabisa, kwa nini huyu mbuzi unambebesha mwanao! *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, mimi nadhani katika kimoja ambacho tunaweza kuipongeza Serikali, ni kurejesha *Operational independence* ya chombo hiki kipya. Sasa hata kuleta sura mpya ya aina ya Bodi, haitusaidii. Mimi nadhani wote sisi tukubali, tuwe ni wateja wa hiyo TAKURU mpya, basi tusiwe tena tunapitia kwenye Bodi, una-*lobby* kwa Katibu Mkuu, una-*lobby* kwa *NGO,* ndio maana yake. Huyu Bwana Mkubwa au Bibi, *whoever it will be*, aendelee, afanye kazi yake bila kushauriwa tena na chombo kingine ambacho kikae kati kati. Kweli tunataka kurudi tena tuweke Bodi, tuanze kukubaliana nani waingie, sijui! Labda Mheshimiwa Halima Mdee kwanza na Wabunge nawajua hampendi urasimu. Nyie mnataka urasimu! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri ya jinsi *Civil Society* zitakavyokuwa zinashirikishwa. Nilichotaka kusimama kusema, kwa sababu mimi hofu yangu ilikuwa hivyo na kumwambia kwamba kwenye *APNAC* sikuwepo, nilikuwa Tunduru. Kwa hiyo, inawezekana hivyo anavyovisema, mimi sikuvisikia. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Pole sana! Nilitaka tu kusema kuhusu Tunduru, nasikia sehemu zingine mito imejaa na inabidi mpite katika hali ngumu kidogo na wewe Mheshimiwa Halima Mdee, uliweza? *(Kicheko)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mfano wako ulioutoa, nadhani ni mfano mzuri. Lakini, kwanza nipende kuweka *record* sahihi, mimi bahati nzuri ndiye Katibu Mkuu wa *APNAC* na mimi ndiye niliyewasilisha Serikalini mapendekezo ya wadau waliotokana na mkutano wa *APNAC*. Sasa kwa bahati mbaya Waziri ame-*quote* mifano ya mtu mmoja mmoja walioeleza hisia zao. Lakini, taarifa ya mwisho iliyokuwa *summed up* na Profesa Kabudi, ambaye alikuwa *rappotuer* wetu ambayo mimi ndiye nikaja kuiwasilisha, haikusema hivyo. Taarifa ya Kabudi inasema wangependa mfumo wa Bodi hata kama utabakia ulivyokuwa umependekezwa kwa maana ya kwamba *in case* Serikali itang'ang'ania jinsi ilivyokuwa, lakini kuwe na

wadau wafuatao, *Civil Society* na iongezwe pia ipanue madhehebu ya dini. Sasa, mimi nafikiri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa mujibu wa kanuni, aliye-*move amendment* karidhika amekaa. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea na hayo unayoyasema. *(Makofi)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yangu ambayo nimeomba Bunge hili liweze kuyakubali yanahusiana na suala la rushwa katika uchaguzi na suala la rushwa katika siasa. Hapa nina *executive summary* ya Tume ya Jaji Warioba, ambapo anasema katika moja za kurasa za *paper* hii kwamba; *"Members of Parliament have offered bribes to voters in order to be elected."* Mheshimiwa Jaji Warioba anaendelea kwa kusema kwamba; "*some of the top leaders had already been compromised and were deeply involved in corruption. These problems are rose for the following reasons,"* kuna sababu nne na sababu ambayo mimi ningependa kui-*quote* ni *appointment of corrupt leaders* na *erosion of integrate* ya *leadership. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Rais Jakaya Kikwete alipohutubia siku ya kuzindua Bunge alisema maneno yafuatayo katika ukurasa wa 9 wa Hotuba ya Rais Kikwete; "yameanza kujitokeza mawazo pamoja na kuanza kujengeka utamaduni kuwa uongozi unaweza kununuliwa. Tusipokuwa waangalifu nchi yetu inaweza kuwekwa rehani kwa watu wenye fedha za kununua uongozi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kuomba sheria hii ya rushwa iweze kuwekwa vipengele ambavyo vitaweza kuifanya taasisi ya kuzuia rushwa iweze kushughulikia makosa katika rushwa za kisiasa na katika rushwa za kiuchaguzi.

Kwa hiyo, sasa katika kifungu cha 20 (1) yaongezwe hayo maneno ambayo *clause 20 (a)* na pia ili kuiwezesha *clause 20(a)* iweze kuwa na nguvu za sheria na iweze kuwa rahisi kwa watu wanaosoma sheria, naomba iongezewe *margin* itakayosomeka; *"Corruption in political activities and electoral processes."*

Vile vile pawepo na *clause 20 (b)* ambayo sasa itaweza kusomeka; *"Application of Act number one of 1985," Act number one* sheria ya uchaguzi na *Act number 5 of 1992* na *Act number 5* ni sheria ya Vyama vya Siasa. Utakapoweka haya maana yake ni kwamba tutakuwa tumetoa mamlaka kwa *PCB* kuweza kuingilia kesi zinazohusiana na rushwa katika uchaguzi na vile vile na rushwa katika siasa. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumetekeleza kwa dhati kabisa hotuba ya Rais Jakaya Kikwete, aliyoitoa hapa katika Bunge hili Tukufu siku ambayo anazindua tarehe 30 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimuombe Mheshimiwa Waziri akubaliane na haya mabadiliko ili sheria hii iweze pia kushughulikia rushwa katika uchaguzi na rushwa katika vyama vya siasa. Hili halihitaji mabadiliko ya Katiba ni suala la *application* ya sheria. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabwe Zitto, amenukuu taarifa ya Mheshimiwa Jaji Warioba, kwa hakika Muswada huu unatekeleza yale maagizo ya taarifa ya Jaji Warioba kwa sehemu zile ambazo zimeelekezwa kwa sheria ya mwaka 1971 ya kuzuia rushwa. Tujue hilo kwamba mapendekezo yale yaliyoelekezwa ya kurekebisha sheria ya rushwa mwaka ya 1971 haya ndiyo matokeo yake.

Sasa kwa upande wa zoezi la uchaguzi, mazoezi ya uchaguzi ya siasa, chaguzi za Serikali za Mitaa, chaguzi za Serikali Kuu. Nirejee tena wakati na-*windup* kwamba eneo hili, ni eneo pana sana. Mimi katika kusoma na katika kutembea duniani kote sijawahi kuona sheria ya rushwa ikitekeleza mambo yote yanayohusiana na uchaguzi. Huwa kunakuwa na sheria ya uchaguzi na kunakuwa na chombo rasmi kinachosimamia masuala yote ya uchaguzi. Imekuwa hivyo hapa kwetu na ni hivyo katika nchi za Jumuiya za Madola, ambazo sheria zote zinafanana na zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia busara hiyo basi na pia kwenda ndani zaidi pengine ndio maana Mheshimiwa Rais, akaagiza kuwe na mjadala wa Kitaifa katika eneo hili pengine tutaibua mambo makubwa na mazuri zaidi ili tuwe na chaguzi bora zaidi kuliko ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema pale awali kwamba hapa tungependa tutatue tatizo la rushwa katika uchaguzi ambalo hatukatai kwamba liko, liko, tulitatue kutoka kwenye mizizi, unapata wapi fedha, nani anakupa. Ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zitto, anatembea sana duniani bila shaka sasa hivi na pengine nitumie taarifa ya leo ya

Amerika kwa Chama cha *Democrat* leo nafikiri Obama na Hilary Clinton kila mtu amefikia dola milioni 70 kuchangisha fedha kwa taratibu zinazojulikana kwa kutumia sheria ya uchaguzi ya Amerika, sasa tunataka tuelekee huko kwamba tuwe na sheria moja ambayo itaenda kwa undani zaidi katika eneo hili. Hamna anayependa viongozi wanaonunua kura, hatupendi. *(Makofi)*

Sasa kama sheria hiyo itataja Mkurugenzi wa TAKURU atahusika moja kwa moja na atakuwa shahidi kwenye mashauri yatakayotokana na malalamiko ya uchaguzi tutafika huko. Kwa nini tuanze kujaribu kuvuka mto ambao hatujaufikia? Kwa hiyo, mimi nadhani busara ya Mheshimiwa Rais, bado ni ya msingi kwamba tuibue mjadala wa Kitaifa hatimaye tuwe na sheria ya uchaguzi ambayo inakwenda kwa undani zaidi kutatua matatizo ya uchaguzi katika nchi yetu na itabadili sheria ya sasa uchaguzi kwa vyovyote vile na pia Sheria ya Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu kaeni nifafanue kidogo kwa sababu ni vizuri niwe nafanya hivyo. Nimetazama mapendekezo ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, hapa kuna vipengele vitatu tu. Halafu wakati huo huo tunazungumza wote kwamba tatizo la rushwa katika Vyama vya Siasa na katika chaguzi ni kubwa sana. Sasa tujiulize kwa njia hii ya kuweka vipengele hivi vitatu kweli tunakidhi haja ya jinsi tatizo lilivyo zito? Kwa sababu ukitazama alichoomba Mheshimiwa Rais, anataka eneo lote la *election funding* mpaka kuishia sasa kwenye chaguzi zenyewe na *political parties funding* litazamwe vizuri. Isitoshe Uchaguzi Mkuu ni mwaka 2010. Ukizingatia yote hayo mawili kuna kazi ya kufanya ya kushirikisha jamii, wapiga kura na sisi wenyewe tutafakari vizuri tukaja na sheria maalum ambayo kipengele kwa kipengele inagusia yote hayo, itakuwa ni bora zaidi, tukiweka hivi vitatu bado kutakuwa na utata kwamba aliwapa chai wasaidizi wake, aliwapa *campaign team* na nini. Mimi nadhani TAKURU ina *agenda* ya kutosha katika yale mambo mazito sana yanayoendelea hivi sasa ambayo yanahusu uchumi. *(Makofi)*

Lakini kwenda sasa tupachike tu kwa haraka haraka vipengele vitatu tuseme ndio tunashughulikia jambo gumu kama uchaguzi mimi nadhani kweli tutakuwa hatufanyi jema hata kidogo na tutapata tatizo tu. Tutajidanganya kwamba tumetatua kumbe bado kabisa. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, nadhani tunahitaji sheria mahususi ikashughulikia rushwa katika siasa kwa maana ya uchaguzi na vyama. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na maelezo, ni maelezo mazuri sana. Lakini utamaduni tulionao ni utamaduni wa kutoenzi *commitments* na huu umekuwa ni utamaduni wetu, ni wa kawaida na ni lazima tubadilike tuweze kuenzi *commitments*. Madhumuni hasa ya kuweza kuweka vipengele hivi siyo kwamba naliona tatizo la rushwa kwenye uchaguzi mdogo, ni tatizo kubwa sana. Mheshimiwa Rais, amelizungumzia na ni kweli Mheshimiwa Rais, alizungumzia masuala mazima ya mjadala wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utakumbuka katika Mkutano wa Pili wa Bunge, nilimuuliza Mheshimiwa Philip Marmo, kuhusiana na huu mjadala wa Kitaifa utakuwa lini, akasema hivi karibuni. Sasa hivi anavyozungumza anasema hivi karibuni. Hivi

karibuni inaweza kuwa mwaka 2010 na inaweza kuwa mwaka 2015, kwa sababu hakuna *commitment* ya hivi karibuni. Lengo la kuweka haya ni kuhakikisha kwamba *PCB* mjadala wa Kitaifa utakapofanyika mpaka hapo sheria mpya itakapofanyika itaweza kuwa na mamlaka ya kushughulikia masuala ya rushwa katika uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikukumbushe tu juzi tumetoka kwenye uchaguzi Tunduru haina maana kwamba uchaguzi lazima mwaka 2010 hapa katikati siombei yatokei hayo lakini kuna chaguzi ndogo zinatokea za Madiwani, za Wabunge, za Wenyeviti wa Vijiji, kwa hiyo, ni lazima tuwe na *provision* sasa hivi kabla ya mjadala wa Kitaifa ambayo itaweza kuhakikisha kwamba tunalishughulikia suala la rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba tunapoweka hii *provision* Waheshimiwa Wabunge, tunakuwa tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais, katika vita dhidi ya rushwa na wala haiharibu lolote lile katika mjadala wa Kitaifa. Lakini nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kwamba tunapokataa kuweka *provision* inayozungumzia rushwa katika siasa na rushwa katika uchaguzi maana yake ni kwamba tunawaambia Watanzania sisi tunatoa rushwa. Tunawaambia Watanzania kwamba sisi tunachaguliwa kwa mujibu wa rushwa. *Commitment* pekee ya kuwaonyesha Watanzania kwamba sisi tunachukua rushwa ni kuweka hivi vipengele. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *is just our own decision,* tuamue tunajiua namna gani kwamba tunawaonyesha Watanzania na wanatuona sasa hivi kwamba sisi hatutaki *PCB* isihusike na sisi tusiwe wateja wa *PCB* au tuwe wateja wa *PCB it is our own decision*. Tuamue leo na Watanzania wanatuona. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba ni-*move* kwamba vipengele hivi Serikali iviingize kwenye sheria kama *commitment* yake kwa ajili ya mijadala itakayokuja inayohusiana na *campaign financing* na *funding* ya *political parties* kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais, alipendekeza katika hotuba yake alivyotuhutubia kuzindua Bunge tarehe 30 Desemba, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nitaomba mwongozo wako kwamba hili lifikie katika upigaji kura. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako kama baada ya majibu ya Waziri na iwapo hatakubaliana na hiyo *commitment* tupige kura ili tuweze kuamua. *(Makofi)*

**MHE. JOHN. M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kwamba ni vigumu sana kubishana na Spika anapotoa mawazo mazuri kwenye Muswada kama huu. Lakini pia ni wajibu wetu kama Wabunge kuweza kuhakikishia wananchi kwamba Tanzania kama vile *preamble* inavyosema ya Muswada kwamba hatutaki rushwa ya aina yoyote. Tukipiga hapa kura tunasema lakini rushwa ya kisiasa inakubalika basi hili lina *water down* Muswada wote na dhamira yetu ambayo tumesema tutaifanya Tanzania iwe mahali ambapo hakuna rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa tu siyo wakati wa uchaguzi, rushwa sasa hivi tuna vyama ambavyo wanachama wake wananunuliwa kiwazi wazi. Siyo mambo tu ya kungojea uchaguzi. Kuna wafanyabiashara mimi sitaki kutaja majina hapa ambao wanajitolea *up to a level 15 to 20 million shillings* kumnunua mwanachama aende

akatangaze mbele ya Rais kuwa mimi nimetoka chama hiki naenda chama hiki. Inafanywa *with impurity,* yaani mtu anafanya wazi na anajivuna na matokeo yake ya kufanya hivyo tunayaona mara huyo mtu anapata *contract* aidha, na Halmashauri au mtu huyo anapata *contract* na Serikali. Sasa tunakataza nini na tunakubali nini?*(Makofi)*

Tunajua pia kwamba hata wakati wa uchaguzi kuna watu wengi ambao wanachangia siasa na zaidi wanajihusisha zaidi na chama ambacho wanafikiri kitashinda, najua sitaki kukisema hicho chama lakini wanachama wengi wanajua hapa ni nani wanaoshinda kila wakati. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale mara moja unaona kwamba Kampuni hiyo inayotoa mapesa kibao mara nyingine mpaka tumeona *figures* zinafikia karibu bilioni moja, kufanikisha uchaguzi aidha wa Mbunge au wa nani. Sasa kama Bunge hili kwa kauli moja kabisa lisipokataa sasa hivi mambo hayo tunafanya nini katika kutunga sheria hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono kabisa katika kutunga sheria hii. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakupongeza sana kwa jinsi ulivyoongoza sheria hii mpaka hapa tulipofika, nakupongeza sana kwa busara zako. Lakini pili, niipongeze Wizara na hasa Mheshimiwa Philip Marmo na viongozi wa *PCB* kwa jinsi walivyoshirikisha watu wengi sana wa kutosha kwenye kutunga sheria hii. Niwashukuru rafiki zetu wa Upinzani kwa michango yao na umakini wao katika suala hili, tumefurahishwa sana na jinsi ambavyo wamekuwa wamejiandaa. *(Makofi)*

Lakini tusiwekeane maneno ya kushitakiana. Sisi na Mwenyekiti wa Chama chetu ndiyo aliyekwenda hadharani na kusema tunalichukia suala la rushwa na tutalishughulikia kikamilifu. Sasa Mheshimiwa Mbunge anaposema hakuna *commitment,* hatuna hakika, unataka uhakika gani zaidi ya haya tunayoyafanya hivi sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo sheria hii imepata mjadala mkubwa nchini na mjadala mzuri tungetaka vile vile suala la uchaguzi na sheria ya uchaguzi na upatikanaji wa fedha upate mjadala wa kutosha ndani ya nchi yetu. Tupate utaratibu ndani ya vyama vile vile ili tuanze kuulizana baadhi ya fedha wanapata wapi na kama zinakubalika. *(Makofi)*

Sasa tusiuogope mjadala, tuusubiri mjadala, tuwashirikishe Watanzania wote ndipo tuje na sheria hapa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuhakikishia kwamba Serikali ya CCM imejianda kabla ya uchaguzi unaofuata tutakuwa tumekuja na sheria ya uchaguzi inayokidhi mambo haya ambayo tunayajadili hivi sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani kwa tamko hilo la Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na inajibu nadhani hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba hakuna

*commitment.* Sasa Kiongozi wa Shughuli za Serikali amesema wazi kabisa kwamba jambo hili linashughulikiwa na ametaja *time frame.* Je, bado Mheshimiwa Kabwe Zitto unalo lingine la kusema?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru pia kwa maneno ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Lakini naomba kwamba Bunge letu litambue kwamba Rais Jakaya Kikwete ni Rais wa Watanzania wote. Siyo Rais wa wana CCM peke yake. Amechaguliwa kwa kura milioni 9 CCM wana wanachama milioni tatu tu. Kwa hiyo, sisi pia *as a head of state* na tunampomzunguzia Rais Jakaya Kikwete, tunamzunguzia Rais wa Tanzania, hatuzungumzii Mwenyekiti wa Taifa wa Chama na sisi tuna Wenyeviti wetu. Kwa hiyo, tunapozungumzia kutaka *commitment* ya Rais itekelezwe tunazungumzia kama Watanzania na tunataka itekelezwe. Nashukuru kwa maneno ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba kabla ya uchaguzi ujao. Lakini ni *commitment* ambayo ni *general* sana. Ndiyo ukweli huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea ni haki yako ingawa kama unavyoona ukizisoma dalili za nyakati unaanza kuwakera wenzio. *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunieleza hayo lakini, sijali kumkera mtu yeyote ambaye siyo mpiga kura wa Kigoma Kaskazini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo ukweli huo mimi nimeletwa na watu wa Kigoma Kaskazini ndiyo nawajali kwamba naweza kuwakera, sana sana watu wa Chama changu. Kwa hiyo, mtu mwingine kama namkera kivyake vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ni-*move* hoja ambayo iwapo mkono na Wabunge kumi tutakuomba tupige kura kuhusu suala hili. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hatujafika hatua hiyo hata kidogo na pia kuhusu hilo alilosema Mheshimiwa Kabwe Zitto, amekosea kabisa Kanuni yenyewe. Kanuni hiyo haihusu Bunge katika Kamati ya Bunge Zima inahusu Bunge lenyewe nikiwa kwenye kiti pale.

Kwa hiyo, kilichopo hapa ni Kanuni ya 72 (4) ambayo nitawahoji kukubali au kukataa kwenye Kamati. Sasa nitawahoji wanaokubali kwamba mapendekezo ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, yaingie waseme ndiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Basi ni dhahiri ameshindwa kwa hiyo hayaingii. Kifungu hicho maana yake sasa kimeafikiwa kama kilivyo. Tunaendelea na kinachofuata. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 23

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo na mjadala ulitokea kwenye kifungu cha 20 na baada ya Serikali kutoa *commitment* yake kupitia kwa msimamizi wa Serikali Bungeni na mimi kwa sababu kifungu hicho kilikuwa kinazungumzia suala zima la *election*. Nimekubaliana na Waziri tukipe hiki kipengele kama Rais alivyosema ndiyo huyo huyo aliyeeleza kwenye Bunge wakati wa ufunguzi wa Bunge jipya tukipe kipengele hiki muda. Siyo muda lakini Watanzania wengi washiriki. Mimi Mwenyekiti wa *APNAC* nitafanya utaratibu ule ule kuwasaida Watanzania washiriki. Baada ya kusema hivyo, hilo nimeliondoa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 35

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri akiwa anajibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, marekebisho hayo ambayo nilikuwa nimeyapendekeza ameyafanyia *consideration* kwa hiyo, naondoa mapendekezo haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 47

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 48

**MHE. DR. WIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu ufafanuzi, kwanza nakubaliana na namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwamba ameingiza suala la taarifa ya *PCB* sasa kuingia Bungeni. Sasa kwenye Kamati tulikubaliana kwamba marekebisho isiwe tu ni ku-*lay on the table* iwe *to lay and debate* kwa sababu kwa taratibu zetu za Bunge, uki-*lay* siyo lazima zijadiliwe mpaka Mbunge aombe kujadiliwa. Sasa je, kuna sababu yoyote ya kutokuweka neno ku-*table and to debate*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiawa Dr. Slaa, wewe ni mzoefu, utaratibu ni kwamba kwa hoja maalumu tunaweza tuka-*debate* lakini siyo lazima kila kinachokuwa *tabled* kiwe *debated* kwa sababu kila siku kama mnavyoona tuna-*table* vitu vingi sana taarifa za Mashirika na mamia ya mimia *pigeon hole* zinajaa. Sasa itakapofika wakati na inahitajika ku-*debate,* Spika ataangalia uzito wa jambo. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja na ndiyo kwa sababu hatupendi kila kitu kilichokuwa *laid* kiwe *debated* au kiombwe ni kwa sababu hiyo kwa kukwepa hiyo unayosema ndiyo maana tulitaka hii taarifa rasmi iweze kuwa *debated* bila Mbunge kusimama na kuiomba.

Leo sisi tunaopitisha sheria hii tunaijua hiyo, mimi kama ulivyosema ni mzoefu lakini siyo Wabunge wote na kila baada ya muda fulani Wabunge, wanaingia wapya hawajui hizi taratibu. Lakini ukisema tu *lay and debate* maana yake *automatically* inakuwa *laid* na *automatically* inakuwa *debated*. Sasa hayo ndiyo tuliyokubaliana nilitaka kujua kumetokea nini na kuna tatizo gani na kwa nini baada ya marekebisho hilo halikuwekwa?

**MWENYEKITI:** Sasa hapo Mheshimiwa Mbunge unaingilia Kanuni za Bunge. Suala *whether* liwe *debated* au vipi ni uamuzi wa Spika, siyo uamuzi wa Serikali. Kwa hiyo, ukisema sasa liwekwe sasa kwenye sheria utakuwa unaweka sheria ambayo inalazimisha mabadiliko ya Kanuni ambayo kwa shughuli zetu Kibunge hilo siyo sahihi na mimi napenda nieleweke ni Spika ninayetenda haki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama kweli kutakuwa na jambo ambalo linaonekana lina uzito, isije ikawa kila mtu imepotea shilingi 500 *PCB* wanafuatilia basi tuna-*debate* hayo itakuwa Bunge la ajabu, lakini kama kuna jambo la maana, mmeona baadhi ya mambo ambayo tunaweza ku-*debate* nadhani mmwamini Spika, mwachieni ikifika tutafanya. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49

Kifungu cha 50

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 51
Kifungu cha 52

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 57

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 58
Kifungu cha 59

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif.ungu cha 60

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hiki cha 60 nimeomba yawekwe mabadiliko yanayosema kwamba basi *DPP* akipelekewa *investigation* iliyofanywa na TAKURU tumpe muda wa siku 60

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Dr. Zainab Gama samahani nitakuruhusu tu uendelee. Lakini kifungu cha 60 nadhani mnaleta pendekezo jipya. Kwa sababu 60 iliyopo ni ku-*repeal.* Kwa hiyo, kama una-*introduce another factor* basi itakuwa kifungu cha 57, ni kwenye kifungu cha 57, uzungumzie kifungu cha 57 siyo kifungu cha 60 ambayo tumekwishaipitisha, sasa lakini nadhani *schedule of amendments* imetubabaisha.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Hapana Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki nimesema naomba niisome kama nilivyoandika: *"By deleleting clause 6*

*and substituting for it the following accept for the offense under Section 16, prosecution of the offence under this Act shall be instituted with written consent of the Director of Public Prosecution made within 60 days from the day he or she received from the offence from the Bureau." Second, "where the Director of Public Prosecution refuses to give consent under Section One, he or she must give reasons" and third, "if the Director of the Public Prosecution fails to give consent within 60 days it shall be taken that the consent has been given and the Bureau shall prosecute the offence."*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi. Nadhani ni lazima niruhusu tu kwa sababu iliyokuwa kifungu cha 60 kwenye Muswada ndiyo kifungu cha 57 sasa. Kwa hiyo, wenzetu waliokuwa wanaandika zile *amendments* siwezi kuwa-*penalize* kwa hiyo, kwa sababu namba zimebadilika baada ya kuondoa ile sehemu ya tatu. Ikatupunguzia vifungu vitatu. Kwa hiyo, sasa kwa kweli ni kifungu cha 57 ambacho kinasomeka kwamba; *"Accept for offences under Section 16 Prosecution for an offence and this Act shall be instituted with written concern with the DPP."*

Sasa naona pendekezo hapa la mabadiliko ni kuongeza kwamba huyo *DPP* asilikalie jalada au sivyo Mheshimiwa Dr. Gama? Unasema ndani ya siku 60.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilisema ndani ya siku 30, lakini naomba niungane mkono na Mheshimiwa Dr. Gama siku 60. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa ili tuliingize badiliko hili itabidi, ama kuna maelezo ya Serikali, samahani.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kwa mchango wake. Lakini kwa uandishi wa sheria ningependekeza haya maneno *he or she* yasiingie katika sheria. Kwa sababu tunaongozwa na sheria za nchi hii katika kutafsiri sheria na neno *he* kwa mujibu wa sheria za nchi yetu inajumuisha pia *she.*

**MWENYEKITI:** Kwa lugha ya Kiingereza kisheria wanasema *he embrasses she.* Kwa hiyo, pendekezo la ...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunakubaliana na pendekezo hili kwa sasa. Lakini katika kuliandika ili iwe sehemu ya Muswada huu na sheria hii baadaye tutajitahidi isigongane na Katiba. Kwa hiyo, yale aliyosema Mheshimiwa Dr. Zainab Gama tutajaribu kuya-*take* lakini isitufikishe kwamba sheria itakuja kupingana na Katiba baadaye. Ile siku 60 tuna hakika tunahakikisha kwamba haipingani na Katiba kwa hiyo, itakuwa hivyo, lakini yale maneno yote aliyoyasema tutajaribu kuya-*catch* isipokuwa pale tu maneno yale yatakapopingana na Katiba. Tumwachie Mwandishi Mkuu wa Sheria eneo hili kwa sababu yeye ndiyo anafahamu zaidi tafsiri ya sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, nadhani ni sahihi kusema baada ya Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi huo ambao unaikubali siku 60 kama haigongani na Katiba basi

tuichukulie kwamba hii tunaikubali kama *amendments* kwenye *stage* ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo kama jinsi nilivyosema hapo mwanzo kwamba nimekubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ya kwamba ni siku 60. Mimi nilikuwa napendekeza siku 30 nilivyosema hapo mwanzo na jinsi ambavyo niliandika nadhani Mheshimiwa Waziri anayo *schedule* ya *amendments* nadhani inaendana kabisa na jinsi ambavyo Mwanasheria Mkuu Mstaafu wa Serikali ambaye sasa ni Waziri wa Miundombinu amezungumza na vile vile katika mapendekezo yangu hayo hayo kama ambavyo yako hapo mezani tumeweka ku-*take into consideration* wasi wasi wa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Katiba.

Nimesema hapa kwamba *a new sub-clause four* yaani *sixty four to read as in exercising the power granted under clause 61; the Director of Public Prosecutions shall conform to Article 59(b)* ibara ndogo ya (iv) (a), (b) na (c) *of the Constitution* kwa hiyo nimefanya *application on the Consititution* katika hilo ili kuweza kuondoa wasi wasi ambao Mheshimiwa Waziri ameutoa na hivyo basi kwa kuwa Kamati kimsingi tumekubaliana siku 60 nilikuwa naomba sasa Mwenyekiti hizi *provisions* ambazo nimezi-*propose* hizi *provisions* ambazo nimezi-*propose* kwa kuwa zinaendana na mapendekezo ya Mawaziri wote na pia zinaondoa *worry* wa Katiba nilikuwa naomba ndizo zichukuliwe.

**MWENYEKITI:** Pamoja na tahadhari kuhusu, si rahisi tukajigeuza hapa tukafanya *the actual drafting* mimi nadhani kimsingi likishakuwa limekubaliwa hivyo, nadhani tuachie *the final drafting* kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**ND. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipitisha jinsi ilivyo katika hali ya kawaida inatakiwa iwe *reflected* kama inavyoonekana kwenye hizi *schedule of amendments* ambazo zimeletwa.

Sasa kwa sababu kuna *technicalities* za *languages* na uandishi, mimi nilikuwa nashawishika kwamba pengine mabadiliko haya yanakubalika lakini kwa maelekezo kwamba Mheshimiwa Waziri ayalete mabadiliko ambayo yataingia kwenye Sheria yenyewe ili kusudi yapitishwe na Bunge moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hata tukipitisha Muswada Mheshimiwa Waziri maana yake yale mabadiliko nayo neno kwa neno yaweze kukubaliwa na Bunge. Sawa sawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mabadiliko haya ambayo yameletwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama ambayo tunayajidili kwa kina na kuyakubali ni mabadiliko yale yale ambayo pia yameletwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini kimsingi ni mabadiliko ambayo tumeyajadili sana kwenye semina ya *APNAC*. Kwa hiyo,

tunafahamu *wording* yake. Isipokuwa sisi tumeenda mbali zaidi kuchukua tahadhari ili mabadiliko ambayo sasa yatachukua nafasi yasipingane na Sheria.

Nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa ni kama yako tayari na ninazo nakala za kusambaza. Kwa hiyo, ni sehemu ya Jedwali. Isipokuwa haijasambazwa kwa sasa kwa sababu ya hali halisi ya makubaliano tuliyoyafanya sasa hivi na mimi hapa nina dokezo la Mwandishi Mkuu wa Sheria na amenihakikishia kwamba...

**MWENYEKITI:** Ninamwona Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anataka kufafanua.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna-*propose* kwamba hiyo *amendment* iwe kama ifuatavyo, kile kifungu cha 57 kiwe na kifungu kile cha pili ambacho kitasema kama ifuatavyo: *"The DPP shall within 60 days give or withhold consent for prosecution." (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani safi hiyo, maana yake ama atoe ama aachie na ndiyo lengo nadhani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo, *schedule* imeshafutwa.

**MWENYEKITI:** Aah! Imefutwa

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imeshafutwa.

**MWENYEKITI:** Ile ndiyo ya Bodi kweli, basi haina maana tena. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeufikiria Muswada huu

na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo naomba Muswada wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2007 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, inayohusu kusomwa kwa mara ya pili na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2007 yaani *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007)* imeletwa mbele yetu, imetolewa na imeungwa mkono, kwa hiyo Muswada wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2007 *(The Prevention and Combating of Corruption Bill, 2007)* sasa umepitishwa.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo tumefikia mwisho wa shughuli za leo na hakuna muda wa kutosha wa kuanza Muswada wa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ambao tutauanza kesho. Kwa hiyo, kabla tu sijaahirisha Bunge naomba kukumbusha kwamba kesho saa saba na nusu mchana Kamati ya Uongozi yaani Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bungetuna Mkutano pale katika Ukumbi wa Spika kuzingatia mambo muhimu sana ya shughuli zilizobaki katika kalenda yetu ya Mkutano huu wa Saba.

Kesho kutwa saa saba na nusu mchana, Tume ya Huduma za Bunge tukutane kuzingatia mambo mengine muhimu sana kwa Wabunge. Natoa taarifa za awali kwa sababu vikao hivyo ni muhimu sana, tuhudhurie ili tuweze kukamilisha kazi zetu za Mkutano wa Saba vizuri.

Baada ya kusema hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.20 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 17 Aprili, 2007 saa tatu asubuhi)*